# Nipashe

Alhamisi Julai 25, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579979

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





## Mbaroni madai kumpiga trafiki ngumi na makofi

UKURASA 4




UKURASA 13

# Haijapata kutokea



• **Dhahabu** kilo 35 iliyotoroshwa yatua Ikulu, yamo mamilioni yaliyoibwa NBC miaka 15 iliyopita, JPM na Kenyatta walonga mubashara... *Endelea ukurasa 2 & 3*



Rais John Magufuli akisaidia kuhesabu vipande vya dhahabu, huku akishuhudiwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (kushoto), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (wa pili kulia), Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kulia) na Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya, Balozi Monica Juma (wa pili kushoto), Ikulu jijini Dar es Salaam jana. Dhahabu pamoja na pesa zilikamatwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi zikitoroshwa kutoka Tanzania. PICHA NDOGO: Makasha yenye dhahabu na fedha hizo, baada ya kuwasili na ndege maalum ya Jeshi la Kenya katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere, jana. **PICHA: IKULU**

## DC akana kuomba rushwa

UKURASA 4

## Wastaafu wenye pingamizi walipwa mabilioni ya mafao

UK. 4


TAIFA STARS vs KENYA

JULAI 28, 2019 • UWANJA WA TAIFA




HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18, TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

# JPM, Kenyatta walonga mubashara

**Na Salome Kitomari**

MARAIS John Magufuli wa Tanzania na Uhuru Kenyetta wa Kenya jana walitumia dakika sita na sekunde tisa kuzungumza kwa simu hadharani na kueleza jinsi wanavyoshirikiana kulinda rasilimali kwa manufaa ya wananchi wao.

Katika mazungumzo yao hayo, waliweka wazi kuwa kama wangekuwa viongozi walafi, wangegawana dhahabu na fedha za wizi zilizokamatwa na wangeitumia pasi na wananchi wa nchi zote kujua, lakini wamedhamiria kuwatumikia wananchi ndiyo maana waliamua kuzirejesha ili zisaidie upelelezi wa kesi na ni mali ya wananchi wa Tanzania.

Mazungumzo ya simu kati ya wawili hao yalifanyika wakati Rais Magufuli akipokea vipande 22 vya madini ya dhahabu vyenye uzito wa Kg 35.34 na fedha za Tanzania Sh. milioni 170, Dola za Marekani 77,500 na fedha za Kenya Sh. milioni 171,600 zinazodaiwa kuibwa Tanzania mwaka 2004.

Baada ya kupokea dhahabu na fedha hizo kutoka kwa wawakilishi wa Rais Kenyatta walioongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Monica Juma, Rais Magufuli kabla ya kutoa neno kwa waliohudhuria hafla hiyo Ikulu jijini Dar es Salaam, alianza kwa kumpigia simu Rais Kenyatta lakini hakupokewa na baadaye wakati anaongea, alibaini Rais mwenzake huyo alikuwa anamtafuta kwa simu na kuamua kumpigia.

Baada ya Kenyatta kupokea simu, alisema hakupokea simu yake awali kwa kuwa alikuwa kwenye kikao, kisha Rais Magufuli akamshukuru kwa ujumbe aliomtumia na kumweleza kuwa Waziri Monica amefikisha mzigo Tanzania. "Tulisema mali ya wananchi wetu lazima irudi kwa wananchi wetu, tunataka kuhakikisha yale ambayo wananchi wametupatia imani ya uongozi sisi ni kuhakikisha tunatenda haki, tunalinda na mali ya wananchi ijenge hospitali, barabara, shule na afya," Rais Kenyatta alisema huku akiitikiwa na Rais Magufuli aliyesema "safi kabisa".

"Walaghai hawana nafasi tena katika nchi zetu, tuendelee kushirikiana namna hiyo, Kenya na Tanzania hatuna mpaka, sisi ni kitu kimoja na lazima tuendelee kuwa kitu kimoja.

"Tusaidiane tuondoe umaskini katika nchi zetu. Kwa hayo machache Mungu akubariki, awabariki Watanzania wote tuendelee na ushirikiano, ujirani mwema.

"Vile tulizungumza tukiwa Chato, mtu anajitafutia marafiki lakini Mungu ndiye anakuchangulia, Mungu ametuchagua tuwe pamoja, lazima tuendelee pamoja," Rais Kenyatta alisema huku Rais Magufuli akiitikia kwa kusema "asante sana".

Rais Magufuli alisema undugu wa Kenya na Tanzania uko palepale na kamwe hakuna wa kuutenganisha, huku akiahidi wataendelea kupendana hadi maendeleo yapatikane kwenye nchi zote.

"Nimewaambia Watanzania, kama sisi wabaya dhahabu tungeikata moja kwa moja... Rais Kenyatta ni Rais mwenye moyo wa kizalendo, anawapenda Watanzania na Wakenya.

"Tungekuwa wabaya tungezungumza kwa sirisiri, hela wasingeiona, tungekata tugawane polepole, wangebaki kuandika kwenye magazeti lakini wasingeziona.

"Napenda nikuhakikishie wale wanaofanya mabaya, Wakenya wanafanya huko wanakimbilia huku, kuanzia sasa wasifanye, tutawarudisha kwa nguvu na watashughulikiwa kikamilifu na nashukuru wanaofanya mabaya na kukimbilia huko unawashughulikia kikamilifu."

Katika mazungumzo hayo ya simu Rais Magufuli alimwambia Rais Kenyatta kuwa anavipongeza vyombo na ulinzi vya Kenya na kuahidi kuandaa zawadi kwa ajili yao na kumwomba kutoa mbinu zao kwa askari wa Tanzania.

Rais Magufuli pia alimpatia simu Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kuongea na Rais Kenyatta. Katika mazungumzo hayo Samia alimshukuru Rais huyo kwa moyo wa upendo kwa Watanzania.




# Dhahabu zilizot mamilioni yatu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana ameshuhudia makabidhiano ya kilo 35.267 za dhahabu, zilizokamatwa Februari 15, mwaka jana, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Jomo Kenyatta, Nairobi nchini Kenya.

Sambamba na madini yaliyokamatwa yakiwa yanatoroshwa kutoka Tanzania kwenda Dubai, pia Sh. milioni 170 za Kitanzania, Sh. 171,000 za Kenya na Dola za Marekani 77,500 zilikabidhiwa katika hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Dhahabu ambayo ni vipande 22 vyenye kilo 35 na fedha hizo, ziliLetwa nchini na Mjumbe Maalum wa Rais Uhuru Kenyatta wa Jamhuri.

Mjumbe huyo maalum, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya, Balozi Monica Juma, alikabidhi dhahabu na fedha hizo kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi.

Hafla ya kukabidhi dhahabu na fedha hizo ilihudhuriwa na Makamu wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, viongozi wa taasisi mbalimbali zinazohusika na masuala ya sheria, fedha na madini na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Pamoja na kushuhudia makabidhiano hayo, Rais Magufuli alishuhudia uhakiki wa dhahabu hiyo. Wataalamu wa madini wa Tanzania na Kenya walipima ubora na kubaini kuwa vipande 21 kati ya 22 vilikuwa na dhahabu kiasi cha kati ya asilimia 80.2 na 94.1 (purity), kipande kimoja kilikuwa na dhahabu asilimia 59.9 huku vipande vyote vikiwa na uzito wa kilo 35.267.

Akizungumza baada ya kushuhudia makabidhiano hayo, Rais Magufuli amemshukuru Rais Kenyatta kwa kuleta dhahabu na fedha hizo baada ya kukamatwa na vyombo vya ulinzi na usalama na mamlaka za Kenya. Alisema kitendo hicho kinadhihirisha uhusiano mzuri wa kidugu, kirafiki na kijirani uliopo kati ya Tanzania na Kenya.

"Dhahabu hii imekamatwa katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Jomo Kenyatta tangu tarehe 15 Februari, 2018 na fedha hizi zilikamatwa tangu mwaka 2004, zimetunzwa kwa miaka 15 sasa. Hii inaonyesha jinsi Uhuru Kenyatta alivyokuwa mwaminifu na mwenye upendo wa dhati kwa Watanzania. Lakini zaidi kitendo hiki kinaonyesha jinsi uhusiano wetu ulivyo mzuri. Napenda kuwahakikisha hakuna mtu atakayeharibu uhusiano huu wa Tanzania na Kenya," alisema Rais Magufuli.

Rais alibainisha kuwa kwa kutam-

# Ataja sababu kumreje

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli ameeleza sababu za kumrejesha kazini Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mataragio, aliyesimamishwa kazi mwaka 2016.

Akizungumza Ikulu jijini Dar es Salaam jana wakati wa kupokea vipande 22 vya dhahabu vyenye uzito wa kilo 35.34 na fedha zilizodaiwa kuibwa nchini mwaka 2004 katika Benki ya NBC Moshi mkoani Kilimanjaro, Rais Magufuli alifichua mchezo mchafu uliofanywa dhidi ya kigogo huyo.

Alisema mkurugenzi huyo alisimamishwa kazi baada ya kupinga kuuzwa kwa vitalu vyote vya gesi na Tanzania kubaki bila kitalu hata kimoja inachomiliki.

"Huyu mkurugenzi alisimamishwa kazi baada ya kukataa rushwa ya

## HABARI KITAIFA



Rais John Magufuli akishuhudia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akipokea kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Kenya, Balozi Monica Juma, dhahabu pamoja na pesa iliyokamatwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi zikitoroshwa kutoka Tanzania, katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# toroshwa, a Ikulu

bua tatizo la utoroshaji wa madini na manufaa madogo ambayo Tanzania inapata kutoka kwenye rasilimali zake, serikali iliamua kuchukua hatua madhubuti.

Alizitaja hatua hizo kuwa ni kutunga sheria, kusimamia kwa ukaribu na kuanzisha masoko ya madini kote nchini na matokeo yake mapato ya madini yameongezeka kutoka Sh. bilioni 191 mwaka 2017/18 hadi Sh. bilioni 335 mwaka 2018/19 na mwaka huu 2019/20 yanatarajiwa kufika Sh. bilioni 470.35.

Kuhusu udhibiti, alisema matukio 102 yaliyoripotiwa yamefanikisha kukamatwa kwa kilo 163,575 za madini mbalimbali na kalati 6,826.38 za madini ya vito, yote yakiwa na thamani ya Sh. Bilioni 45.

Rais alivipongeza vyombo vya ulinzi na usalama vya Kenya kwa kufanikisha kukamatwa kwa dhahabu na fedha hizo na kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama vya Tanzania kujitafakari vinavyotekeleza wajibu wake wa kulinda rasilimali za umma yakiwamo madini.

"Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Tanzania mjiulize ilikuwaje madini yametoka Uwanja wa Ndege wa Mwanza hamkuyashika, yakatua na kuondoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) hamkuyashika, kisha yakaenda kushikwa Uwanja wa Ndege wa Jomo Kenyatta, Nairobi, Kenya.

"Navipongeza vyombo hivi vya Kenya, nitaandika barua ya pongezi kwa waliokamata dhahabu na pia nitawatafutia zawadi," alisema.

Aidha, Rais alisema Tanzania na Kenya zitaendelea kushirikiana kukabiliana na uhalifu na kwamba mhalifu yeyote atakayefanya uhalifu Kenya na kukimbilia Tanzania atashughulikiwa, na mhalifu atakayefanya uhalifu Tanzania na kukimbilia Kenya atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

# esha bosi TPDC

kampuni fulani iliyokuwa inataka vitalu baharini. Alipigania tubaki na vitalu viwili, tuwekeze fedha kidogo kidogo na kuchimba wenyewe kuliko kuwapa vyote wawekezaji," alibainisha Rais Magufuli.

Jumatatu wiki hii, Ikulu ilitoa taarifa kwa umma ikieleza kuwa Rais Magufuli ameagiza kurejeshwa kazini kwa mkurugenzi huyo mara moja.

Mkurugenzi huyo alisimamishwa kazi na Bodi ya Wakurugenzi wa TPDC Agosti 20, mwaka 2016 na Rais amebatilisha uamuzi huo na kumwagiza Waziri wa Nishati kumrejesha kazini haraka.

# Siri ziara ya Kenyatta Chato

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli ameeleza makubaliano yake na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, aliyemtembelea kijijini kwake Chato mkoani Geita, hivi karibuni.

Akizungumza Ikulu jijini Dar es Salaam jana baada ya kushuhudia makabidhiano ya dhahabu na fedha zilizoibwa nchini na kukamatwa Kenya, Rais Magufuli alisema lengo la ziara hiyo ya Kenyatta Chato lilikuwa kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo kwa Tanzania kuiuzia nchi hiyo mahindi na gesi asilia kwa ajili ya viwanda vyake.

"Siku tulipokutana Chato tulizungumza mambo mawili na alisema atawatuma viongozi wa Wizara ya Kilimo ambao watakuja kwa suala maalum pamoja na wa gesi," alisema.

Rais Magufuli aliongeza kuwa Kenya inataka kununua unga wa mahindi, hivyo ni kutoa fursa ya ajira kwa Watanzania kupitia viwanda.

Alisema tayari amezungumza na Mkuu wa Majeshi nchini ambao wana viwanda vya mahindi na kutaka yafanyike mazungumzo zaidi ya namna ya kusafirisha unga.

"Jeshi linunue kwa wakulima wapate fedha na wapate bei nzuri na wawauzie Kenya, lakini hamlazimishwi kufanyabiashara na jeshi, hata wafanyabiashara wengine ambao mtataka kuingia nao mkataba kwa mawasiliano na wizara husika," alisema.

"Rais Kenyatta pia aliniambia anataka kuanza kununua gesi ya Tanzania, wanataka wakaitumie Kenya, amemtuma Katibu Mkuu wake anayehusika na gesi.

"Wizara ya Nishati mkae mwangalie ni namna gani gesi yetu inaweza kutumika kuingiza fedha, nchi ya Msumbuji imetutanguliwa sana wakati tulianza nao pamoja," alisema. Alisema Rais Kenyatta alizungumza kwa hisia kuwa kupitia Kituo cha Uwekezaji kampuni 404 kutoka Kenya zimesajiliwa nchini wakati kuna 24 tu za Watanzania nchini humo.

Waziri wa Kilimo wa Kenya, Mwangi Kiunjuri, alisema Kenya ina changamoto ya chakula kutokana na mvua kuchelewa na sehemu nyingine ilikatika mapema.

"Kwa takwimu tutapata asilimia 60 ya mavuno, tutakuwa na upungufu, udugu ni kufaana, tumekuja ili mtufae kwa mwezi tunatumia magunia milioni 4.3 kwa matumizi mbalimbali," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa wizara inayohusika na masuala ya gesi nchini humo, Joseph Nyorige, alisema nchi hiyo ilijenga kituo cha kupokea gesi ambayo walitaka kuinunua Qatar, lakini Rais alitaka inunuliwe kutoka Tanzania.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema Bodi ya Mazao Mchanganyiko inayomiliki vinu vya kusaga na kukoboa mahindi mikoa ya Mwanza, Dodoma na Iringa, ina mahindi ya kutosha na inatafuta masoko kwa zaidi ya mwaka mmoja na nusu.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema wanashirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na kwa sasa dhahabu iliyokuwa inapatikana kwa mwaka inapatikana kwa siku kutokana na uwapo wa masoko ya madini.

# Magufuli avimwagia sifa vyombo usalama Kenya

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amevipongeza vyombo vya ulinzi na usalama nchini Kenya, huku akivitaka vyombo vya nchini kuongeza umakini kwa kuwa tukio la kutoroshwa dhahabu na kukamatiwa nchini humo ni aibu kwao.

Kutokana na hali hiyo, ameahidi kutoa zawadi kwa askari na usalama wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini humo vilivyohusika kukamata dhahabu yenye uzito wa kilogramu 35.34 iliyosafirishwa kutoka Uwanja wa Ndege Mwanza hadi KIA na baadaye hadi Uwanja wa Ndege wa Jomo Kenyatta, Kenya na kukamatwa.

Akizungumza jana baada ya kupokea vipande 22 vya dhahabu hiyo na fedha zilizoibwa nchini mwaka 2004 katika Benki ya NBC tawi la Moshi, mkoani Kilimanjaro, alisema vyombo vya dola nchini vinapaswa kujifunza na kuungana katika kulinda raslimali za nchi zisivuke mpaka.

Alisema madini hayo yalikamatwa Februari 15, mwaka jana, yakiwa yametoroshwa kutoka Tanzania hadi Kenya, bila vyombo vya ulinzi na usalama nchini humo kufahamu.

"Navipongeza sana vyombo vya ulinzi na usalama nchini Kenya, nitoe wito kwa vyombo vyetu na nadhani watakuwa wamejifunza, dhahabu imetoroshwa kutoka Mwanza ikaenda hadi KIA na baadaye Kenya ikakamatwa," alisema na kuongeza:

"Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama mkoa huo lazima niwatandike hapa hapa mbele za watu, mali imetoka Tanzania ila ikakamatiwa Kenya na vyombo vya ulinzi na usalama Kenya, je, ilipokuwa ikibebwa kutoka Mwanza au KIA vilishirikiana na mhalifu au walimwachia?" Alihoji.

INAENDELEA UK. 8



Rais John Magufuli akimsikiliza Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wakati akisalimiana kwa simu ya mkononi na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, baada ya viongozi hao, kushuhudia makadhiano ya dhahabu na pesa iliyokamatwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi zikitoroshwa kutoka Tanzania, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# DC akana kumwomba rushwa mwekezaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ametoa ufafanuzi kuhusu kipande cha video kinachosambaa kwenye mitandao ya kijamii, akituhumiwa kuomba rushwa kwa mfanyabiashara na mmiliki wa Hoteli ya Kitalii ya Weruweru River wilayani huko.

Akizungumzia video hiyo katika mkutano wake na waandishi wa habari jana, Ole Sabaya alisema kiini cha kusambazwa kwake ni uamuzi wake wa kumwondoa mfanyabiashara huyo kwenye eneo la ardhi analodaiwa kumpoka mjane, Mary Diriwa (86).

Kipande cha video hiyo kilianza kusambaa juzi kikimwonyesha mfanyabiashara Curthebert Swai, akidai kuombwa rushwa na kiongozi huyo wa wilaya.

Akijibu tuhuma hizo jana akiwa kwenye ardhi ya mjane anayedaiwa kupokwa eneo la ekari moja na robo na mwekezaji huyo, Ole Sabaya alisema: "Na ninyi waandishi wa habari mnanipigia simu kuniuliza juu ya hiyo 'clip' (kipande cha video), mkitaka maelezo yake chanzo chake ndiyo hiki.

"Kwenye taarifa yake, mliyoiona hiyo clip inayozunguka huko, inazungumzia mtu aliyemwomba pesa ya rushwa mara nne, mara ya kwanza, mara ya pili, mara ya tatu na mara ya nne na akisema kwenye hiyo clip kwamba huyu mtu najua siyo, Rais amemtuma.

"Lakini kuna vyombo vya dola hapa, kuna Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) Wilaya, kuna Takukuru Mkoa na unajua huyo mtu anafanya kwa matakwa yake na toka mwezi wa 11, 2018, leo ndiyo unakuja kuchukua hatua uliyoombwa rushwa, baada ya kuchukua mali za hawa kina bibi.

"Kuna 'clip' mnaipeleka huko duniani, anasema kwa mazingira hayo ametishiwa usalama, usalama umetishiwa kwa sababu na yeye ametishia usalama wa wanyonge, kwa hiyo OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya-Lwelwe Mpina), nakuelekeza kwa sababu na yeye ametoa tuhuma zake hizo akijua kabisa leo (jana) nilikuwa nakuja kufanya uamuzi hapa na ana taarifa hiyo na hata taarifa ya mkutano huu anayo kwamba nitakuja leo tarehe hii."

Akiwa katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kijiji cha Kimashuku, Kata ya Mnadani, Wilayani Hai, Mkuu huyo wa Wilaya amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Hai, Lwelwe Mpina, kumhakikishia usalama mfanyabiashara huyo ili haki yake naye itendeke wakati vyombo vya dola vikifuatilia ukweli wa madai yake.

"Kwa hiyo kwanza OCD, fanya hivi mhakikishie Curthebert Swai usalama wake mwenyewe na kwa kuwa wewe ndiyo chombo cha kuhakikisha usalama wake na wewe ili wawe salama," alisema.

"Bibi (mjane aliyedai kunyang'anywa eneo lake), kuanzia tarehe ya leo, tutakuandikia barua, eneo hili ni la kwako na mtu yeyote haruhusiwi kuingilia.

"Zile fedha Sh. milioni 16.3 mlizopatiwa na upinzani kwa ajili ya kusaidia kuandikisha wapigakura wao mngezitumia kuwasaidia watu wanyonge badala ya kuzitumia kuzitumia kunyanyasa wanyonge kama bibi huyu mjane."

# Wastaafu wenye pingamizi walipwa mafao ya bil. 123/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WASTAAFU 108 kati ya 227 waliokuwa na mapingamizi ya mwajiri kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo vyeti feki, wamelipwa mafao yao.

Wastaafu hao ni miongoni mwa wale 2,650 ambao wamelipwa kiinua mgongo chenye thamani ya Sh. bilioni 122.9 kwa kipindi cha Juni Mosi hadi Julai 24, mwaka huu.

Meneja Kiongozi Uhusiano wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Eunice Chiume, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, jijini hapa.

Alisema wastaafu hao 227 ni kati ya 10,000 waliokuwa wa mifuko mbalimbali iliyounganishwa kwenye mfuko huo, lakini hawakulipwa mafao yao kutokana na mapingamizi mbalimbali ya mwajiri.

"Kulikuwa na wastaafu 227 ambao walikuwa hawajalipwa, idadi hiyo imepungua hadi kufikia 119, wastaafu 108 wamelipwa mafao yao," alisema.

Alitaja sababu zilizofanya kutolipwa kwa wastaafu hao kuwa ni kukosekana kwa viambatanisho mbalimbali, pingamizi la waajiri juu ya vyeti feki, kupokea mshahara baada ya kustaafu na kutofautiana kwa sababu za kustaafu kati ya nyaraka halisi na mfumo wa utumishi.

Hata hivyo, alisema juhudi zinafanyika ili kasoro zote zifanyiwe kazi na wanachama hao wapate mafao kwa mujibu wa sheria.

"Tunatarajia Septemba, mwaka huu, tuwe tumemaliza kuwalipa kulingana na watakavyoweza kumaliza mapingamizi yao," alisisitiza.

Kuhusu ulipaji wa kiinua mgongo na pensheni kwa Juni hadi Julai, mwaka huu, Chiume alisema wastaafu 2,650 wamelipwa kiinua mgongo cha Sh. bilioni 122.9 huku Sh. bilioni 92.7 wamelipwa pensheni ya mwezi kwa wastaafu.

**MAFAO YA UZAZI**

Meneja huyo alisema kanuni za malipo ya mafao ya uzazi zinatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu ili kuwalipa wanachama ambao waliwasilisha maombi ya kulipwa mafao hayo baada ya kuundwa kwa PSSSF.

"Baada ya mifuko ya PPF, LAPF, GEPF, na PSPF kuunganishwa na kuundwa kwa PSSSF Agosti Mosi, 2018, serikali inafanya tathmini juu ya mafao ya uzazi na tathmini ikikamilika taarifa itatolewa kwa umma," alisema.

Alisema mfuko huo unaendelea kupokea maombi ya kulipwa mafao ya uzazi kutoka kwa wanachama wa iliyokuwa mifuko hiyo.

"Utaratibu wa malipo ya mafao ya uzazi kwa waliojifungua kabla ya kuanzishwa kwa PSSSF wanalipwa kwa taratibu za mifuko ya awali kwa wale ambao fomu zao zilishawasilishwa kwenye mifuko hiyo," alisema.

Chiume alisema kwa kanuni za mafao hayo kwa PSSSF ziko kwenye mchakato mbalimbali na ziko wizarani na wanatarajia zitaanza kutumika Septemba, mwaka huu.



Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Eunice Chiume (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu malipo ya Sh. bilioni 92.7 yaliyolipwa kama kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi kwa wastaafu kuanzia Juni 1, hadi Julai 24 mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbaroni kwa kudaiwa kumpiga trafiki ngumi, makofi

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

DIWANI wa Kata ya Mwanga Kaskazini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Clayton Revocatus (34) maarufu Baba Revo, amefikishwa katika Mahakama ya Mwanzo Mwandiga kwa kosa la kumpiga askari polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ngumi na makofi.

Mshtakiwa alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Florence Ikorongo na aliposomewa shtaka lake alikana kosa hilo na yuko nje kwa dhamana.

Alitakiwa mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. 500,000. Pia mdhamini awe tayari kusaini fungu la dhamana la ahadi ya Sh. 100,000. Mshtakiwa huyo alidhaminiwa na Diwani wa Kata ya Kigoma Mjini kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Hussein Kalyango.

Hakimu Ikorongo alisema upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na mlalamikaji anatakiwa kufika na mashahidi wake wote mahakamani kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Alisema mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza Julai 22, mwaka huu, lakini alikosa wadhamini na kupelekwa mahabusu katika Gereza la Bangwe. Kesi hiyo ilikuwa imepangwa kusikilizwa jana, lakini mshtakiwa aliiomba mahakama kuwa hayupo tayari kusikilizwa kwa madai kuwa mwili wake kiafya hauko sawa pia ni mara yake ya kwanza kukaa mahabusi kuanzia Jumatatu na Jumanne hivyo kuomba ipange siku nyingine kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Hakimu Ikorongo alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Julai 26, mwaka huu.

Akisoma hati ya mashtaka jana, Hakimu Ikorongo, alisema Julai 15, mwaka huu majira ya saa moja usiku maeneo ya Mwanga kwa Bela katika Mataa ya Barabara ya Lumumba, mshtakiwa huyo bila halali na kwa makusudi alimshambulia askari polisi mwenye namba F 8350 PC Msafiri wa Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kumpiga ngumi na makofi kinyume cha sheria.



Mtaalamu wa nyuki, Elizabeth Nkomola (kushoto), akitoa maelezo kuhusu ufugaji wa nyuki kwa kutumia mizinga ya kibiashara na njia ya kisasa kutoka Shirika la Vijana (TAYOA), wakati wa ugeni kutoka Global Fund, ulipolitembelea shirika hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mama wa kambo adaiwa kumjeruhi mtoto

**Na Elisante John,** SINGIDA

MTOTO mwenye umri wa miaka sita, Emmanuel Fortunatus kutoka Kijiji cha Damankia, wilayani Ikungi, amelazwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Singida, baada ya kudaiwa kupigwa na mama yake wa kambo na kumsababishia jeraha kwenye mguu wake wa kushoto na kulazimika afanyiwe upasuaji.

Mtoto huyo anayesoma shule ya awali katika shule ya msingi iliyopo kwenye kijiji hicho, amelazwa kwenye hospitali hiyo kwa muda wa mwezi mmoja sasa.

Akizungumza na Nipashe, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Ng'hungu Kuzenza, alisema kuwa mtoto huyo alipelekwa kwa mara ya kwanza hospitalini hapo Juni 10, mwaka huu na kulazimika afanyiwe upasuaji ili kutibu kidonda chake.

Dk. Kuzenza alisema baada ya mtoto huyo kufikishwa hospitalini hapo, kidonda chake kilitakiwa kufanyiwa upasuaji kwa kukata sehemu ya nyama kutoka kwenye paja la mguu ambao ni mzima, ili kupandikiza sehemu yenye kidonda, kwa ajili ya kutibu jeraha.

Alisema baada ya upasuaji huo hali ya mtoto inaendelea vema.

Akisimulia mkasa huo, bibi wa mtoto huyo, Justina William, alidai kuwa licha ya mwanamke aliyemtaja kwa jina la Asha David, kumfanyia ukatili huo mjukuu wake, hata yeye amenusurika mara kadhaa kupigwa, kila anapohoji tabia yake isiyofaa mbele ya jamii.

Justina alidai hafahamu sababu ya mjukuu wake kujeruhiwa.

Baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Singida walioongea na gazeti hili akiwamo Zulfa Hamisi, Janeth Herman, na Musa Athumani, wasikitishwa na ukatili huo na kuziomba mamlaka husika kumchukulia hatua kali za kisheria, mwanamke huyo.

Vitendo vya ukatili bado vinaendelea kuikandamiza jamii hapa nchini, Afrika na Dunia kwa ujumla, kutokana na vipigo wanavyofanyiwa watoto, wanawake na hata baadhi ya wanaume.

Kwa mujibu wa dawati la jinsia polisi mkoa wa Singida, tayari jeshi hilo linamemtia mbaroni mwanamke huyo, na atapandishwa kizimbani wakati wowote kujibu mashtaka yake mawili, likiwamo la ukatili, na shtaka la pili likiwa la kosa la jinai, baada ya kujeruhi mtoto huyo.

# Kanyasu aagiza ukiritimba kwa watalii uondolewe

**Na Mwandishi Wetu,** SERENGETI

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameliagiza Shirika la Hifadhi za Taifa nchini (Tanapa) kuondoa mara moja utaratibu wa watalii walioingia hifadhini kutoruhusiwa kutoka nje na kurudi hata kama muda wa kibali haujaisha, maarufu kama 'single entry' ambao umeonekana kuathiri shughuli za utalii hasa ukanda wa magharibi.

Akizungumza wakati wa kufungua maonyesho ya utalii wa kitamaduni mjini Mugumu, wilayani Serengeti, Kanyasu alisema tayari wizara ilishatoa maelekezo kwa Tanapa kutafuta utaratibu mpya ambao hautaathiri shughuli za utalii katika maeneo husika.

Utaratibu huo unafanya mtalii akiingia ndani ya hifadhi haruhusiwi kutoka nje na kurudi tena hata kama muda wa kibali chake bado haujaisha na kama akitoka nje hutakiwa kulipia upya tofauti na ilivyokuwa

INAENDELEA UK. 8

# Sababu wahandisi 67 kusimamishwa

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

SERIKALI imewasimamisha wahandisi 67 baada ya kupoteza sifa na kutemwa kwenye muundo mpya wa Wizara ya Maji kwa kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) itakayokuwa mwarobaini wa kero ya maji nchini.

Vile vile, Wizara ya Maji imewasilisha orodha ya kampuni ya makandarasi zaidi ya 30 kwenye Bodi ya Usajili wa Kampuni ili yaweze kufutwa kutokana na kudaiwa kutumika kuchota mamilioni ya fedha za serikali za miradi ya maji bila kufanya kazi.

Naibu Waziri wa Maji, Juma Aweso, alisema hayo katika Kijiji cha Chankorongo, Kata ya Bukondo na kutembelea mradi mkubwa wa maji uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.5 ulioanza kutoa huduma hiyo. Waziri Aweso alitembelea mradi wa visima vya maji vyenye kina kirefu ya Manga, Kasamwa na Bulela, ambayo kila kimoja kimegharimu zaidi ya Sh. mlioni 22.

Waziri Aweso alianza ziara yake juzi kwa kukutana na uongozi wa Wilaya ya Geita na Mkoa wa Geita na kueleza kuwa serikali ya awamu ya tano imedhamiria kumaliza kero ya maji kwa kumtua mama ndoo kichwani.

Akielezea lengo la serikali kuunda Wakala wa Maji Vijijini, Waziri Aweso alisema inalenga kukomesha hujuma zilizokuwa zikifanywa na baadhi ya watendaji wa wizara hiyo wakiwamo wahandisi kwa kulipa mamilioni ya fedha kwa makandarasi feki, wasio na uwezo na wengine hata ambao hawakufanya kazi wakitumika kuchota mamilioni ya fedha za serikali.

Akizungumzia hali ya upatikanaji maji katika mji wa Geita juzi, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Josephat Maganga, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, alimwambia Waziri Aweso kuwa wakazi wa wilaya hiyo asilimia 51 ndio wanaopata huduma ya majisafi na salama.

Mbunge wa Jimbo la Geita, Costatine John Kanyasu ambaye pa ni Naibu Waziri wa Madini alimweleza Naibu Waziri Aweso kuwa hali ya upatikanaji wa maji katika mji wa Geita kwa sasa ni asilimia 51 na lengo ni kumaliza kero ikiwamo kutoa kipaumbele kwa taasisi za serikali zinazotoa huduma za kijamii.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Pongezi nyingi Ikulu Dar es Salaam, Nairobi*

**SABABU** kubwa inayotajwa kuwa ni chanzo cha maendeleo kwa nchi za Ulaya hasa za Sweden, Norway, Finland na Denmark ni uaminifu na uadilifu mkubwa miongoni mwa viongozi wa serikali na wananchi.

Mataifa yanayotajwa kuwa na kiwango kikubwa cha maendeleo hayo ya ni nchi za Nordic, sababu kubwa ya kuendelea kwa kiwango kikubwa ni uaminifu uliotukuka miongoni mwa viongozi wa raia wa mataifa hayo.

Tunachojifunza ni kwamba uaminifu kwenye kusimamia mali za umma, rasilimali za taifa, sera, sheria na kanuni zote zinazohusika na kuleta maendeleo ya nchi ndiyo nguzo ya maendeleo.

Kwa tukio la jana kuonyesha uadilifu, uaminifu na uzalendo, tunazipongeza serikali za Kenya na Tanzania kwa kufikia viwango vikubwa vya uaminifu ambavyo vimewezesha kurejeshwa nchini kilo zaidi ya 35 za dhahabu zenye thamani ya mabilioni ya Shilingi zilizokuwa zimesafirishwa kwa hila kutoka Tanzania na kutoroshwa Kenya kupitia KIA.

Aidha, tunazipongeza zaidi mamlaka za ulinzi na usalama za mataifa hayo zilizokamata, kulinda na kusimamia urudishwaji nchini wa fedha za Benki ya NBC zilizoibwa nchini ambazo ni takribani Sh. milioni 500.

Hatua hiyo ni ya kuheshimiwa na kutukuka na tunaweza kusema kuwa ni jambo la kihistoria ambalo limefanywa na Ikulu za Nairobi na Dar es Salaam.

Tunaamini uaminifu na uadilifu kama huu unavutia watu mbalimbali duniani kuanzia wawekezaji, watalii na hata raia wengine wa kawaida ambao kama sisi Watanzania tunajifunza neno kubwa la uaminifu.

Hatua hizo zilizofanywa na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya na Rais John Magufuli, zinawapandisha ngazi na kuwafanya kuwa marais wa kuigwa na kuheshimika kwa uadilifu na uwazi uliotukuka barani Afrika.

Katika wakati huu ambao kila kiongozi hasa barani Afrika anatuhumiwa kwa ufisadi na uhujumu uchumi kuanzia kujilimbikizia mali, ubinafsi na hata kung'ang'ania madaraka kunakotokana na kuhujumu mali za umma, viongozi hao wawili wanaweza kutumiwa kuielezea Afrika kwa sura tofauti na ya kung'ara.

Marais Magufuli na Kenyatta wanaingia kwenye ramani ya uongozi wa uadilifu Afrika ambao umelinda na kutetea mali za umma na kuishi misimamo kuwa mali za umma ni za wananchi hivi ni lazima ziwanufaishe watu wote kwa haki.

Kama Rais Magufuli alivyosema, viongozi hao wawili wangeweza kuficha siri wala Watanzania wasifahamu kuhusu mali hizo. Lakini wameamua kuwa waadilifu na kuwapa wananchi kilicho chao na hicho ndicho kilichofanyika.

Watanzania wanapongeza hatua hiyo ya uzalendo na uadilifu na kuwaomba viongozi wengine kuiga mfano huo kwa ajili ya kutunza na kuheshimu mali za umma zinazoleta maendeleo. Viongozi wa serikali walio kwenye sekta za ulinzi na udhibiti wa madini, wawe waadilifu na wazalendo kuenzi kazi kubwa inayofanywa na Marais hawa.

Kadhalika, watumishi wa umma na wa watu waheshimu na kuthamini mali za umma na kuendeleza uadilifu na uaminifu ili kuthibitisha ukweli kuwa kama Rais anavyosena Tanzania si maskini bali na tajiri na kwamba iwapo watu wataacha kuiibia taifa hili ni la mfano kwa maendeleo na utajiri duniani.

Hatua ya Marais hao itumike kulinda na kuheshimu mali za mataifa haya hasa madini na nyara ambazo zinadaiwa kuwa huporwa na wafanyabiashara wasio waadilifu na kutoroshwa nje ya nchi kupitia Kenya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Uko wapi mbadala wa 'waterguard'?

Na Gaudensia Mngumi

**HIVI** karibuni wakazi wa maeneo yasiyo na maji wakiwamo wanaoishi Mpigi Magohe, Msumi na Makabe jijini Dar es Salaam, wanazungumza na Nipashe na kuelezea jinsi uhaba wa maji unavyotikisa maeneo yao na hata kusababisha vifo.

Wananchi hao wanaeleza kuwa wanaotumia maji ya mabondeni au ya kutoka kwenye visima vinavyokusanya maji wakati wa mvua au vya kuchimba kwenye sehemu zenye madimbwi yaliyokauka.

Wananchi hawa wanalalamika kuwa hawana dawa za kusafishia maji na kuiomba serikali iwafahamishe kuwa baada ya kupigwa marufuku 'water guard' iliyokuwa inatumika kutibu maji, mbadala wake uko wapi na ninini?

Wakazi hao walisema kuwa sehemu za Msumi na Makabe na baadhi ya maeneo ya Mpigi Magohe wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam, wananchi hunywa maji yanayotoka kwenye madimbwi.

Wanaeleza kuwa maji hayo hujikusanya wakati wa mvua na pale inapokatika na akiba zilizoko nyumbani kumalizika, watu hukimbilia kwenye madimbwi na visima vya kuchimbwa.

Wanadai kuwa hawana maji ya bomba tangu uhuru mwaka 1961 na hayo ndiyo maisha wanayokutana nayo wakati wakisubiri Shirika la Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasco) na Mamlaka ya Usambazaji Maji na Uondoaji Majitaka (Dawasa) kukamilisha upanuzi wa miundo mbinu na usambazaji huduma utakaowawafikishia maji safi na salama kwenye miji hiyo mipya.

Wanaeleza kuwa kwa muda mrefu wanatumia maji hayo bila kuyatibu, japo kuna baadhi yao hutumia shabu, kuyasafisha ili yawe myeupe lakini hawana dawa ya kuyatibu ili kuua vimelea ili waweze kuosha vyombo, kuogea, kunywa na kupikia.

Wanasema licha ya kwamba maji hayo ni ya chumvi si salama kwa kuwa yanatuama muda mrefu na huchimbwa kutoka chini kwenye madimbwi ya asili.

Wanadai kuwa baadhi walikwenda kwenye ofisi za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuthitishiwa madai kuwa 'waterguard' imepigwa marufuku na kuelezwa kuwa ni kweli imekatazwa kutumiwa.

Hata hivyo, hawakupata mbadala ni nini kitumiwe kutibu maji hayo, licha ya kuwa kuna baadhi yao hutumia shabu kuyasafisha ili kuondoa tope, lakini vimelea vya magonjwa havijatibika.

Hata hivyo, wanaeleza kuwa hawafahamu kipimo cha shabu. Wapo wanaotumia nyingi au pungufu kwa vile hawajapata maelekezo.

Wanasema enzi za 'water guard', walikuwa wanafahamu kuwa inatumika kidonge kimoja kwa ndoo au dumu la lita 20.

Au kifuniko kimoja cha chupa kwa ajili ya ndoo.

Hivyo, walitumia vipimo hivyo kusafisha maji kwenye mapipa na vyombo vikubwa kutegemeana na idadi ya ndoo zilizohifadhiwa, lakini sasa hawafahamu kwa vile shabu hazina maelezo hayo.

Baadhi ya wakazi hao ambao wengi ni wanawake wanaoimba Dawasco na kampuni nyingine zinazouza maji kuwapa maelezo sahihi.

Lakini pia kuwafikishia maji ya kunywa kwenye magari mara kwa mara kuwa, wakati mwingine hununua maji ya kunywa kwa wauzaji binafsi na wajasiriamali ni changamoto. Baadhi wanayachanganya na maji yenye chumvi.

Wanadai wananunua ndoo ya maji ya lita 20 kwa bei kati ya Sh 500 hadi 800 ndiyo maana wanahitaji 'waterguard 'ili kusafisha maji wanayochimba kwenye madimbwi kwa kuwa si wote wanaomudu gharama hizo.

Wanaamini kuwa mashirika hayo yakiweka utaratibu wa kuuza maji yatakuwa na bei nafuu pengine hata Sh 200 kwa ndoo.

Hata hivyo, wanaziomba taasisi za teknolojia na vyuo vikuu kuandaa wataalamu wanaoweza kutatua kero na masuala ya maji mijini na vijijini.

Wanadhani iwapo wataalamu wanaosoma katika vyuo vikubwa, wanapofika maeneo hayo wanaweza kutoa ufumbuzi wa muda wakati wananchi wakisubiri ujenzi wa miundombinu na ukamilishaji kazi ya usambazaji maji maeneo yao.

Wanawake hao wanadai hukesha usiku kucha kusaka maji kwenye visima hivyo vya kuchimba ili kukusanya maji hasa misimu ya kiangazi, kwani maji hukauka. Ni kwa mujibu wa maelezo yao.

Aidha, walidai kuwa baadhi yao wanasikitika zaidi kwa kuwawengine hupoteza watoto wanaotumbukia visima wakati wa kusaka maji hayo.

Walidai kuwa hivi karibuni mtoto mdogo alipoteza maisha maeneo hayo kutokana na kutumbukia kisimani kwa bahati mbaya wakati wa harakati za kusaka maji kwenye madimbwi hayo.

## HABARI KITAIFA

# NEC yatangaza uchaguzi kata 13

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza uchaguzi mdogo wa Kata 13 ambao utafanyika Agosti 17, mwaka huu.

Taarifa kwa umma iliyosomwa na Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji (Rufaa), Mbarouk Salim Mbarouk, Mjini Babati, mkoani Manyara jana, ilieleza kwamba fomu za uteuzi wa wagombea zitatolewa kati ya Julai 29 hadi Agosti 3, mwaka huu.

Jaji Mbarouk alisema uteuzi wa wagombea utafanyika Agosti 3 na kampeni zitafanyika kuanzia Agosti 16.

Alizitaja kata zenye uchaguzi na halmashauri zake kwenye mabano ni Laroi, Lemanyata na Likiding'a (Wilaya ya Arusha), Kimokouwa (Longido), Kwembe (Ubungo), Izigo (Muleba) na Mahida (Rombo). Nyingine ni Makanya (Same), Barikiwa (Liwale), Kikeo (Mvomero), Biro (Malinyi), Myangayanga (Mbinga) na Kapenta (Sumbawanga).

Jaji Mbarouk alisema Tume imetangaza nafasi hizo kuwa wazi baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, ameitaarifu Tume uwapo wa nafasi wazi za madiwani katika kata 13 zilizopo katika halmashauri 11 na mikoa minane ya Tanzania Bara. Alisema nafasi wazi za udiwani katika kata hizo zimetokana na sababu mbalimbali zikiwamo vifo, kujiuzulu na uamuzi wa mahakama. "Baada ya kupokea taarifa hiyo na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa; Tume ina utaarifu umma kuhusu kuwepo kwa uchaguzi mdogo katika kata hizo 13," Jaji Mbarouk alisema. Jaji Mbarouk alisema Tume inavialika vyama vya siasa, wadau wote wa uchaguzi na wananchi kushiriki katika uchaguzi huo.

"Tume inachukua fursa hii kuviasa vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia matakwa ya Katiba, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2015, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015 pamoja na maelekezo yote yaliyotolewa au yatakayotolewa na tume wakati wote wa uchaguzi mdogo," alisema.

# Wavuvi watatu wakutwa Mombasa, mmoja afariki

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

WAVUVI wanne kati ya wanane waliozama baharini eneo la Shumba Mjini katika Wilaya ya Micheweni, wamepatikana Mombasa nchini Kenya wakiwa na hali mbaya, huku mmoja akiwa amekufa.

Kwa mujibu wataarifa za uhakika kutoka kwa ndugu na jamaa za watu hao kutoka Mombasa nchini Kenya, chombo kimoja kati ya viwili vilivyopotea Jumatatu na watu hao na kukutwa Kenya na wavuvi watatu wamepatikana wakiwa hai.

Chanzo hicho kutoka Mombasa kimewataja walionusurika kuwa ni Rashid Othuman Ali, Kombo Ali Hasan na Omar Ali Hasan ambao wamekimbizwa hospitalini kupatiwa matibabu.

Kilisema aliyefariki dunia hajatambuliwa, na kwamba nahodha, Mohamed Makame Mwinyi hajapatikana, ingawa jitihada za kuwatafuta zinaendelea.

Baadhi ya waokoaji walioko baharini kuwatafuta walisema kwamba jana upepe mkali umepungua na wanapata nafasi ya kwenda mbali zaidi kuwatafuta katika maeneo tofauti ya bahari na kwenye fukwe za eneo la mbali na karibu kwa kuwa wamejigawa katika makundi.

Mkuu wa Mkoa Kaskazini, Omar Khamis Othuman, alisema taarifa za uhakika walizo nazo ni kuwa watu hao walionekana Kenya na moja wao alifariki wakiwa katika jitihada za kujiokoa.

Alisema wamesimulia kuwa baada ya chombo chao kuzama walikishiklia huku wakipigwa na mawimbi makubwa, ila mwenzao alifika mahala wakamwona akiwa hoi na kushindwa kuendelea kushikilia ndipo alipopotea na hadi wanaokolewa mwenzao huyo hakuwapo.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ), Shamata Khamis Shaame, ambaye pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni, alisema jitihada za kuwatafuta zinaendelea kwa kasi huku wakiwa wamejenga matumaini bada ya kuwaona wavuvi wanne ambao hawajaonekana.

Alisema kuonekana kwa wenzao kumepunguza machungu, licha ya mmoja kukutwa amekufa.

"Tutaendelea kuwatafuta katika hali yoyote tukavyowakuta wakiwa hai au wamekufa hadi tutakapo waona," alisema.

Hili ni tukio la pili wavuvi kisiwani Pemba kupokea, kwani hivi karibuni wavuvi wapatao 100 kutoka kisiwa cha Fundo walizama baharini katika hatakati za kuvua kisha kukutwa nchini Kenya.



Mmoja kati ya wavuvi wanane waliozama baharini Shumba Mjini, Wilaya ya Micheweni akibebwa na wasamaria wema baada ya kupatikana kwenye ufukwe wa Mombasa nchini Kenya. **PICHA: SULEIMAN OMAR**

# TIC kutumia mkutano wa SADC kutangaza uwekezaji

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesema kitatumia mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini kwa sababu soko la jumuiya hiyo ni kubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia kongamano la kimataifa la zao la korosho lililofanyika Mtwara na kueleza kuwa anaamini linakwenda kusaidia katika kuongeza thamani ya zao hilo nchini. Akizungumza kuhusu mkutano wa SADC, Mwambe alisema TIC inatambua umuhimu na fursa zinazotokana na mkutano huo, hivyo wamejipanga kikamilifu kuhakikisha wanatumia nafasi hiyo kuitangaza Tanzania kwenye uwekezaji.

"Jumuiya ya SADC ina watu milioni 450, hili ni soko kubwa na Tanzania inayo nafasi ya kutosha kuitumia kwa ajili ya kufanya maendeleo yake kupitia uwekezaji. Yapo mambo mengi ambayo nchi wanachama wamekubaliana na yanatoa nafasi kwa nchi hizo kutumia soko hilo kufanya biashara," alisema.

Alisema SADC ni eneo kubwa la soko ambalo kama nchi ina nafasi ya kuitumia vizuri.

Tanzania ina nafasi kubwa endapo itaamua kutumia jumuiya hiyo ni eneo kubwa.

"Tunafahamu tulianza na SADC iliyokuwa na lengo la kukomboa nchi za Kusini mwa Afrika na baadaye tukawa na SADC ambayo imejikita kuzungumzia maendeleo," alisema.

Mwambe alisema Tanzania ni mwanzilishi wa SADC iliyokuwa na CC mbili na baadaye nchi zilizomo kwenye jumuiya hiyo zikaingia kwenye SADC yenye C moja. "Mkutano wa SADC kufanyika hapa Tanzania ni fursa ya pekee, tutautumia kujitangaza kama ambavyo tumekuwa tukifanya siku zote," alisema. "Mkutano huu ambao unatarajia kufanyika mwezi ujao, Rais John Magufuli atakabidhiwa Uenyekiti wa SADC na hivyo ni fursa nzuri itakayoiwezesha nchi kujiimarisha kwenye soko la biashara kwa nchi wanachama," alisema.

Akizungumzia kongamano la kimataifa la zao la korosho Mtwara, Mwambe alisema zaidi ya washiriki 400 walihudhuria wakiwamo wageni 100 kutoka mataifa 23 duniani.

"Baada ya kongamano hili wengi wao wameonyesha nia ya kuja kuwekeza katika zao la korosho, kwa kuwa mikoa inayolima ni Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma iko tayari kupokea wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika kuinua zao la korosho," alisema.

Mwambe alisema maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya uwekezaji yanatakiwa kuandaliwa mapema ikiwa ni pamoja na kupimwa na kuwekwa michoro ili mwekezaji akipatikana iwe rahisi kuanza kazi.

Pia aliwataka Watanzania kuwekeza kwa kuwa wakiamua wanaweza na kikubwa ambacho wanatakiwa kukifanya ni kuunganisha nguvu ya pamoja.

"Watu wengi wanaogopa kuwekeza kwa sababu ya neno uwekezaji wakifikiri kuwa mwekezaji ni mzungu, nitoe rai kwa Watanzania wajitokeze kwa wingi," alisema.

# Magufuli avimwagia sifa vyombo usalama Kenya

INATOKA UK. 3

Aliendelea kuhoji kuwa kwa hali hiyo ni dhahabu kiasi gani imetoroshwa bila watuhumiwa kushtakiwa na kwamba jambo hilo wanaliacha kwa wakuu wa vyombo hivyo.

"Mnafanyakazi nzuri sana, lakini kuna mahali hamfanyi vizuri, hii inadhihirisha ni aibu kwetu kwa vyombo vyetu kwamba tunaachia mali hadi zinakwenda kushikwa kule," alisema Rais Magufuli.

Aidha, alisema ataandika barua ya kuvipongeza vyombo vya ulinzi na usalama nchini humo kwa kuwa vimefanya kazi nzuri sana, na kwamba wasingefanya dhahabu hiyo isingeshikwa na isingeshikwa kusingekuwa na hafla hiyo wala Rais Kenyata asingetuma ujumbe wa viongozi kutoka nchini humo.

"Niviombe vyombo vya ulinzi na usalama kuongeza bidii, vishirikiane siyo kila mmoja afanye kivyake, mshirikiane ili mali za Watanzania zisiendelee kuibiwa, hii ni bahati nzuri alipitia Kenya inawezekana angepita baharini tusingemwona na ndiyo maana Kenya wanahitaji heshima ya pekee," alisisitiza Rais Magufuli.

Aidha, alibainisha na hata katika mazungumzo yake na Rais Uhuru Kenyatta kwa simu alieleza kuwa unaandaliwa utaratibu wa kuwapongeza askari na usalama wote waliohusika kukamata mali hiyo na kwamba watapewa zawadi.

**KAULI YA IGP SIRRO**

Hata hivyo, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, aliomba radhi kwa kumtia iabu Rais baada ya mali hiyo kukamatwa Kenya wakati wanalipwa mishahara kwa ajili ya kulinda mali za Watanzania.

Wanasema kufanya kosa mara moja siyo kosa, lakini kurudia kosa ndiyo kosa zaidi zaidi, nikuhakikishie lililotokea hilo kosa tutajipanga vizuri," alisema na kuongeza:

"Nitoe salamu kwa wahalifu wasifikiri wanaweza kucheza kama walivyokuwa wanacheza, walivyocheza nyuma, niwaambie waache wakiendelea wasiilaumu serikali, madini ni mali yetu, mali yetu yote lazima tuhakikishe tunailinda na ulinzi wa mali yetu lazima tushirikiane, wale wachache sheria itachukua mkondo wake na wataacha familia zao."

"Hii imetokea kwa bahati mbaya na Wakenya wanajua majeshi yetu yako vizuri, tunawaomba Watanzania waendelee kutuamini," alisema.

Baada ya hapo, Rais Magufuli alisema amefurahishwa na kauli kuwa watajirekebisha, na kuwa halitatokea tena na kwamba majeshi yote yanafanya vizuri na ndiyo maana nchi iko salama, lakini katika eneo hilo lilileta dosari.

"Mkatekeleze ili mali zetu zisishikiwe nje ili wale wanaofanya tuwalete huku watusaidie, ila siyo vizuri mali zetu kuendelea kutoroshwa na vyombo vyetu vipo, kwingine mmefanya vizuri sana. Nina imani kubwa nanyi, ila wananchi watoe ushirikiano ili kuhakikisha rasilimali zinazoibiwa zitumike nchi kujenga barabara na hospitali," alisema.

Aidha, alipongeza nchi hiyo kwa kuipenda Tanzania kwa kuwa fedha zilizoibwa nchini mwaka 2004 zimerejeshwa nchini kwa ajili ya kutumika kama ushahidi wa kesi ya uporaji wa kutumia silaha mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Tanzania na Kenya tutaendelea kushirikiana kwa masuala haya kwa nguvu zote, ukifanya makosa Kenya ukakimbilia Tanzania utashughulikiwa kikamilifu, ukifanya makosa Tanzania ukakimbia Kenya utashughulikiwa kikamilifu, mkosaji wa Kenya ni mkosaji wa Tanzania na mkosaji wa Tanzania ni mkosaji wa Kenya," alisema.

Aidha, alisema ushirikiano wa Ofisi za Wakurugenzi wa mashtaka nchini ziendelee kushirikiana kama matakwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yanavyotaka.

Awali, Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), Biswalo Mganga, alisema mtuhumiwa kwa kesi ya utoroshaji wa dhahabu hiyo ni Baraka Chaulo aliyetokea Mwanza akielekea Dubai kupitia Kenya, na kwamba kwa sasa anakabiliwa na kesi namba 8 ya mwaka 2018.

Alisema mazungumzo kati ya ma-DPP wa pande zote yamewezesha dhahabu hiyo na fedha hizo kurejeshwa kwa mujibu wa sheria, na kwamba wamekubaliana kushirikiana katika maeneo yote.

"Katika ushirikiano huu tunashuhudia kurejeshwa kwa fedha zilizokamatwa Kenya baada ya kuibiwa Tanzania mwaka 2004 katika tukio la uporaji kwa kutumia silaha la Mei 21, mwaka 2004 ndani ya benki ya NBC tawi la Moshi.



Tukio hilo ambalo lilitokea wakati benki hiyo ikifungwa ambapo wateja waliongezeka kwa ghafla, waliwafungia ndani ya chumba cha kuhifadhia fedha wateja na wafanyakazi kisha kupora zaidi ya Sh. bilioni 5.2 kikiwa ni kiasi kikubwa cha fedha kuwahi kuporwa kwenye taasisi za benki nchini wakati ule.

Kutokana na tukio hilo watuhumiwa mbalimbali walikamatwa wakiwamo Watanzania wanane ambao walikuhumiwa miaka 30 jela na wengine kuachiwa, huku raia wawili wa Kenya na Uganda wakiendelea kutafutwa.

Aidha, katika ushahidi wa kesi mbili ambazo zimemalizika kwa nyakati tofauti, Patrick Ayisi Ingoi alitajwa kama kiongozi wa uvamizi huo, na jitihada za kumleta nchini kwa miaka 15 zilishindikana licha ya Tanzania kufungua kesi mbalimbali katika Mahakama Kuu ya Kenya na kushindwa.

Januari mwaka huu, Ingoi alifikishwa mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi, akidaiwa kuhusika na tukio hilo lakini alikana mashtika na kesi yake inaendelea kusikilizwa.

Katika mashtaka yanayomkabili raia huyo, anadaiwa kuiba Dola za Australia 610, Dola za Canada 1,422, Faranga za Uswis 5,300, Euro 16,690, Paundi 1,235.

Nyingine ni Krona za Norway 2,200,Krona za Sweden 2,140, Dola za Kimarekani 4,532 na hundi za kusafiria za thamani ya Dola za Kimarekani 11,050.

Mshtakiwa huyo anadaiwa pia kuiba Sh. milioni 126.2 ambazo zilikuwa mali ya Benki ya NBC isipokuwa Sh. bilioni 5.3 zilizokuwa mali ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

**TANZANIA ILIVYOFANIKIWA**

Licha ya vikwazo mbalimbali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Kenya alifungua mashtaka kwa niaba ya Tanzania ili mshtakiwa huyo na mwenzake, Wilfred Onyango, waletwe nchini, lakini waligonga mwamba hadi walivyofanikiwa mwaka jana.

Onyango alikamatwa na watuhumiwa wengine 11 wakiwa Msumbuji, na aliletwa nchini akashtakiwa na kuhukumiwa miaka 30 jela.

Aidha, kwa Uganda watuhumiwa Charles Lumago na Shaban Wayabona, walitoroka nchini na raia wengine wa Kenya, na mahakama jijini Kampala ilitupilia mbali ombi la Tanzania dhidi ya watuhumiwa hao.

## Kanyasu aagiza ukiritimba uondolewe

INATOKA UK. 5

zamani.

Ulianzishwa baada ya kubainika kuwa baadhi ya kampuni za kitalii zilikuwa zinatumia mwanya huo kuibia Tanapa kwa kuingiza wageni tofauti na waliolipiwa awali hivyo kuikosesha mapato.

"Single entry inadumaza utalii upande wa magharibi hivyo lazima iondolewe mara moja huku Serengeti. Mageti ya Ndabaka na Ikoma (ya kuingilia watalii katika hifadhi ya Serengeti) yamedumaa kabisa. Naliagiza hili very strongly (kwa nguvu) na litekelezwe immediately (mapema), " alisisitiza.

Naibu Waziri Kanyasu alisema Tanapa inapaswa kutafuta njia mbadala ya kudhibiti tatizo la baadhi ya kampuni za kitalii kuihujumu ikiwa ni pamoja na kutumia mfumo wa alama za vidole (biometric) badala ya kuendelea na mfumo wa sasa wa single entry.

Kuhusu suala la Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kushindwa kukusanya kodi katika hoteli zilizopo ndani ya Hifadhi ya Serengeti, Kanyasu alisema huo ni uzembe wa mkurugenzi wa halmashauri hiyo kwa kuwa suala hilo lipo kisheria na asilimia 80 ya hifadhi hiyo iko ndani ya Wilaya ya Serengeti.

Vile vile, aliagiza kuwa viongozi wote wa maeneo ya hifadhi za kijamii (WMA) waliomaliza muda wao waendelee mpaka pale wizara itakapomaliza kutunga kanuni za kusimamia hifadhi hizo.

Awali Mbunge wa Serengeti, Joseph Rioba na Mkuu wa wilaya hiyo, Nurdin Babu, walisema utaratibu wa single entry umeathiri utalii wilayani humo baada ya watalii kuzuiwa kutoka na kurudi hifadhini hivyo hata wananchi waliokuwa wakiuza bidhaa zao kukosa soko.

Maoenyesho hayo ya siku tatu yameandaliwa kwa lengo la kukuza utalii wa kitamaduni wilayani Serengeti.


**NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kampuni ya **KOTI BROTHERS COMPANY LTD** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara gari, iliyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo mteja husika ameshindwa kulipa mikopo wake kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku saba (7) kwa dhamana ya Gari; Dhamana husika itauzwa kwa njia ya mnada kwa siku husika iliyopangwa.Mnada utafanyika sehemu gari husika ilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na | Jina La Mdaiwa | Jina la mwenye Dhamana | Aina ya Dhamana | Tarehe | Mahali Ilipo Dhamana Na Kampuni Inayouza | Muda wa Mnada |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | AJE HARDWARES AND CONSTRUCTION COMPANY | KYANDO/KENETH,ASIFIWE | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 40466-MBYLR | IJUMAA 09/08/2019 | VETA MANGA, MBEYA MJINI - KOTI BROTHERS 0762058614 | KUANZIA SAA 8.00 ASUBUHI |
| 2. | SANGA/VONEKE,EMELIANA | SANGA/VONEKE,EMELIANA | NYUMBA YA KULALA WAGENI (GUEST HOUSE) | JUMAMOSI 10/08/2019 | KABWE, MBEYA MJINI - KOTI BROTHERS 0762058614 | KUANZIA SAA 5.00 ASUBUHI |
| 3 | MBWILO/N,AYUBU | MBWILO/N,AYUBU | NYUMBA | ALHAMISI 08/08/2019 | IGAWILO, MBEYA - KOTI BROTHERS 0762058614 | KUANZIA SAA 5.00 ASUBUHI |
| 4 | LUPONDO/SAMOJA,RODRICK | LUPONDO/SAMOJA,RODRICK | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 14264-MBYLR | JUMAMOSI 10/08/2019 | NJIAPANDA YA KYELA MJINI - KOTI BROTHERS 0762058614 | KUANZIA SAA 9.00 JIONI |
| 5 | NGOGO/NELSON,NURA | NGOGO/NELSON,NURA | NYUMBA | IJUMAA 09/08/2019 | AIR PORT YA ZAMANI,MBEYA MJINI - KOTI BROTHERS 0762058614 | KUANZIA SAA 5.00 ASUBUHI |
| 6 | LYIMO/P,EMMANUEL | LYIMO/P,EMMANUEL | NYUMBA | ALHAMISI 08/08/2019 | ILOLO,MBEYA MJINI - KOTI BROTHERS 0762058614 | KUANZIA SAA 7.00 MCHANA |
| 7 | MWAKASANGA/F,DENIS | MWAKASANGA/F,DENIS | NYUMBA | JUMAMOSI 10/08/2019 | IPINDA,KYELA- KOTI BROTHERS 0762058614 | KUANZIA SAA 7.00 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**

**Dhamana zitauzwa mahali zilipo**

Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.

*Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.*

Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

*WOTE MNAKARIBISHWA.*

215340302

## HABARI KITAIFA

# Teknolojia yapandisha mapato hadi bil. 600/-

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

MFUMO wa ukusanyaji mapato kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki umeziwezesha halmashauri nchini kuongeza mapato ya ndani kutoka Sh. bilioni 553.39 hadi Sh. bilioni 661.36 mwaka huu.

Kwa mujibu wa Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa Tanzania (Alat), mapato hayo yameongezeka katika kipindi cha mwaka 2017/18 hadi 2018/2019.

Mwenyekiti wa Alat Taifa, Gulamhafeez Mukadam, alisema hayo juzi jijini Mwanza alipokuwa akisoma taarifa katika mkutano mkuu wa 35 wa Alat taifa uliomalizika jana.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu, kupitia mfumo wa ukusanyaji mapato wa kielektroniki halmashauri nchini zimeongeza mapato ya ndani hadi kufikia Sh. bilioni 661.363 ," alisema Mukadam.

Aliwaambia wajumbe kuwa mfumo huo umesaidia halmashauri nyingi nchini kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani akitaja Ilala, Kinondoni, Temeke, Dodoma, Dar-es Salaam, Arusha, Ubungo, Tanga, Mwanza pamoja Mbeya.

Alisema kuwa baadhi ya halmashauri zimeshika mkia katika ukusanyaji wa mapato ambazo ni Kakonko, Buhigwe, Kigoma, Gairo, Bumbuli, Madaba, Songea, Rorya, Kondoa na Momba ambazo serikali inaendelea kusisitiza kuongeza bidii.

Alisema kuwa katika hatua nyingine jumuiya hiyo inatarajia kujenga jengo la makao makuu na kitega uchumi jijini Dodoma lenye ghorofa nne linalokadiriwa kugharimu Sh. bilioni 15 na kwamba ujenzi huo haujaanza kutokana na changamoto ya fedha na kwa sasa inajenga ofisi ndogo jijini Dodoma itakayogharimu Sh. milioni 117, ambao umefikia asilimia 95.

Katika mkutano huo Mweyekiti wa ALAT Mwanza ambaye pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Elisha Hilal, aliwasilisha kilio cha madiwani na wenyeviti wa halmashauri kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiomba serikali kuwaongezea posho zao.

"Mheshimiwa waziri sisi kilio chetu madiwani na wenyeviti wa halmashauri ni kuiomba serikali kutuongezewa posho zetu. Hivi sasa tunazolipwa ni kidogo mno, wakati sisi ndiyo wasimamizi wakubwa wa miradi ya maendeleo ya wananchi, tuna kazi kubwa," alisema Hilal.

Hoja ya kuongezwa posho kwa madiwani na wenyeviti wa halmashauri iliungwa mkono na mwenyekiti wa Alat Taifa, Mukadam na wajumbe wengine kadhaa, lakini Waziri Mkuu Majaliwa alijibu kuwa hata wabunge nao wanamatatizo kama ya kwao na kwamba wawe wavumilivu ili serikali iangalie suala hilo.

Mkutano huo umewashirikisha viongozi mbalimbali kutoka katika halmashauri zote za wilaya na majiji, wadau wa sekta binafsi, viongozi mbalimbali wa serikali, wilaya, mikoa,wakiwamo wakurugenzi.

Aidha, wengine kutoka Afrika Mashariki, mashirika ya umma na yasiyokuwa ya kiserikali, taasisi mbalimbali pamoja wabunge.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, akizindua kiwanda cha Plasco Tanzania kinachotumia teknolojia ya Weholite ambayo ni ya kwanza nchini Tanzania, Afrika Mashariki na Kati, jijini Dar es Salaam, jana. Watatu kushoto ni Mkuu wa Uendeshaji wa kiwanda hicho, Alimiya Osman na kulia ni Balozi Finland Tanzania, Antila Sinnika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake, vijana walamba mabilioni

**Na Mwandishi Maalum**

WANAWAKE, vijana na walemavu katika Halmashauri ya Mji wa Geita wamepokea zaidi ya Sh. bilioni 1.6 ambayo ni mikopo nafuu inayotolewa kwa ajili ya kuondoa umaskini. Wananchi hao walipokea fedha hizo hadi kufikia mwezi huu (Julai mwaka huu) ili kutimiza lengo na azma ya serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Rais John Magufuli la kuondoa umaskini katika jamii.

Mbunge wa Geita Mjini ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema. Alieleza kuwa mikopo hiyo imetolewa ili kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira na kuwezesha kuinua kipato cha wananchi kwa kunufaika na miradi mbalimbali na hatimaye kuweza kujikwamua kiuchumi.

Kanyasu alisema hayo kwenye mkutano kati ya wananchi na mbunge huyo kuhusu utekelezaji ahadi mbalimbali alizozitekeleza ikiwamo ya kuwezesha kupatikana kwa mkopo wa Sh. bilioni 1.6 kwa vikundi mbalimbali kwa lengo la kupunguza umaskini katika jamii. Akiwa kwenye mkutano uliofanyika katika kata ya Ihanamila Wilaya ya Geita, Kanyasu aliwaeleza wananchi hao kuwa kutokana na uhusiano mzuri uliopo miongoni mwa madiwani katika halmashauri hiyo serikali yao imetoa mikopo hiyo kwa ajili ya maendeleo.

Alisema kuwa mikopo hiyo itasaidia katika uanzishwaji wa viwanda vidogo, ambavyo vitatengeneza ajira na kukuza uchumi.

Akizungumza katika mkutano huo, Kanyasu alisema anajisikia fahari kwa halmashauri kutoa mkopo huu ikiwa ni moja ya ahadi zilizotolewa na kutimizwa na kuhakikisha wananchi wake wanajihusisha kwenye shughuli za kiuchumi ili kupunguza umaskini kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Alisema kuwa kutokana na changamoto iliyoko katika taasisi za fedha, ambazo hutoa mikopo kwa riba kubwa na kuhitaji dhamana ya nyumba na ardhi jambo ambalo linawakwamisha wakopaji hivyo, serikali imeamua kutoa mikopo ya masharti nafuu.

Aidha, alisema mikopo hiyo itawasaidia makundi hayo kuongeza mitaji na kutoa ajira ndani ya jamii.

Kadhalika, Kanyasu alisema katika awamu ya pili ya utoaji mkopo amesema kuwa wataongeza viwango vya mikopo kwenye vikundi ambapo kila kikundi kitakuwa na uwezo wa kukopeshwa hadi Sh. milioni 20 tofauti na ilivyokuwa awali.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Ihanamiro, Joseph Lugaira, amemweleza mbunge huyo kuwa katika kata hiyo jumla ya vikundi 19 vimenufaika na mkopo huo kwa kuanzisha shughuli za kiuchumi.

Alisema vikundi hivyo vimekuwa vikifanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo biashara pamoja na kilimo ambapo anaamini wataweza kupata faida pamoja na kurejesha mkopo huo na kukopa tena. Diwani wa Viti Maalum, Suzana Mashala, aliwahimiza wanawake wakope kwani hawawezi kujiendeleza kiuchumi pasipo kukopa.

## Wadau wajitetea kutorosha madini

**Na Moab Dominick,** KAHAMA

SIKU chache baada ya Waziri wa Madini, Doto Biteko, kutoa agizo kwa Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Shinyanga, Joseph Kumbulu, kushirikiana na viongozi wengine kudhibiti mialo inayotorosha dhahabu, baadhi ya wamiliki wa mialo wameibuka na kujitetea.

Waziri Biteko alisema kuwa kunautoroshwaji mkubwa wa dhahabu kupitia mialo mbalimbali iliyopo kata ya Bulyanhulu katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga.

Aidha, aliagiza viongozi wa serikali kuanza msako mkali kwa wilaya nzima ya Kahama wa kubaini vichochoro vya mialo inayotorosha madini.

Deogratius Antony, anayemiliki moja ya mialo katika mgodi wa Kakola, akizungumza jana na wanahabari, alikana na kusema asilimia kubwa ya mialo iliyopo ndani ya mgodi haihusiki na utoroshaji wa dhahabu na kuongeza kuwa watu pekee wanaoweza kuhusika ni wanaochenjua nje ya migodi.

Aidha, aliahidi kushirikiana na serikali ili kuona dhahabu inayotoka katika mialo yao haitoroshwi.

"Sisi wamiliki wa mialo tumepokea kwa mikono miwili agizo la Mheshimiwa Waziri wa Madini la kudhibiti utoroshaji lakini wengi tuliopo eneo la mgodi hatuhusiki," alisema Antony.

Mdau wa Madini, Athuman Said, alisema serikali ya awamu ya tano ni mfano wa kuigwa akisema kuwa Rais John Magufuli ni mtetezi wa wanyonge kwani zamani wachimbaji wadogo hawakuthaminika ukilinganisha na ilivyo sasa.

Kaza Roho alisema Rais Magufuli kuwajali wachimbaji haona kuwataka kuungana kwa pamoja ili kufanikisha ulipaji wa kodi ni lazima ili serikali ipate mapato na kuongeza kuwa wachimbaji wanalithamini na hawako tayari kutorosha madini.

# Wajawazito waitwa hospitali kutokomeza vifo vya uzazi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAJAWAZITO hususan wanaoishi maeneo ya vijijini mkoani Shinyanga, wameaswa kujenga utamaduni wa kuhudhuria kliniki mapema na kwa wakati pamoja na kujifungua watoto wao hospitalini, ambako ni salama, ili kupunguza ama kutokomeza kabisa vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi.

Rai hiyo ilitolewa juzi na mwandishi wa habari wa kituo cha matangazo Radio Faraja iliyopo Shinyanga Mjini Josephine Charles, alipotembelea wodi ya kinamama waliojifungua kwa njia ya upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo, kwa ajili ya kutoa zawadi wakati akisherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Alisema ili tatizo la vifo vya mama na mtoto mkoani Shinyanga lipate kupungua, ni lazima wajawazito wapende kuhudhuria kwenye huduma za afya, ili waanze kupatiwa huduma mapema pamoja na kupewa ushauri wa namna ya kuilea mimba, kufanya mazoezi na kula vyakula vyenye vitamini ili siku atakapojifungua ajifungue mtoto salama.

"Nimeamua kusherehekea siku yangu ya kuzaliwa kwenye wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga, wodi ambayo na mimi nilijifungua mtoto wangu, ili kutoa zawadi na hamasa kwa kinamama kupenda kujifungulia watoto hospitali na kupunguza tatizo la vifo vya uzazi mkoani hapa," alisema Charles.

"Nasema haya kwa sababu siku ambayo mimi nalazwa kwenye wodi hii kwa ajili ya kujifungua mtoto wangu, alikuja mama mmoja akiwa hoi, na alipohojiwa na wauguzi ili kuchukuliwa taarifa zake aligundulika hakuwahi hata siku moja kuhudhuria kliniki, na alipozidiwa ndipo akaona aje hospitali, kitendo ambacho ni hatari kwa maisha yake," aliongeza.

Pia alitaja zawadi ambazo alizitoa kwa kina mama ambao wamejifungua watoto kwenye hospitali hiyo ni taulo za kike, sabuni za kufulia, kuogeshea watoto pamoja na poda, na kutoa wito kwa watu wengine wawe wanasherehekea siku zao za kuzaliwa kwa kutoa msaada kwa wenye uhitaji na siyo kufanya anasa.

Baadhi ya wazazi waliojifungua watoto wao kwa njia h ya upasauaji, Dotto Jumanne na Winfrida Joseph, wakazi wa mkoani Shinyanga, walishukuru kupewa zawadi hizo huku wakipongeza huduma ambayo wanapatiwa hospitalini hapo, ambapo wameweza kujifungua watoto wao salama.

Daktari wa wodi ya wajawazito katika hospitali hiyo, Dk. Amon Amon, alitoa wito kwa wadau wa afya mkoani hapa kuendelea kutoa elimu kwa kinamama juu ya umuhimu wa kuhudhuria kliniki mapema na kwa wakati pamoja na kujifungua watoto kwenye huduma za kiafya.

Taarifa ya mratibu wa huduma ya uzazi na mtoto mkoani Shinyanga, Joyce Kandolo, inataja takwimu za vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi mkoani hapa kwamba mwaka 2017 walifariki 73, mwaka 2018, 56 na mwaka 2019 kuanzia Januari hadi Aprili wameshafariki 18.

Pia ilitaja takwimu za vifo vya watoto wachanga mwaka 2017 walifariki 913, ambapo mwaka 2018 walikuwa 815, na mwaka huu kuanzia Januari hadi Aprili wameshafariki 218, na kubainisha kuwa ili vifo hivyo vipungue, ni lazima wajawazito wapende kuhudhuria kliniki na kujifungulia hospitali.



Wananchi wakiangalia ujenzi wa barabara inayochongwa kwa michango yao waliyochangia katika eneo la Mamlaka ya mji mdogo Bagamoyo, Kitongoji cha Udindivu mkoani Pwani jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Madereva wasafirisha mizigo ya kemikali wapewa angalizo

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amewataka madereva wanaosafirisha mizigo ya kemikali nchini kutumia elimu waliyopata kuepusha ajali ili kulinda afya za binadamu na mazingira.

Dk. Mafumiko alitoa wito huo juzi jijini Dar es Salaam, wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya usafirishaji salama wa kemikali kwa madereva 36 kutoka kampuni zinazojihusisha na usafirishaji wa mizigo ya kemikali.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwapa elimu juu ya usafirishaji salama wa kemikali na misingi ya kufahamu kemikali ili wanaposafirisha mizigo hiyo wawe makini ili kulinda afya zao, wananchi na mazingira kwa ujumla. "Napenda kuwapongeza sana kwa kuhudhuria mafunzo haya na kupata elimu kuhusiana na usafirishaji salama wa kemikali. Mnapaswa kufahamu lengo la mafunzo haya ni kuwapatia ufahamu juu ya usafirishaji salama wa mizigo ya kemikali kwa lengo la kulinda afya zenu, wananchi na mazingira mnayopita wakati wa kusafirisha kemikali.

Nimefurahi kusikia kwa kauli zenu kwamba mafunzo haya yamewabadilisha na kuwafanya kuwa madereva bora na makini zaidi, basi kwangu ni faraja kubwa mnanipa moyo wa matumaini na kunithibitishia kuwa timu iliyotoa mafunzo haya imefanikiwa kutimiza lengo," Dk. Mafumiko alisema.

Aidha, aliwataka kutumia elimu waliyopata kuwaelimisha madereva wengine ambao hawajafanikiwa kupata mafunzo kwa lengo la kuepusha ajali za kemikali na kulinda afya ya binadamu na mazingira.

"Vyeti mlivyopewa leo isiwe ni kama pambo au sifa tu ya kuonyesha umepitia mafunzo kuhusu usafirishaji salama wa kemikali bali mnapaswa kuvitumia pamoja na elimu mliyopatiwa kusaidia kuepusha ajali za kemikali ikiwamo kuwaelimisha madereva wenzenu ambao hawajafanikiwa kupata mafunzo ili kulinda afya za binadamu na mazingira," Dk. Mafumiko alisisitiza. Mmoja wa madereva hao, Theobald Makanji, akitoa neno la shukrani kwa niaba ya madereva wenzake walioshiriki mafunzo hayo, alisema mafunzo waliyopata ndani ya siku mbili yamewabadilisha na kuwajiona ni madereva wapya watakaofanyakazi kwa ufanisi mkubwa.

"Kwa niaba ya madereva wenzangu tunashukuru kwa mafunzo mazuri maana yametubadilisha na kutufanya kuwa madereva wapya. Sasa tunaelewa namna ya usafirishaji salama wa kemikali kuanzia kwenye maandalizi ya mzigo kupakia, kusafirisha na mpaka kushusha.

Kemikali ni muhimu na ni hatari hivyo usafirishaji wake unapaswa kuwa na umakini ili ifike salama. Tumepata mafunzo katika hali ya weledi mkubwa na tumependa na tunaahidi kuwa mabalozi wazuri barabarani," Makanji alimaliza kusema.

## Shirika lajipanga kutokomeza ukatili wa kijinsia Simiyu

**Na Happy Severine,** ITILIMA

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali la Kawiye Social Development Foundation (KASODEFO), limesema limejipanga kuhakikisha linatoa elimu ili kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wilayani Itilima mkoani Simiyu.

Mbali na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, pia kumekuwapo kwa vitendo vya ukatili wa vipigo, ndoa za ututoni na ukatili wa kiuchumi vimeonekana kushamiri wilayani humo hali inayorudisha nyuma ukuaji wa uchumi wa familia na maendeleo kwa ujumla.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo jana, Mkurugenzi wa KASODEFO, Ezekiel Kassanga, alisema mradi huo unalenga kutokomeza vitendo na aina zote za ukatili wanaofanyiwa kinamama na watoto majumbani.

Alieleza kuwa katika mradi huo wanakusudia kuchangia jitihada za utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) wa mwaka 2017/18 hadi 2021/21.

"Katika mradi huo asasi inakusudia kujenga na kuimarisha uelewa wa wanajamii kuhusu kuepuka na kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike, hasa masuala ya ndoa za utotoni, vipigo kwa wanawake na ukatili wa kiuchumi... baada ya mavuno wanawake wamekuwa hawapati kipato sawa na wanaume," alisema Kassanga.

Aliongeza kuwa dhamira kuu ni kuiwezesha jamii ya Itilima kuwa na uthubutu wa kuchukua hatua endelevu katika kukomesha vitendo vyote vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wilayani humo.

Alisema utekelezaji wake utahusisha mafunzo kwa njia ya vyombo vya habari, machapisho, maonyesho ya barabarani, sinema, warsha kwa wanajamii, wanawake, watoto na wadau wengine wakiwamo viongozi wa serikali za mitaa na vijiji.

Mradi huo unaofadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), unatarajia kuwafikia wanajamii 60,000 na utagharimu Sh. 50,000,000 na umelenga kuimarisha mfumo wa utokomezaji wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kuzingatia malengo ya kitaifa.

# Longido wamtupia lawama mkandarasi

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WAKAZI wa Kata ya Tingatinga Tarafa ya Enduiment Wilaya ya Longido mkoani Arusha, wamelaani kitendo cha mkandarasi aliyehusika kutandaza mabomba kutoka chanzo cha maji Mto Simba hadi makao makuu ya wilaya hiyo kutokufanya kazi kwa umakini, na kusababisha migongano kati ya wananchi na viongozi.

Diwani wa kata hiyo, Peter Lekanet, wakati akiwasilisha changamoto zao kwa Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, alidai serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 15 kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji kwa wakazi wa Longido ambao zaidi ya kilomita 30 za mradi huo umepita katika kata yake.

"Rais ametujalia wana-Longido, lakini mkandarasi aliyehusika na ulazaji wa mabomba kutoka chanzo kikuu hadi tangi kuu Longido kuna vitu hajaviweka sawa, kwa kuwa walidai bado wapo kwenye matazamio tunaomba warekebishe madhaifu yao," alisema Lekanet.

Lekanet alikemea kuwapo kwa matukio ya kukamatwa kwa wananchi wa kata hiyo pamoja na viongozi na kufikishwa kituo cha polisi kwa kile kinachodaiwa kuhusika kuhujumu mradi huo unaotokea Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro kuelekea Wilaya ya Longido, na kuitaka serikali kuingilia kati changamoto zilizopo katika mradi huo. "Wananchi wengi wa kata hii wamekimbia na mifugo yao kwa kuhofia usalama wao...mabomba haya yanavuja hayajaunganishwa vizuri kwenye viungo," alisema na kuongeza:

"Hakuna mwananchi wa kawaida anaweza kupasua au kutoboa. Leo wanasumbua wananchi ili ionekana ni wananchi wameharibu."

Naye Mbunge Dk. Kiruswa alisema amepitia mradi huo wa Mto Simba na kujionea madhaifu yaliyopo ikiwamo baadhi ya chemba kuachwa wazi bila mifuniko na maeneo mengine kuwapo kwa maji kuvuja.

"Nimepita na nimeona mkandarasi hajafunika chemba hizi. Eneo hili lina wanyama waharibifu, lakini pia watoto wawapo machungani wanaweza kugonga na mawe na kuhujumu mradi huu...kuna tatizo kwa mkandarasi kwa kweli," alisema Dk. Kiruswa.

Aliwataka wananchi hao kukemea mtu yeyote mwenye mawazo yakutaka kuhujumu mradi huo wa fedha za serikali na kuwataka kuwa wazelendo katika kutunza miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao.

Mkurugenzi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Arusha (AUWSA), Mhandisi Ruthi Koya, alipokuwa akiwasilisha taarifa ya mradi huo hivi karibuni kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, kwenye hafla ya makabidhiano ya mradi huo kutoka wilaya ya Longido na kusimamiwa ma mamlaka ya maji mkoa wa Arusha, alisema mradi huo umekamilika na kwa sasa upo kwenye hatua ya uangalizi kwa mwaka mmoja.



Mwalimu wa Mazingira wa Shule ya Sekondari Mirerani B.W. Mkapa, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Ally Juma, akiwaeleza baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo umuhimu wa kutunza mazingira yanayowazunguka jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Waziri ataka Watanzania kutumia bidhaa za ndani

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa amewataka Watanzania kujenga tabia ya kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani ili kuviwezesha kujiendesha na kuwa na masoko ya uhakika kwa maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa taifa. Bashungwa alitoa kauli hiyo jijini hapa juzi alipotembelea kiwanda cha A to Z na Sunflag vinavyozalisha nguo na kuwataka Watanzania kuacha kukimbilia mavazi ya mitumba yanayotoka nje ya nchi badala yake wajijengee utamaduni wa kununua bidhaa zinazozalishwa nchini.

Waziri huyo pamoja na kupongeza uzalishaji wa bidhaa katika viwanda hivyo vikubwa katika Mkoa wa Arusha vinavyoongoza kuajiri wafanyakazi wengi, alisema adhima ya serikali ni kuhakikisha viwanda vinaongeza uzalishaji wa bidhaa bora zitakazomudu ushindani katika masoko ya kimataifa.

"Viwanda vyetu vijitahidi kuongeza uzalishaji na serikali ipo tayari kusaidia kutangaza bidhaa za ndani kuuzika nje ya nchi," alisema. Awali Meneja wa Kiwanda cha Sunflag kilichopo Njiro jijini hapa, Harun Mahundi, aliiomba serikali kukubali viwanda vyake kutumia wataalamu wa kigeni ili ujuzi wao uweze kuwasaidia Watanzania kuwa na uelewa katika uzalishaji wa ubora wa bidhaa.

"Tunaiomba serikali iruhusu wataalamu kutoka nje ya nchi kuajiriwa hapa nchini ili watusaidie kutufundishia vijana wetu wapate ujuzi utakaotusaidia kuzalisha bidhaa bora katika viwanda vyetu," alisema Mahundi.

Naye Ofisa Biashara na Masoko wa Kiwanda cha A to Z, Sylvester Kazi, aliiomba serikali kuwaondolea ongezeko la thamani VAT katika bidhaa ya vyandarua wanavyozalisha kiwandani hapo.

Alisema jambo hilo limekuwa la muda mrefu na lipo ngazi za juu ila anaamini serikali ni sikivu na italishughulikia na kuhakikisha bidhaa hiyo inaondolewa VAT ili ipatikane kwa bei rahisi kuweza kuwasaidia wananchi kujikinga na mbu wanaoambukiza malaria.

## TRA yahimiza wafanyabiashara

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAMLAKA ya Mapato nchini (TRA), imewahimiza wafanyabiashara kuhakikisha wanatunza kumbukumbu zao, ili kurahisisha ukokotoaji wa hesabu na kuondoa mkanganyiko na malalamiko ya udanganyifu wakati wa kulipa kodi.

Rai hiyo ilitolewa na Naibu Kamishna Mkuu waTRA, Msafiri Mbibo, alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha pamoja na wafanyabiashara na mashirika yasiyo kuwa ya kiserikali mkoani Arusha kwenye ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa (AICC) kwa ajili ya kusikiliza kero zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema utunzaji wa kumbukumbu utawezesha TRA kukusanya kodi halali, hivyo wafanyabiashara hawatalalamika wala kukandamizwa.

Mbibo, alisema mamlaka imeboresha mfumo wa ulipaji kodi ambao umekuwa ni rafiki na kuwasisitizia matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD), ambazo zinarahisisha utunzaji wa kumbukumbu za mlipakodi.

Alisema mifumo hiyo itasaidia kuondoa baadhi ya changamoto na kuweka uwazi katika kukusanya mapato na kuondoa ukiritimba ili kila mmoja aweze kulipa kodi bila vikwazo.

Aliwataka wafanyabiashara wasitumie njia za panya kuingiza bidhaa toka nje, bali wahakikishe wanafuata taratibu na wawe wanaweka taarifa sahihi za bidhaa zao badala ya kuweka taarifa za udanganyifu ambazo zinaikosesha serikali mapato.

Wafanyabiashara wakichangia mjadala waliitaka TRA kukaa pamoja na wafanyabiashara waliofunga maduka kutokana na kudaiwa kodi kubwa ili waweze kufungua maduka na kulipa kodi wanazodaiwa taratibu. Kwa upande wake, Chama cha Madalali wa Madini (Tasgedo), kimeiomba TRA kukaa nao kuelimishwa namna ya kukusanya kodi kwa madalali wa madini kwa kuwa TRA haina mbinu wala ujuzi wa kukusanya kodi za madini.

Mwenyekiti wa Tasgedo, Khamis Rioba, aliitaka TRA ijadili kwa kina na madalali ili waweze kukusanya kodi kutoka kwa madalali hao, kwani imeonekana mamlaka hiyo haina utaalamu wa kukusanya kodi kutoka kwa madalali wa madini.

Pia waliiomba Wizara ya Madini kutowachanganya na leseni iwe moja, badala ya sasa kila mkoa kuwa na leseni yake, hivyo kuwakwamisha katika ununuzi na uuzaji wa madini, kwa sababu leseni hizo ni kikwazo kwa madalali wa madini nchini.



Kamishna wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (wa kwanza kutoka kushoto), akipokea maelezo ya shughuli za mradi huo kutoka kwa Mkandarasi wa Kampuni ya KEC Internatinal LTD ya nchini Kenya, Mhandisi Taj Sandeep alipotembelea mradi huo. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# Mama aliyetelekezwa afaidi mali

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MAMA wa watoto wanne, Sauda Mohamed (33), mkazi wa Same mkoani Kilimanjaro ambaye 'alitalikiwa' na mumewe kutokana na mgogoro wa ndoa kisha kutelekezwa watoto hao, ameanza kufaidi mali za mchumo wa pamoja baada ya Mahakama ya Mwanzo wilayani hapa kumpa ushindi.

Kwa sasa, Sauda anamiliki kiwanja kimoja katika mji huo na anapewa matunzo ya watoto ya Sh. 350,000 kila mwezi na uhusiano na watoto wake umerejea.

Mahakama ya Mwanzo Same, kabla ya kutoa uamuzi wa kuivunja ndoa hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ilijiridhisha kwamba ndoa hiyo haiwezi kuendelea na ikaivunja na mgawo wa mali za ndoa kugawanywa.

Akitoa simulizi ya mafanikio ya kazi iliyofanywa na Wasaidizi wa Kisheria Wilaya ya Same, Sauda alisema tatizo lililosababisha mgogoro huo ni yeye kuonekana tatizo na Julai, mwaka jana, alifika kwa mara ya kwanza katika ofisi hiyo akiomba kusaidiwa ili kupata haki zake alizochuma na mumewe waliyeoana mwaka 2007.

"Mali hizo za mchumo wa pamoja alizigawa mume wangu tuliyeachana, lakini sikuridhika, hivyo nikaenda kwa wasaidizi wa kisheria Wilaya ya Same tarehe 20/7/2018 ili kupata msaada zaidi. "Mume wangu alipewa barua ya wito lakini hakufika katika ofisi hizo wala kwa ofisa ustawi wa jamii, Shirika la Wasaidizi wa Kisheria Same likakata tena rufani kwa Baraza la Kata Same na hatimaye Mahakama ya Mwanzo Same Mjini. Baada ya shauri kupokewa mwafaka ulipatikana kuwa ndoa hairekebishiki, hivyo kuvunjwa na mgawo wa mali za ndoa kufanyika."

Kwa mujibu wa Sauda, mgawo huo wa mchumo wa pamoja wa mali za ndoa umemwezesha kupata kiwanja kimoja na kila mwisho wa mwezi atapata Sh.350,000 na matunzo ya watoto na ataendelea kuishi na watoto wake na mume atawajibika kuhakikisha watoto wanasoma na kupatiwa matibabu.

Mama huyo alisema kwa mgawo huo wa haki, ameridhika na sasa anaishi kwa furaha bila bugudha yoyote.

Haki za wanandoa katika ndoa kwa mujibu wa sheria ya ndoa ni, mwanamume na mwanamke wana haki sawa katika ndoa. Haki za mke katika ndoa ni pamoja na haki ya kumiliki mali kama nyumba na shamba kwa jina lake mwenyewe, haki ya kutoa idhini katika uuzaji wa mali yoyote ya familia na haki ya kuishi katika nyumba ya familia iwapo mume amemkimbia.

Iko pia haki ya kupewa matunzo yake na ya watoto wakati wa ndoa au iwapo mume amemkimbia, wameachana kwa amri ya mahakama, haki ya kutokupigwa na au kufanyiwa ukatili wa aina yoyote, haki ya kupewa unyumba, haki ya kutumia mali ya ndoa na haki ya kuomba amri ya talaka dhidi ya mwenzi wake.

# Upimaji homa ya ini kutolewa bila malipo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HOSPITALI ya Rufani ya KCMC na Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikristo cha Tiba Kilimanjaro (KCMCo), vimetangaza neema ya kuanza kwa huduma ya upimaji wa homa ya ini kwa wananchi bila malipo.

Ugonjwa wa homa ya ini (Hepatitis B), umekuwa tishio kwa kuua, huku maambukizi yake yakitajwa kuongezeka kila siku.

Taarifa iliyotolewa jana na kuthibitishwa na Mkuu wa Idara ya Uhusiano ya KCMC, Gabriel Chisseo, ilisema huduma hiyo ya vipimo vya homa ya ini itafanyika kuanzia Julai 27 hadi 28, mwaka huu, nje ya majengo yake, kwenye eneo maalum la maegesho ya magari.

"Ni kweli tutafanya uchunguzi huo kwa siku mbili za Julai 27 na 28 kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:30 jioni kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Homa ya Ini Duniani ambayo hufanyika kila Julai 28," alisema Chisseo.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, utafiti wa mwaka 2018, takwimu za ugonjwa huo zimeongezeka tofauti na takwimu za mwaka 2017.

Takwimu za mwaka 2017, zinaonesha wachangiaji damu 233,953 sawa na asilimia 4.9 takribani watu 11,417 walibainika kuwa na maambukizi ya homa ya ini aina ya B.

Aidha, kwa mwaka 2018 vipimo vya damu vilivyofanyika kwa watu 307,835 vilibaini watu 13,613 sawa na asilimia 4.4 kuwa na maambukizi ya homa ya ini aina ya B na uwepo wa maambukizi ya homa ya ini aina C kwa watu 1,092 sawa na asilimia 0.35.

Inaelezwa na wataalamu kwamba chanjo ya homa ya ini hutolewa kwa miezi mitatu mfululizo, ambapo mtu huchomwa sindano moja kila mwezi.

Ugonjwa wa homa ya ini, ni ugonjwa unaoshambulia ini na husababishwa na virusi au bakteria wa makundi yaliyogawanyika katika aina za Hepatitis A, Hepatitis B, Hepatitis C na Hepatitis D.

Wataalamu wa afya wanasema ugonjwa huo, kusababishwa na fangasi, unywaji wa pombe, dawa, magonjwa yanayosababishwa na kinga ya mwili kuushambulia mwili (auto immune) na magonjwa ya kimetaboliki.

Hata hivyo, Shirika la Afya Duniani (WHO), mwaka jana lilitoa takwimu zinazoonyesha kuwa takriban ya watu milioni moja hupoteza maisha duniani kote kutokana na ugonjwa huo kwa mwaka.

Kwa mujibu wa shirika hilo, ugonjwa wa homa ya ini umekuwa hatari kwa sababu una virusi vyenye uwezo wa kuishi nje ya mwili wa binadamu, wakati virusi vya ukimwi haviwezi kuishi nje ya mwili wa binadamu hata kwa dakika moja.

# Wapata mwanga mfumo wa elimu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUFUNZI Mkazi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Amina Mbughi, amewaondoa fikra hasi wananchi mkoa wa Kilimanjaro kuhusu tofauti ya mfumo rasmi wa elimu ya sekondari na mfumo usio rasmi.

Mbughi amesema mfumo usio rasmi unatolewa nchini ili kuondoa vipingamizi vinavyopatikana katika mfumo rasmi wa elimu.

Alitoa ufafanuzi huo jana wakati akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa jengo jipya la hosteli ya wasichana ya Kiwoce Open School iliyoko katika Kijiji cha Msasani, Moshi Vijijini yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80.

"Kazi yangu mimi na Ofisa Elimu Sekondari haiwezi kutenganishwa. Nieleze tofauti iliyopo ni kwamba elimu ya mfumo usio rasmi inatolewa kwa kuondoa vipingamizi vinavyopatikana katika mfumo rasmi," alisema Mbughi.

Alisema elimu katika mfumo usio rasmi ni sawa na elimu iliyo katika mfumo rasmi ambao Mkoa wa Kilimanjaro peke yake ina vituo zaidi ya 30. Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Juma Tukosa, akizungumza na wanafunzi, wadau wa elimu na wazazi wa wanafunzi wanaosoma katika kituo hicho alisema serikali inatambua vituo vyote vinatoa mfumo usio rasmi ni sawa na mfumo rasmi.

Mkurugenzi wa Kiwoce Open School, Graceanna Lyimo, alisema licha ya kupata mafanikio katika sekta ya elimu, ndoto yake kubwa aliyonayo ni kuhakikisha kituo hicho kinakua kwa ajili ya vijana wanaotoka katika mazingira magumu.

"Ndoto yangu nyingine niliyonayo sasa hivi ni kwa wale ambao hawawezi kusoma na kuandika lakini kwa vitendo wanaweza wakafanya. Mfano tuna wasichana wa kazi za ndani wanaochukuliwa kwenda kufanya kazi anaweza kupika na kufanya kila kitu lakini hawezi kupata ajira. Hivyo ndoto yangu ni kuwainua vijana ambao hawawezi kusoma kitaaluma na wanaweza kufanya kwa vitendo," alisema.

Kwa mujibu wa Lyimo, awali ndoto yake ilianza mwaka 2007 alipoamua kubadili eneo kilipojengwa kituo hicho ambacho ilikuwa ni sehemu ya wanawake kukutana na kujifunza mambo mbalimbali ya kujiinua kiuchumi kama vile kilimo na biashara ndogo ndogo.

Awali, akisoma risala ya wanafunzi wa kituo hicho cha Kiwoce Open School, Angel Emanuel alisema katika kumjengea msichana mazingira rafiki ya kujifunzia ili aweze kufanikisha malengo yake.

Pia alisema hali hiyo inatokana na changamoto zinazowakabili wasichana, shule yao inatilia mkazo uwezeshaji wanafunzi wenye mazingira magumu kwa vile bado jamii haijajielekeza kwa dhati kutatua changamoto hiyo.

ama
ALHAMISI JULAI 25, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 19

## Dawasa: Mwisho kilio cha maji



Ukurasa 18

Umewasikia vinyonga wenye pembe mbili?



Ukurasa 14

## Uvutaji sigara 'kukomeshwa' ifikapo 2030?



# TPRI yashtukia janga vifungashio viuatilifu 'vinawamaliza' wakulima

Ukurasa 14

## Uvutaji sigara 'kukomeshwa' ifikapo 2030?

SERIKALI ya Uingereza imetangaza kampeni kubwa kwa wananchi wake wavuta sigara, wapunguze ya kuacha kabisa sigara ifikapo mwaka 2030.

Wanafanyaje? Katika moja ya mikakati ni kwamba, kila mgonjwa anayelazwa hospitalini anapewa 'ofa' ya kuachishwa sigara;

Katika mkakati wake, mtazamo wa serikali unajielekeza katika kudhibiti magonjwa yanayozuilika, kisukari kikiwamo katika orodha ya mpango huo ambao ni mkakati wa kisera uliotolewa hivi karibuni.

Imegundulika, sehemu kubwa ya raia wanatumia kati ta miaka 16 hadi 19 ya maisha yao wakiugua, ikiwa ni sawa na asilimia 20 ya umri wanaoishi, visa vikuu ni maradhi hayo.

Pia, wanafunzi wa chekechea na elimu ya msingi wamefikiwa kwa mpango wa kupigishwa miswaki ya ziada; watu kusimamiwa muda wa kulala unaostahili, ili kuwa salama kiafya.

Lingine ni kwamba mapambano ya kisukari kuongezewa bajeti, ikizingatiwa aina ya pili ya kisukari inapatikana kupitia tabia binafsi ya mtu, hasa katika mlo.

Hata hivyo, mara tu waraka huo ulipotolewa, wapo waliouponda kwamba 'si chochote.' **BBC**



Mtu akivuta sigara. **PICHA: MTANDAO.**

MAZINGIRA

# TPRI yashtukia janga vifungashio viuatilifu 'vinawamaliza' wakulima

## • Babati walia: Kansa, tumbo, mapunye



Mtaalamu wa taasisi ya TPRI akitoa elimu kwa washiriki kuhusu vifungashio vya viuatilfu na athari zake kwa wakulima. **PICHA ZOTE: MARY MOSHA**

**Na Mary Mosha,** BABATI

JAPO kilimo kinatajwa kuajiri asilimia 60 ya Watanzania, lakini bado ni sekta inayochangia asilimia 30 ya pato la taifa, huku ikikabiliwa na changamoto nyingi na za aina mbalimbali, ikiwamo ukosefu wa elimu ya matumizi bora ya vifungashio vya viuatilifu.

Ni mapungufu yanayochangia baadhi ya wakulima nchini kukumbwa na magonjwa mbalimbali, hata kiasi cha kudhuru uhai wao, baadhi yanatokana na shughuli zao za vyakula na malighafi kwa ajili ya uzalishaji viwandani.

Katika kupata undani wake, Nipashe ilimtafuta Mwema Felix, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa Viuatilifu na Utunzaji Mazingira kutoka (TPRI), anayekiri, utafiti wa awali zilionyesha asilimia kubwa ya wakulima wilayani Babati

> **Mpaka sasa tumechelewa sana kupewa hii elimu na tunaiomba serikali ya kijiji, kata na wilaya kutumia hii kama ajenda kuu.**

Anasema, viuatilifu wanavyotengeneza kwa ajili ya kuzalisha mazao ya chakula na biashara, tatizo kuu ni kutojua matumizi sahihi ya utunzaji vifungashio, hali inayochangia madhara kwa afya ya jamii zinazowazunguka.

Felix anasema utafiti huyo uliofanyika mwezi Machi mwaka huu, ulihusisha kata tano zilizoonyesha kuwa kwa kipindi cha kila mwezi mmoja, watu 29 wanapata madhara bila ya kujua, kutokana na kutumia vifungashio vya viuatilifu.

Kwa mujibu wa Felix, hizo ni taarifa za kiafya kutoka kwa wanaofikishwa hospitalini kwa ajili ya matibabu, chanzo kikubwa ni kukosa matumizi potofu ya vifungashio vya viuatilifu.

Anarejea takwimu katika wilaya ya Babati, kwamba kuna kata 25 zenye jumla ya wakazi 370,175 wasio na elimu juu ya matumizi mabaya ya viuatilifu, yanayosababisha madhara kwa jamii, baadhi kufikia hatua ya vifo.

### HATUA ILIYOCHUKULIWA

Felix anataja hatua iliyochukuliwa ni kujikita zaidi katika kuielimisha jamii ya wilayani hapa, wakiwemo wasambazaji wa viuatilifu, wauzaji pamoja na watumiaji wa viuwatilifu lengo ni kumkomboa mkulima katika maradhi yatokanayo na viuatilifu.

"Ikiwa vifungashio vya viuatilifu havitasafishwa vyema mara baada ya kumalizika kwa matumizi ya sumu, asilimia 10 hadi 14 hubaki kwenye vifungashio, hivyo kusababisha madhara kimazingira na kiafya, kutokana na baadhi ya wakulima kuvitupa kando kando mwa maji," anasema.

Felix anaongeza: "Maji hayo ambayo hutumika na watu wengine kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo ya binadamu na wanyama, hali inayochangia ongezeko la madhara kwa jamii, ikiwamo miwasho, ugonjwa wa ngozi (mapunye), kupata magonjwa ya tumbo, kansa na hata kupoteza uhai.

"Tumekuja na mpango wa kutoa elimu maalumu kwa jamii ya watu wa Babati kuhusu namna bora ya kusafisha vifungashio hivyo, mara baada ya kumaliza matumizi na kujenga vibanda, ambayo vitasaidia katika ukusanyaji wa vifungashio ili kuepuka kuvitupa ovyo.

"Sumu inapomalizika katika kifungashio, kilaze kifungashio kwenye bomba kwa sekunde thelathini, kisha weka maji kiasi yatingishe sekunde thelathini na urudie kwa mara tatu," anasema na kuongeza:

"Kisha toboa kifungashio hicho ili kisiweze kutumika kwa matumizi mengine ya binadamu na utapeleka katika eneo lililotengwa kwa ajili ya matumizi mengine."

Mtafiti wa Athari za Viuatilifu kwa Afya ya Binadamu na Mazingira kutoka TPRI, Raphael Mwezi, anasema, pia wanajaribu kuhakikisha kuwa vifungashio vyote vilivyobebea viuatilifu vinakusanywa kwa kutumia vifaa vya kujikinga.

Ombi lake kwa serikali za vijiji, kata na wilaya zishirikiane na wasambazaji wakubwa wa maduka ya viuatilifu mjini Babati, wanaopaswa kujenga vibanda vidogo karibu na mashamba ya wakulima, kwa ajili ya kusafisha vifungashio hivyo na kuvihifadhi katika sehemu moja.

MAZINGIRA

# TPRI yashtukia janga vifungashio viuatilifu 'vinawamaliza' wakulima

"Tunawaomba wakulima kufuata njia bora za usafishaji wa vifungashio na kuvitoboa, ili mtu yoote asiweze kutumia kwenye matumizi ya binadamu na baada ya hapo hakikisha chupa zote zinawekwa kwenye vibanda maalumu bila kutoa vibandiko vyake,"anasema.

### WANENAVYO WATEKELEZAJI

Ruben Aron, ni mkazi wa kijiji cha Magugu, Babati, anakiri kutumia vifungashio vya viuatilifu kwa matumizi mbalimbali, kama kuwekea maziwa, mafuta na hata maji ya kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

"Tumekuwa tukiokota vifungashio vya viuatilifu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ingawa zilikuwa hazioshwi ipasavyo na matatizo ya kiafya yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara, bila ya kufahamu chanzo cha changamoto hizo,"anasema.

Amosi Kagani, anasema asilimia 100 ya wananchi hawana elimu ya kutosha kuhusu utunzaji mazingira, badala yake wamekuwa wakisafisha vifungashio kwa maji ya moto.

Kagani anaeleza kuna wakati walitumia maziwa, wayanayoyaamini kuwa ina uwezo wa kuondoa sumu yote katika vifungashio ndani ya muda mwafaka.

"Watu wengi wamepoteza maisha kwa ajili ya kukosa elimu. Pia, tumeharibu mazingira kwa asilimia kubwa, kwani wapo baadhi yetu huchoma vifungashio vyao na kuvichoma.Tumechelewa kupata elimu hii na tunaomba serikali kutoa kwa Watanzania wote ili kuepuka madhara kama haya," anatamka na kuendeleza ufafanuzi:

"Baadhi ya vifungashio hasa vya makopo ya plastiki, hupendwa na wafanyabiashara kwa ajili ya kuuzia maziwa mtindi, pamoja na mafuta, bila ya kufahamu madhara ya sumu ambazo zinapatikana kwenye vifungashio hivyo,"anasema mwananchi, Martha nchimbi.

Anasema katika kundi la wanafunzi wa shule za msingi, huokota vingungashio hivyo vya viuatilifu kwa ajili ya kuwauzia wafanyabiashara, matumizi yakiganyanyika katika makundi ya: kutekea maji ya kumwagilia shambani pamoja na wapo wanaopikia majumbani.

Prisca Saidi anasema, baada ya kupata elimu wamebaini imekuwa chanzo cha madhara makubwa kwa wakazi wa Magugu, Babati kwani baadhi ya wananchi wamekuwa wakiviambatanisha na imani za kishirikina na magonjwa ya zinaa.

"Mpaka sasa tumechelewa sana kupewa hii elimu na tunaiomba serikali ya kijiji, kata na wilaya kutumia hii kama ajenda kuu, ili kuhakikisha tatizo hili linatokomea. Pia, tunaiomba Serikali kuangalia namna ya kutengeneza viwatilifu zisivyo na madhara,"anasema



> Nawaagiza watendaji wa vijiji, kata na wilaya kusimamia zoezi hili la uokotaji na uoshaji wa vifungashio vya viwatilifu ili kuokoa afya za wananchi wetu.



### SERIKALI

Elizabeth Mtundu, ni Mkuu wa Wilaya ya Babati, ambaye anaanza kukiri kuwapo uzagaaji wa vifungashio hadi kwenye vyanzo vya maji, hasa mashambani waliko wakulima.

Anasema, kupitia tafiti hizo zilizofanywa na serikali, kupitia wataalamu wa TPRI, ahadi yake ni kwamba serikali itahakikisha inachukua hatua za kukabili vitendo hivyo vinavyokaribisha adha za kiafya .

Mkuu wa Wilaya anasisitiza, itafanyika jitihada ya kuzunguka na kaulimbiu anayoitaja kwa jina la 'Babati bila ya vifungashio vya viuatilifu inawezekana.'

Sambamba na kauli hiyo, Elizabeth anawaagiza watendaji serikalini ngazi ya kitongoji hadi wilayani, kuhamasisha uokotaji wa vifungashio, ili kuhakikisha wanazitunza afya za wananchi wetu.

"Nawaagiza watendaji wa vijiji, kata na wilaya kusimamia zoezi hili la uokotaji na uoshaji wa vifungashio vya viwatilifu ili kuokoa afya za wananchi wetu.

"Hawa ni wazalishaji wakubwa wa chakula hapa nchini hivyo sisi kama serikali hatutakubali kuona jambo hili linaendelea kwani tumeshabaini linamadhara makubwa kwa jamii yetu," anasema Elizabeth

Aidha. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Babati, Hamis Malinga, anawataka wataalamu wote wa kilimo kuhakikisha wanatekeleza maagizo hayo, ili kutokomeza madhara yatokanayo na vifungashio vya viuatilifu.

"Halmashauri hii tunazalisha chakula cha kulisha kanda ya Kaskazini na kuuza nchi jirani ya Kenya, mwaka 2017/18 mazao ya nafaka tu ilipata tani 161,638 ambapo mahitaji yalikuwa tani 93,000, hii ni licha ya mazao yasiyokuwa ya nafaka ni tani 13,974 hii inaridhisha kabisa hivyo tutaweka jitihada kubwa kutoa elimu ili kuokoa wazalishaji wetu," anasema.

### MTAALAMU UMWAGILIAJI

Ofisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Halmashauri ya Babati (DAICO), Jetrida Kyewawa, anasema katika wilaya hiyo, udongo wa kilimo wa eneo hilo, haliwezi kufanikiwa kwa mavuno bora, pasipo kutumia viuatilifu.

Hivyo, anasema kupitia elimu hiyo, kunaweza kusaidia mabadiliko chanya kwa nchi nzima, kwani vyakula vinavyolimwa husambazwa Tanzania nzima.

AFYA

## KUELEKEA SIKU HOMA YA INI

# Pata uelewa, fahamu majanga, inavyobeba sura kamili ya uuaji



Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Homa ya Ini na Matumbo wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk John Lwegasha, alipozungumza na waandishi wa habari. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Sabato Kasika**

HOMA ya ini ni ugonjwa unaotajwa kuwa hatari na unaendelea kupoteza maisha ya watu, huku mataifa yote duniani yakitolewa wito wa kuongeza huduma za haraka za upimaji na matibabu dhidi ya homa.

Hiyo ni wito wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini Duniani kwa mwaka 2018, yaliyokuwa na kaulimbiu isemayo; 'Pima, Tibu, Homa ya ni'.

Inaelezwa kwamba homa ya ini aina ya B na C huathiri watu milioni 325 duniani na ikiwa vidudu vyake havitibiwi haraka vina uwezo wa kusababisha saratani ya ini ambavyo viliuwa watu zaidi ya milioni 1.3 mwaka 2015.

Wakati nchi ikielekea katika maadhimisho hayo, Jumapili ijayo, Watanzania wanakumbushwa kuufahamu ugonjwa huo wa homa ya ini, kinga na tibalishe zake, ili waweze kuwa salama kiafya.

Mtaalamu wa afya, Dk. Anorld Pius, anaeleza kuwa homa ya ini ni ugonjwa unaoambukizwa kwa njia ya virusi vinavyoitwa HBV (Hepatitis B Virus), vinavyoingia mwilini na kushambulia, kabla ya kugeuka maradhi sugu.

"Zipo aina mbalimbali za homa hii na hutofautiana kutokana na mazingira ya utokeaji au usambaaji wake. Kwa Tanzania ugonjwa wa homa ya Ini B ndio aina kubwa ya ugonjwa, ambao unaiathiri jamii kwa kiwango kikubwa na ndio unaoongoza kwa vifo vya watu zaidi. Homa ya Ini B huathiri kwa virus," anasema.

> **Inampa nafasi kila mmoja kupimiwa kile anachostahili kulingana na fedha yake. Mizani inapima, aidha inakokotoa gharama.**



Kliniki ya homa ya ini ikiendelea

Dk. Pius anasema, takriban watu billion mbili duniani mwaka jana na wengine milioni 350 wanaishi na ugonjwa huo.

Pia, anasema kuna watu 600,000 wanapoteza maisha duniani kila mwaka na homa ya ini (Hepatitis B) na ugonjwa huo usipotibiwa hutengeneza uvimbe katika ini na kusababisha maradhi ya saratani ya ini na kuishia vifo.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anaieleza homa ya ini kuwa "inaua taratibu, tofauti na magonjwa mengine" huku akifafanua kwamba dalili zake huchukua muda mrefu kujulikana na kujitokeza wazi.

Kwa mujibu wa Ummy, chanjo ilitarajiwa kuanza kupatikana kwa wananchi wote bila kujali kigezo cha umri wala uwezo wa kifedha kwa wananchi wenye hatari au ugonjwa wa ini kwa bei nafuu hadi kufikia mwaka 2020.

Aliahidi kwamba ni miongoni mwa matazamio yaliyokuwapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 na kwamba chanjo hiyo ya homa ya ini kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, sasa inapatikana kwenye vituo vya huduma ya afya vya serikali na watu binafsi.

Waziri Ummy, anabainisha kuwa sehemu kubwa ya wanaotumia dawa za kulevya kwa kujidunga sindano, nao ni wahanga wa matumizi hayo na kuepuka ngono zembe.

### UNAVYOAMBUKIZWA

Daktari huyo anasema, katika maeneo hatari zaidi duniani, virusi vya 'Hepatitis B' kwa kawaida husambazwa kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kuzaliwa au kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, hasa utotoni.

"Kama ilivyo kwa (virusi) Ukimwi, virusi vya homa ya ini pia huambukizwa kwa njia ya kujamiiana, mate, jasho na mwingiliano wowote ule wa damu," anasema.

Anazitaja njia kuu za maambukizi kwa mwenye ugonjwa huo wa homa ya ini ni kujamiiana ya bila kinga; kugusana ndimi; mama mwenye ugonjwa kumwambukiza mtoto wakati wa kujifungua; kuchangia damu isiyo salama; kuchangia vitu vya ncha kali kama sindano, wembe, miswaki; kuchangia taulo.

"Vilevile kubadilishana nguo au kukumbatiana wakati mkiwa mnavuja jasho, kwani tafiti za kitaalamu zinaonyesha kuwa virusi hivyo ni hatari kuliko hata vya Ukimwi, kwasababu vinaweza kuishi nje ya mwili wa binadamu (yaani nje ya mfumo wa damu) kwa siku saba," anasema Dk. Pius.

Anafafanua kuwa, virusi vya Ukimwi (VVU) havina uwezo wa kuishi nje ya mfumo wa damu kwa muda unaofikia dakika moja, tofauti na usugu wa HBV.

Dk. Pius anasema, virusi hivyo vinaishi kwenye ngozi, vitaendelea kuwa hai kwa siku saba na katika kipindi hicho mtu anaweza kuambukizwa kwa njia ya damu au jasho.

"Kwa wastani kirusi cha HBV kikishaingia mwilini, hupevuka ndani ya siku 75, hata hivyo upo uwezekano wa kupevuka kati ya siku 30 hadi 180. Pia ndani ya siku 30 hadi 60, mtu mwenye HBV anaweza kugundulika ikiwa atapimwa," anasema.

Mtalaamu huyo analinganisha afya ya mwenye homa ya ini kuwa ana wastani mdogo wa kuhimili kuishi, kuliko mwenye Ukimwi.

### DALILI ZAKE

Anasema wengi wenye hoima ya ini, kwamba hawaonyeshi dalili yoyote na kwamba mtu anaweza kuishi na HBV na kusababisha maambukizi kwa wengine bila kugundulika, lakini pia wengine husumbuliwa na homa kali, dalili ambazo hudumu kwa wiki kadhaa.

"Dalili za ugonjwa huo ni uchovu, kichefuchefu, mwili kuwa dhaifu, homa kali, kupoteza hamu ya kula, kupungua uzito, maumivu makali ya tumbo upande wa ini, macho na ngozi kuwa vya njano na mkojo mweusi," anasema.





> **Kama ilivyo kwa (virusi) Ukimwi, virusi vya homa ya ini pia huambukizwa kwa njia ya kujamiiana, mate, jasho na mwingiliano wowote ule wa damu.**

Anaongeza kuwa, wagonjwa wengine katika virusi vya Hepatitis B hukua hadi kusababisha ini kuharibika kabisa au kuzaa saratani ya ini.

"Chanjo, kutumia kinga wakati wa kujamiana, kuacha kuchangia vitu vya ncha kali kama sindano, wembe, miswaki, kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu na kutochangia damu isiyo salama.

### PICHA HALISI

Dk. Pius anasema kwa sehemu kubwa watoto wachanga huambukizwa katika umri chini ya mwaka mmoja na kiwango kidogo inawaangukia watu wazima.

Homa ya ini imekuwa tishio kwa kuua nchini, huku takwimu za mwaka 2017 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, zinaonyesha kuwa wachangiaji damu 233, 953 waligunduliwa kuwa na maambukizi ya homa ya ini aina ya B.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Catherine Sungura, alitamka Mei mwaka huu, kwamba mwaka jana, vipimo vilifanyika kwa watu 307, 835, kati yao walibainika watu 13, 613(asilimia 4.4).

## Kulipuka malaria 'majuu' tishio jipya la janga Afrika

UCHUNGUZI umefanyika kwa vimelea vya vinasaba (DNA) vinavyoonyesha usugu wa malaria unaosambaa katika nchi za Cambodia, kama ilivyokuwa katika maeneo ya Laos, Thailand na Vietnam.

Watafiti kutoka Uingereza na Thailand, wanaeleza usugu wa vimelea vya ugonjwa wa malaria dhidi ya dawa muhimu, unaonekana kusambaa haraka katika Kusini Mashariki ya Asia.

Watafiti wanaeleza kuwa vimelea wamehama kutoka nchini Cambodia hadi Laos, Thailand na Vietnam, ambako nusu ya wagonjwa hawaponi kwa dawa zilizozoeleka.

Wanasema, malaria katika ukanda tajwa, unatibiwa kwa mchanganyiko wa dawa mbili, ambazo ni artemisinin na piperaquine, mchanganyiko ulioanzishwa nchini Cambodia, mwaka 2008.

Mwaka 2013, ndipo kukaanza kushuhudiwa mikasa ya mabadiliko ya kimelea kujenga usugu na utafiti wa hivi karibuni uliochapishwa katika jarida la kitabibu la Lancet linalohusu magonjwa ya maambukizi, ulitathmini sampuli za damu kutoka za wagonjwa wa Kusini Mashariki mwa Asia.

Uchunguzi wa vimelea vya vinasaba (DNA) ulionyesha usugu ulisambaa kote Cambodia kama ilivyokuwa katika maeneo ya Laos, Thailand na Vietnam.

Pia, ulionyesha vimelea vilibadilika zaidi na kuvifanya kuwa tatizo katika baadhi ya kanda, asilimia 80 ya vimelea wa malaria vilikuwa sugu kwa dawa.

Mtaalamu Dk Roberto Amato, kutoka tasisi ya Wellcome Sanger, anaeleza: "Usugu huu umeenea na kusambaa na umekuwa mbaya zaidi."



Jamii inavyojihami na malaria nchini Cambodia. **PICHA: MTANDAO.**

Pia, utafiti mwingine uliochapishwa na jarida hilo hilo la Lancet, ulionyesha kuwa nusu ya wagonjwa hawakuweza kutibiwa na kiwango cha kawaida na sasa kuna dawa mbadala katika hilo.

"Huku kukiwa na hali ya kusambaa na kuimarika kwa usugu wa vimelea, matokeo ya utafiti wetu yanaonyesha dharura inayohitajika kutumia matibabu mbadala ya awali," anasema Profesa Tran Tinh Hien, mtafiti wa tiba katika Chuo Kikuu cha Oxford, alipokuwa ziarani, nchiniVietnam.

Hata hivyo, bado kuna hatua ya mafanikio makubwa katika kutokomeza ugonjwa wa malaria, huku katika sura ya pili, usugu unaleta tishio

Mtazamo katika suala la usugu wa uaigusa zaidi Afrika ambako maradhi hayo ni tatizo kubwa, huku mtaalamu, Profesa Olivo Miotto, kutoka taasisi ya Wellcome Sanger na Chuo Kikuu cha Oxford, ana ufafanuzi.

"Vimelea hawa wa malaria waliofanikiwa kuwa na usugu dhdi ya dawa, wana uwezo wa kuvamia maeneo mengine mapya na kupata 'jeni' (vinasaba) mpya, anasema na kuongeza:

"Hivyo kusababisha hofu kwa siku zijazo kwamba wanaweza kusambaa hadi Afrika ambako malaria iliwahi kujenga usugu miaka ya 1980 na kusababisha vifo vya mamilioni ya watu."

Watafiti wanachohimiza sasa ni dawa ambazo watu wanapewa baada ya kupata ugonjwa, zinapaswa kubadilika.

Tafiti pia zinaonyesha kuwa, hali hiyo inawakumbusha madaktari, wawe hatua moja mbele dhidi ya usugu wa vimelea vya malaria, unaojitokeza ili kuwapatia wagonjwa tiba sahihi.

Duniani kote, kunaelezwa kuna jumla ya takriban matukio milioni 219 vya malaria kila mwaka, ugonjwa ambao dalili zake ni pamoja na kusikia baridi mwilini, kutetemeka, hali inayofuatiwa na kupanda joto mwilini na kutokwa na jasho jingi.

Kitaalamu inaelezwa, pasipo na matibabu, vimelea vinaweza kumsababishia mgonjwa matatizo ya kupumua na kuharibika viungo vya ndani vya mwili.

Malaria inaua watu wapatao 435,000 kila mwaka duniani na wengi wao ni watoto walio na umri chini ya miaka mitano, kwa mujibu wa takwimu rasmi zilizopo. **BBC**

MAZINGIRA

# Umewasikia vinyonga wenye pembe mbili Hifadhi Magamba?

**Na Elizabeth Zaya**

KUNA umuhimu kwa Watanzania kuthamini vitu vyao kuanzia wanyama, mimea na hata bidhaa za viwandani, hali ambayo itachochea watu kuvutiwa na vya kwao badala ya kuviona havifai na kuhusudu vya wengine hasa kutoka kwa wageni.

Ni hamasa inayoibuliwa na baadhi ya watalii wa ndani waliotembelea hifadhi asilia ya Magamba iliyopo wilayani Lushoto mkoani Tanga kwa bei maalumu waliyoipata kutoka kwa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), msimu wa Sabasaba.

Safari ambayo chimbuko lake lilianzia katika maonyesho ya Saba Saba kwenye banda la TFS lililowasafirisha watalii wa ndani ambao wanasisitiza umuhimu wa kuthamini vya kwao na kuvipatia kipaumbele.

Mtalii wa ndani, Doreen George, anasema bado Watanzania wengi hawajatoa kipaumbele katika kuthamini vya kwao licha ya watu wengine kutoka nje ya Tanzania kuona umuhimu wake na kutumia gharama zao kuja kuangalia.

“Watanzania wengi bado hatujafahamu umuhimu wa rasilimali lukuki tulizonazo, tuna vitu adimu lakini bado hatuvipi kipaumbele lakini tunaona wenzetu wanasafiri kutoka mbali, nje ya nchi kuja kuangalia hivi vitu kwa sababu wanafahamu umuhimu wake, tufike mahali na sisi tubadilike, mimi leo nimeona na kujifunza vitu muhimu hapa Magamba,”anasema Doreen.

Miongoni mwa vivutio ambavyo viliorodheshwa na TFS vya kutembelea watalii hao wa ndani ni pamoja na Jiwe la Mungu, na maporomoko ya maji.

Pia, watalii hao wa ndani, walipata fursa ya kuona eneo maalum lililokuwa likitumiwa zamani kusafirisha magogo angani kutoka Magamba hadi Mombo kwa muda mfupi maarufu kama Skyline, vilele vya milima(view point) mapango ya Wajerumani, ndege wa tofauti na miti ya kipekee.

Utalii mwingine ni utalii wa mabwawa ya kipekee yaliyomo katika hifadhi hiyo pamoja na miti na mimea ya kipekee ambayo watafiti wengi wa dawa za binadamu wamekuwa wakiitumia.

**WATALII KIMATAIFA**

Watalii wa ndani walipofika eneo la Magamba, walijikuta wakifurahishwa na maelezo ya uzuri wa nchi yao baada ya kukutana na watalii wa kimataifa.

Imani yao iliongezeka zaidi kwa watalii hao wa ndani baada ya kukutana na watalii wengine Beata Hechtova na Jan Pisl ambao ni mke na mume kutoka Jamhuri ya Check huko Ulaya ambao wao walikuwa wameweka kambi katika maporomoko ya maji ndani ya hifadhi hiyo ya Magamba kwa siku mbili mfululizo, wakilala na kujipikia wenyewe humo.



Kinyonga akiwa katika Hifadhi ya Magamba, Lushoto. **PICHA: MTANDAO**

> **Sisi hatuogopi kwa sababu katika hifadhi asilia kama hizi huwa hakuna hatari kwa sababu hakuna wanyama wakali, tunafurahia sana kusikia sauti za ndege.**

Watalii hao walikuwa na hema moja ambalo walilitumia kulala na kuhifadhi baadhi ya nguo zao na pia walikuwa wametengeneza mafiga ya mawe ambayo waliyatumia kukoka moto wa kuuota ili kupasha miili joto pamoja na kupika chakula na kuandaa maji ya kunywa.

Watalii hao walitumia kibiriti cha kutumia gesi kuwashia moto na walikuwa wamebeba vyombo vichache vya kupikia, huku wakitumia maji hayo yanayotoka katika maporokomo katika matumizi yote ikiwamo kupikia.

Walipoulizwa kilichowavutia wanasema wanafurahia sana kuona mazingira kama hayo asilia ambayo kwao ni adimu.

“Tangu tumefika Tanzania tuna wiki ya pili sasa, lakini katika maporomoko haya ya Mkuzu hapa Lushoto, tumelala siku mbili na tulivyofika hapa tukapapenda zaidi, tukaamua kuweka tenti letu na bahati nzuri tulikuwa tumebeba mayai na chombo cha kupikia, kwa hiyo tunapika hapa ni siku ya pili,”anasema na kuongeza:

“Huko kwetu tulipotoka hatujawahi kuona vitu vya asili kama hivi, tunapenda sana kuona hali hii na tunafurahia kweli, tutakuwa tunakuja mara kwa mara kutembelea.

Walipoulizwa endapo hawaogopi kulala katika eneo hilo kwa sababu ni katikati ya msitu na kuna msongamano mkubwa wa miti, walisema hawaogopi kwa sababu wanaamini katika hifadhi kama hizo huwa hakuna mambo yoyote mabaya.

“Sisi hatuogopi kwa sababu katika hifadhi asilia kama hizi huwa hakuna hatari kwa sababu hakuna wanyama wakali, tunafurahia sana kusikia sauti za ndege,” alisema

Anaongeza: “Hata kama kuna wadudu wanaong`ata hawawezi kuja kwa sababu hawajazoea kusikia sauti za watu hivi na pia huu moto tunaowasha wanaogopa .”

Wanawashauri Watanzania, kupendelea kutembelea vitu vya asili kwa sababu wanajifunza mambo mengi.

“Sisi tumetoka mbali kuja hapa Tanzania kuangalia vitu kama hivi, na tumetumia gharama kubwa mpaka kufika hapa, tunatamani vitu kama hivi tuwe tunaviona kila siku lakini kwa kuwa tunaishi mbali hatuwezi, tunawashauri Watanzania wapendelee kutembelea vitu kama hivi kwa sababu vina faida,”alisema

Akizungumza kwa niaba ya watalii wa ndani, waliotembelea hifadhi hiyo ya Magamba kwa punguzo la Sabasaba, Fausta Shuma anasema kwa kutembelea katika hifadhi hiyo wamejifunza mambo mengi.

“Tunashukuru sana na tunaipongeza TFS kwa kazi kubwa wanayofanya kutunza rasilimali hizi za hifadhi asili, tulikuwa tunasikia tu lakini tumejionea kwa macho, Tanzania sisi ni matajiri na tuna vitu vizuri mnoo, binafsi nilikuwa sijafika Lushoto na Magamba lakini leo nimeweka historia katika maisha yangu,”anasema Shuma na kuongeza:

“Yaani naona kama ndoto kuona Jiwe la Mungu ambalo nilikuwa nalisikia tu, nimeona mahali magogo yalikuwa yanapita angani, nimetizama mambo mengi, kwa kweli nimepata cha kusimulia watoto wangu na wajuu na itabidi nipange niwalete na wao huku.” Anaeleza Shuma.

**VIVUTIO**

Mhifadhi Mkuu wa Msitu huo asilia Magamba, Gretuda Nganyagwa, anasema ndani ya hifadhi hiyo kuna kila aina ya kivuto cha utalii ambacho kila mtalii anayefika lazima avutiwe kuangalia na kwamba kadri watu wanavyotembelea ndivyo idadi inaongezeka na kuifanya kuwa kivutio zaidi ndani na nje ya nchi.

Anasema hifadhi hiyo imezungukwa na vijiji 21 na kati ya hivyo 17 vipo wilayani Lushoto na vingine vinne vipo katika Wilaya ya Korogwe.

Nganyagwa anasema hifadhi hiyo ina vivutio vingi ambavyo vingine havipatikani katika hifadhi nyingine ikiwamo Jiwe la Mungu na mlima wenye pango la Mjerumani alilolitumia kujificha wakati wa mapigano ya Vita vya Kwanza vya Dunia.

“Hifadhi yetu imekuwa ikitumika kwa ajili ya kufanya mafunzo, utafiti na kubwa zaidi inatumika kwa ajili ya utalii ikolojia na ndiyo maana tunatamani kuona Watanzania wengi wanakuja kushuhudia kwa macho haya ambayo tunayaeleza,” anasema Nganyagwa.

“Katika hifadhi yetu hii ya Magamba pia kuna vinyonga wa pembe mbili, nyani aina ya mbega, kuna wadudu wadogo na wakubwa, wanyama wakubwa ambao wapo katikati ya msitu na kadri siku zinavyokwenda idadi ya watalii wa ndani inaongezeka na hivyo kuchangia katika kuongeza pato la nchi yetu.” Anaongeza ofisa huyo wa TFS.

Anasema kwamba wao kama TFS wanaendelea kutoa hamasa kwa Watanzania kujenga tabia ya kutembelea vivutio asilia hususani katika hifadhi hiyo.

Anasema Hifadhi ya msitu asilia Magamba linavutia hata kupeleka familia ili kuwapa fursa hususani watoto kujionea na kujifunza mambo mbalimbali yanayopatikana humo hasa katika vipindi wanavyokuwa wamefunga shule.

Kwa upande wake Ofisa Misitu, Ugavi na Uenezi kutoka Wakala wa Misitu Tanzania Shaaban Kiulah, anasema wapo katika kampeni ya kuhamasisha Watanzania kujenga tabia ya kutembelea hifadhi za misitu ya asili ambako kuna vivutio vya utalii wa asili.

“TFS tunasimamia hifadhi za misitu ya asili 17 nchini, na hifadhi hizo ziko katika maeneo mbalimbali na kote huko watakaokwenda wataona namna ambavyo Mungu ameipendelea nchi yetu kwa kuweka kila aina ya kivutio cha utalii, tumekuwa na kasumba kwamba utalii eti lazima ufanywe na wenzetu tu wanaotoka nje, kwanini wao ndio wanapenda vitu vizuri na sisi hatupendi,” anahoji Kiulah.

“Wenzetu wanafahamu kwamba kuna faida kubwa kutembelea vitu kama hivyo, tusiwaachie pekee yao na sisi tuamke sasa, na tusione kwamba eti lazima tukaangalie wanyama tu, tufungue macho yetu zaidi, kuna utalii mzuri upo mwingi na uko katika historia zetu za nchi na tunausoma katika vitabu, kwa nini tuishie kuusoma wakati uko hapa hapa kwetu, tutembee tukajionee.” Anasisitiza.

AFYA

# Dawasa: Mwisho kilio cha maji

Na Frank Monyo

- Yaanza miradi yenye sura kimkakati
- Buza, Mwanagati, Vituka maji saa 24



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja, akitoa maelezo kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profresa Kitila Mkumbo, kuhusu ulazaji mabomba yatakayosafirisha huduma ya maji kutoka Kibamba, Wilaya ya Ubungo, hadi Kisarawe mkoa wa Pwani. **PICHA: MTANDAO**

MIONGONI mwa maswali ambayo kila mmoja ana jibu lake ni pamoja na: ni kiasi gani cha maji ambacho mtu anatakiwa kunywa kwa siku? Wapo wanaosema lita tatu mpaka tano kila leo. Wengine wanadhani kiwango kinategemeana na kazi au majukumu unayoyafanya, ukiwa mpishi kwenye jiko la kuni au mkaa unahitaji mengi zaidi.

Lakini, cha msingi ni kila mtu kunywa angalau lita mbili kila siku. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani ni lazima kupata angalau glasi nane au lita mbili ambazo ni sawa na nusu galoni na kanuni hiyo inawezekana iwapo maji yanapatikana kwa uhakika.

Kwa hiyo kwa wakazi wa Dar es Salaam kwenye joto jingi na sehemu ambayo maji hupotea kwa njia ya jasho ni dhahiri kuwa maji yanahitajika mno.

Lakini maji kwa siku nyingi yamekuwa tatizo kwa wateja wa sehemu nyingi jijini hapa zikiwamo Vituka, Mwanagati na Buza ambao walikuwa na shida ya maji kwa muda mrefu. Lakini nao kuanzia sasa watarajie kupata maji safi na salama anaahidi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa) Cyprian Luhemeja.

"Kwa muda mrefu wakazi wa Dar es Salaam na Pwani wamekuwa wakikabiliana na changamoto ya upatikanaji wa majisafi na salama, kwasasa adha hiyo inaelekea kuisha kwani tumedhamiria kumtua ndoo ya maji mama kichwani. Ifikapo Desemba mwaka huu. Kwa vile huduma ya maji kwa wananchi itakuwa inapatikana kwa asilimia 95."

Luhemeja anayasema hayo baada ya miezi michache tangu kusainiwa kwa mikataba ya miradi mikubwa sita ya majisafi inayotekelezwa jijini Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani.

Anaeleza kuwa kukamilika kwake kwa wakati kutamaliza changamoto ya upatikanaji wa maji kwa wakazi wa maeneo hayo.

Akizungumza na Nipashe wakati wa mahojiano maalaum, jijini Dar es Salaam, Mtendaji Mkuu Luhemeja anasema kuwa miradi hiyo mikubwa iliyosainiwa hivi karibuni ni mwendelezo wa kuondokana na kero ya maji Dar es Salaam na Pwani akieleza kuwa mikoa hiyo hasa Pwani ndiyo ukanda wa viwanda.

#### THAMANI YA MIRADI

Luhemeja anasema thamani ya miradi hiyo sita iliyosainiwa na Benki ya Dunia (WB) pamoja na makandarasi mbalimbali ina gharama ya Sh. bilioni 114.

Anasema kuwa miradi mitano kati ya sita iliyosainiwa inatekelezwa na Dawasa kwa kutumia fedha zake za ndani takribani Sh. bilioni 40 zitatumika.

"Dawasa hivi sasa tumeweka mikakati ya kuongeza makusanyo kwa lengo la kuendeleza na kuboresha huduma ya maji kwa kuendesha miradi ya maji kwa kutumia fedha zetu. Kati ya bilioni 114 ya miradi yote sisi tumetenga bilioni 40 kufanikisha miradi mitano ambapo mmoja kati ya miradi hiyo umesainiwa na WB," anasema Luhemeja na kuziainisha kazi hizo kama:

> **Mradi wa ujenzi wa bomba la usambazaji wa maji awamu ya pili unatekelezwa na mkandarasi na usambazaji maji utaanzia kwenye matangi ya Chuo Kikuu mpaka Bagamoyo.**



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (Dawasa) Mhandisi Cyprian Luhemeja, wakikagua ukamilishaji wa kazi ya kulaza mabomba kwa ajili ya kuwapatia maji wakazi wa Kata ya Madale.

#### MATANGI CHUO KIKUU

Luhemeja anasema kuwa mradi wa kwanza ni wa usambazaji wa maji kuanzia kwenye matangi ya Chuo Kikuu cha Ardhi mpaka Bagamoyo ambao unagharamiwa na Benki ya Dunia kwa mkopo nafuu ambao utekelezaji wake ni wa miezi 18 mpaka kukamilika.

#### WATAKAONUFAIKA

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, anataja sehemu zitakazofaidika na miradi hiyo itakapokamilika kuwa ni pamoja na wateja zaidi ya 750,000. Kulingana na usanifu wao kuna wateja wapya zaidi 64,000 wa majumbani watakaounganishwa na kuondokana na tatizo la maji katika maeneo ya Changanyikeni, Bunju, Wazo, Ocean by Zone, Salasala, Bagamoyo na Vikawe ambayo ni maeneo ya wilaya za Bagamoyo, Ubungo na Kinondoni.

Anaendelea kusema:" Mradi wa ujenzi wa bomba la usambazaji wa maji awamu ya pili unatekelezwa na mkandarasi na usambazaji maji utaanzia kwenye matangi ya Chuo Kikuu mpaka Bagamoyo."

#### MRADI WA JETI BUZA

Ofisa Mtendaji anasema kuwa mradi wa pili ni wa kusafirisha maji kutoka Jeti hadi Buza ambapo kazi ya kulaza bomba la kilometa 1.9 imekamilika na kipande kilichobaki cha kilometa 5.6 Dawasa inaendelea kukamilisha kazi hiyo.

Anasema kuwa lengo la mradi huo ni kuhudumia wakazi wa maeneo ya Kiwalani, Vituka, Buza, Mashine namba 5-Tandika na Mwanagati ambapo wateja takribani 173.810 wa kata za Vituka na Buza watapata huduma ya maji katika awamu ya kwanza.

Mhandisi Luhemeja anasema mradi huo ni miongoni mwa miradi ya kimkakati iliyopangwa kutekelezwa na Dawasa kwa mwaka 2019/20 ili kukidhi agizo la serikali la kuhakikisha ifikapo mwaka 2020 upatikanaji wa huduma ya maji inafikia asilimia 95 kwa maeneo ya mjini.

Anasisitiza kuwa kusainiwa kwa mikataba hiyo kutawezesha kubadilisha maisha ya wakazi wa

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Mtaalamu TGNP: Ukatili kijinsia sasa wahamia kwa wavulana

**Na Yasmine Protace**

MATUKIO ya ukatili wa kijinsia yamekuwa yakiripotiwa mara nyingi katika vyombo vya habari, kukiwapo kawaida ya kuripotiwa yalikotokea.

Ni mambo yanayotawala kwa wahusika wote yakitokea kwa watoto,watu wazima na kuhusisha jinsia zote mbili, kinyume na zamani wavulana ilikuwa adimu .

Baadhi ya watu wanadai, kuna ukosefu wa elimu na imani za kishirikina zinahusishwa kuchochea matukio ya ukatili, ambayo yamekuwa yakiwakumba zaidi watoto wa jinsia zote. Hiyo inatokana na ukweli baadhi ya matukio yanabaki na maswali yasiyojibika, kupata sababu na mantiki ya kutokea kwake.

Inaelezwa kuwapo tofauti, kwamba awali ilizoeleka kusikika motto wa kike kafanyiwa ukatili wa kijinsia, jambo ambalo sasa lina mabadiliko makubwa zaidi, kwamba yanachachamaa kwa wavulana.

Wachambuzi wanainisha kwamba, kila matukio hayo yanapofanyika, hukutwa aliyefanyiwa anapotakiwa kuanika ukweli, hutawaliwa na hofu ya usalama wake katika jambo hilo, kikwazo kikubwa cha kushindwa 'kufunguka'ni hofu ya usalama wake na inaelezwa kuwa mzizi wa vikwazo ni elimu duni katika eneo hilo.

Hivi karibuni, wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mabibo, jijini Dar es Salaam, walikusanyika kutimiza ajenda yao ya pamoja ya kuanzisha klabu, inayolenga kuwatetea na kuwalinda katika masuala ya hali za jinsia na vita dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Mwajuma Idrisi, mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo, anasema kuanzishwa klabu hiyo ni furaha kubwa kwao wanafunzi, huku akifafanua: "Tunaipongeza TGNP Mtandao kwa kutuwezesha kupata klabu ambayo imekuwa mkombozi katika shule yetu."




Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mabibo ya jijini Dar es Salaam, wakijadili masuala ya ukatili wa kijinsia katika klabu walioanzisha. **PICHA: YASMINE PROTACE**

> **Jamii haina mwamko wa kuchukuwa hatua kwa watu wanaofanya matukio hayo.**

Anaongeza kuwa, hilo ni jambo linalowasaidia kufahamu jinsi ya kujikinga na matukio ya ukatili wa kijinsia, kupitia elimu.

Mwajuma, anaeleza kuwa, wao wanafunzi hivi sasa wanajitambua, kutokana na kuelimishwa jinsi ya kutoa taarifa na ushirikiano, pale wanapoona wamefanyiwa ukatili au kuna jambo ambalo halijakaa sawa.

Binti huyo anaongeza kuwa, klabu ya shuleni kwao imewasaidia kupatikana viongozi mbalimbali ndani ya shule yao.

Anataja mambo wanayoyajadili, ni kwamba klabu yao inazungumzia masuala ya ukatili wa kijinsia na wanajifunza elimu katika mustakabali salama, ikiwamo| hedhi salama.

Wito wa Mwajuma kwa TGNP Mtandao, ni kwamba wawasaidie kupata chumba cha kujisitili na chumba cha ushauri mahali walipo shuleni.

Anasema kutokana na kupatikaa elimu kupitia klabu hiyo, sasa wanatarajia kutoa elimu hiyo walioipata kwa wenzao wa shule jirani, ili nao wanufaikle katika hatua inayofanana na yao.

Mwanafunzi mwingine, Abdallah Hamisi, anasema kuwa elimu za ukatili wa kijinsia, zinapaswa kutolewa katika maeneo yote, akielekezea "mjini na vijijini" kwani matunda yake yataangukia kuisaidia jamii kupambana na matukio hayo.

"Vijijini, ukatili upo," anasema Hamisi na kuongeza: "jamii haina mwamko wa kuchukuwa hatua. kwa watu wanaofanya matukio hayo."

Happiness Jaffar, mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule hiyo, anasema kuwa wazazi wapatiwe elimu ambayo itakayosaidia kujikinga na matukio yanayokinzana na ustaarabu katika jamii.

Msichana anawashauri wazazi kuwa karibu na watoto wao, ili wasiwafiche baya la ukatili wa kijinsia linalowasibu.

**KUTOKA |TGNP MTANDAO**

Katika maoni yake, Ofisa Programu Mwandamizi wa TGNP Mtandao, Deo Temba, anasema kuwa mazingira ya sasa yamegeuka katika hatua mbaya, kwa kuanza kutawaliwa na matukuo ya kijinsia, watoto wa kiume kufanyiwa ukatili wa namna hiyo.

# Dawasa yatangaza 'stop' kilio maji

**INATOKA UK.19**

kubadilisha maisha ya wakazi wa Dar es Salaam pamoja na Pwani.

**VISIMA KIMBIJI, MPERA**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, anazungumzia kuhusu visima, akisema kuwa mradi wa tatu ni wa uchimbaji wa visima 20 katika eneo la Kimbiji na Mpera ambavyo vitazalisha maji lita milioni 260 kwa siku ambapo mradi huo unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu.

Anataja mkakati wa mamlaka hiyo kuwa umejikita katika kukamilisha visima vya Kimbiji kabla ya kwenda Mpera.

"Mradi wa Kimbiji uligawanywa kwenye awamu mbili, awamu ya kwanza ilihusu uchimbaji wa visima 20 na awamu ya pili ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kabla ya kujua wingi na ubora wa maji kutoka kwenye vyanzo vya maji chini ya ardhi kuthitibishwa kwa uhakika baada ya kuchimba," anasema Luhemeja

Anaongeza kuwa kutokana na mkandarasi wa kwanza aliyekuwa mgeni kushindwa kurejea kazini Dawasa imeingia mkataba na mhandisi mshauri mwingine ambaye ni mzawa ili kuendelea na kazi zilizobaki katika eneo la kipaumbele la Kimbiji ambapo amepewa muda wa miezi sita kuanzia Julai Mosi hadi Desemba 30 mwaka huu.

**MAJI KISARAWE –PUGU**

Mhadisi Luhemeja anautaja mradi wa nne kuwa ni wa usambazaji wa maji kutoka Kisarawe-Pungu- Gongo la Mboto-Pugu Station-Air wing-Ukonga hadi Majohe ambao unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni saba na kwamba kukamilika kwa mradi huo kutakuwa na maunganisho mapya zaidi ya 50,000.

Anasema katika mradi huo bomba kuu litakuwa na uwezo wa kusafirisha maji lita 2,880 kwa siku ambapo wakazi zaidi ya 450,000 watanufaika baada ya kukamilika.

**MAJI MKURANGA**

Mtendaji Mkuu anasema kuwa mradi wa tano utatekelezwa katika mji wa Mkuranga ambapo hali ya upatikani wa maji si ya kuridhisha kwani vyanzo vyote vya maji vimekauka na kufanya wakazi wa mji huo kutumia maji yanayotiririka kutoka kisima kilichochimbwa na Dawasa mwaka 2015 kwa ajili ya utafiti.

"Hivi sasa mtandao wa mabomba ya maji uliopo wenye urefu wa kilomita 11 unahudumia watu 4,500 kati ya watu zaidi ya 25,500 ambao ni sawa na asilimia 17.6.," anasema Luhemeja na kuongeza:

"Mkataba wa kwanza utahusu ujenzi wa tangi la uwezo wa kuhifadhi lita 1,5000,000 na kazi zingine zitakazofanyika ni ujenzi wa kisima au "sump" na ufungaji pamp tatu za kusukuma maji kutoka kwenye kisima hadi kwenye tangi la uchimbaji wa mtaro na ulazaji wa mabomba ya kupeleka maji kwenye matangi."

Anaongeza kuwa watu wa Dar es Salaam na Pwani wanahitaji maji hivyo ni kujumu la Dawasa kuhakikisha miradi hiyo iliyosainiwa na mingine inasimamiwa vizuri kwani itakuwa mkombozi na kubadilisha taswira ya tatizo la maji.

**MLANDIZI MBOGA**

Mhandisi Luhemeja anautaja mradi wa sita kuwa ni wa kusafirisha maji kutoka Mlandizi au Ruvu Juu hadi Kijiji cha Mboga kilichoko Chalinze ambapo utasaidia kuondoa kero ya maji katika maeneo hayo kutokana na kuongeza kwa watu na ujenzi wa viwanda unaoendelea katika eneo la Mboga-Chalinze.



# HABARI MBEYA

## Wananchi waombwa ushirikiano rasilimali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SHIRIKA la Mbarali Water Sanitation and Environmental Conservation (Mweco), linalojishughulisha na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali kwenye miundombinu ya afya, limewaomba wananchi kutoa ushirikiano wakati wa kutekeleza majukumu yake ili kuhakikisha raslimali hizo zinatumika ipasavyo.

Hayo yalisemwa juzi wakati wa uzinduzi wa mradi wa ufuatiliaji wa raslimali za umma (PETS) katika Sekta ya Afya, na Mratibu wa Mradi huo, Tatu Bester, ambapo mgeni rasmi alikuwa Ofisa Maendeleo wa Wilaya hiyo, Stephen Bitta kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune.

Alisema wananchi wanatakiwa kutoa ushirikiano huo kutokana na kwamba lengo la shirika hilo ni kuhakikisha jamii inapata huduma bora za afya kama serikali inavyokusudia wakati wa kuanza kutekeleza miradi hiyo.

Tatu alisema mradi huo unatekelezwa katika kata tatu za Wilaya ya Mbarali ambazo ni Lugelele, Utengule Usangu na Ruiwa ambazo zimejumuisha vijiji sita.

"Awali mradi huu ulikuwa unatekelezwa kwa kata nane, lakini mwaka huu mradi utatekelezwa katika kata tatu, hivyo wananchi wanatakiwa kutoa taarifa mbalimbali za sekta ya afya watakapoulizwa na maofisa wetu kwa lengo la kuimarisha huduma," alisema Tatu.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Terdey Mhagama, alisema lengo kuu la mradi huo ni kutaka kujua matumizi ya raslimali fedha katika sekta ya afya na miundombinu sambamba na uimarishaji na usimamizi wa rasilimali za umma.

Alisema mradi huo utatekeleza shughuli za kutoa mafunzo ya uchambuzi wa taarifa, ushiriki katika mikutano mbalimbali na kwamba mradi huo unafadhiliwa na Shirika la The Foundation for Civil Society.

Bita aliwataka watendaji wa mradi huo kutoa taarifa ya kile watakachokuwa wamekibaini kwa uongozi wa wilaya ili kujadili juu ya changamoto watakazokuwa wamezipata wakati wa utendaji wao.

Alisema ndani ya wilaya hiyo kuna baadhi ya changamoto katika idara ya afya hivyo kwa wale watendaji wa shirika hilo watakapoweza kufika maeneo hayo wahakikishe wanazifuatilia changamoto hizo kwa kina na ziwe msaada kwa taifa.

## Mwanamke matatani kwa tuhuma wizi wa kichanga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia Anna Ezekia (23), mkazi wa Kijiji cha Itumbi Kata ya Matundasi wilayani Chunya kwa tuhuma za kuiba mtoto mchanga ajulikanaye kwa jina la Anjela Anjely (09).

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema tukio hilo lilitokea Julai 21, mwaka huu majira ya asubuhi.

Alisema mtuhumiwa pia ana makazi mengine katika kata ya Igamba wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe, na alikuwa na mazoea na mama mzazi wa kichanga hicho kwa maelezo alikuwa anamtembelea mara kwa mara nyumbani kwake. Alisema baada ya Anna kutokomea na kichanga hicho, mama wa kichanga alitoa taarifa na ndipo Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi wa kijiji hicho walianza kufanya msako ambapo siku ya kwanza waliambulia patupu.

Matei alisema Julai 22, majira ya asubuhi kichanga hicho kilikutwa kimetelekezwa na mtuhumiwa porini katika kijiji jirani cha Mkola kikiwa hai ndipo walimsaka mtuhumiwa na kumtia mbaroni.

"Huyu mtoto alifanyiwa vipimo vya kiafya katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya na akabainika yuko salama, hili ni tukio baya sana maana hatujajua nia ya mtuhumiwa ilikuwa nini na pengine tungechelewa tungekuwa ameshamuua," alisema Kamanda Matei.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi, na kwamba baada ya uchunguzi huo kukamilika, mtuhumiwa atafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Aliwataka wazazi kuwa makini na watoto wao hasa watoto wachanga ambao bado hawajitambui kwa maelezo kuwa hao ndio rahisi zaidi kuibiwa.

Katika tukio lingine, Matei alisema jeshi hilo linamshikilia Michael Watson (25), mkazi wa Kijiji cha Kasasya Kata ya Mtanila wilayani Chunya kwa tuhuma za kukutwa na silaha za moto zilizotengenezwa kienyeji.

Alisema tukio hilo lilitokea Julai 22 majira ya asubuhi, na kwamba mtuhumiwa huyo ambaye anadaiwa kuwa mwindaji haramu, alikutwa nyumbani kwake akiwa na gobole mbili zilizotengenezwa kienyeji na risasi 53 ambazo zinatumika kwenye bunduki hizo.

Vilevile alisema alikutwa na fataki saba pamoja na unga wa baruti akiwa ameuhifadhi kwenye kopo, na kwamba silaha hizo alikuwa anazitumia kwenye uwindaji haramu wa wanyamapori.



Emmanuel Kalinga ambaye ni msimamizi wa bustani ya shamba la miti Sao Hill, iliyopo tarafa ya kwanza Irundi akionyesha namna mche wa mkaratusi ulioboreshwa unavyoandaliwa kwa wageni waliofika bustanini hapo kwa ajili ya kujifunza. **PICHA: NPIGAPICHA WETU**

## Bodi za shule za CCM zamwangukia Magufuli

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BODI za shule za sekondari zinazomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Mbeya, wamemwomba Mwenyekiti wa Chama hicho Taifa, Rais John Magufuli, kusitisha utaratibu wa malipo kwa kutumia namba ya kumbukumbu ambao umeanzishwa.

Kwa mujibu wa utaratibu wa mfumo huo, ada na michango mingine inayokusanywa kwenye shule hizo, zitakuwa zinaingizwa kwenye mfuko mkuu wa jumuiya kisha wenyeviti wa bodi watatakiwa kuomba mafungu kwa ajili ya uendeshaji wa shule.

Wakizungumza kwenye kikao maalumu, wenyeviti wa bodi za shule hizo walisema mfumo huo sio mzuri na utaleta madhara katika uendeshaji wa shule hizo na pengine kuporomosha hata ufaulu wa wanafunzi ambapo walisema madhara hayo yameshaanza kuonekana.

Mwenyekiti wa wenyeviti hao, Stanery Mwangomile, alisema katika Mkoa wa Mbeya shule za wazazi zipo 14 na saba kati yake zimeshaingia kwenye mfumo huo na zingine saba bado na kwamba mfumo huo umesababisha matokeo mabaya kwenye shule zilizoingia kwenye mfumo.

"Agizo lilitolewa bila kushirikisha bodi ambayo inajua changamoto za uendeshaji wa shule, tunaomba kukutana na Mwenyekiti wetu Taifa ili tumweleze changamoto zinazoweza kusababishwa na matumizi ya mfumo huu," alisema Mwangomile.

Alisema mfumo huo utasababisha changamoto kwenye uendeshaji ikiwamo kushindwa kutatua baadhi ya mambo hasa yanayotokea kwa dharura.

Alisema baadhi ya changamoto hizo ni chakula, magonjwa ya dharura kwa wanafunzi na matumizi mengine ambapo fedha hizo zikisha kusanywa zitahitajika mpaka kutuma maombi katika ngazi ya taifa.

Naye Mwenyekiti wa Shule ya Sekondari ya Ivumwe, Dk. Victoria Kanama, alisema kutokana na mfumo huo, baadhi ya shule ambazo zilianza kuutumia zimeshuka kitaaluma tofauti na ilivyokuwa awali kabla ya mfumo.


Alisema miongoni mwa shule hizo ni Sekondari ya Meta ambayo imekuwa ikifanya vibaya kitaaluma tofauti na shule zile ambazo hazijaingia kwenye mfumo wa kukusanya mapato katika kapu moja.

Dk. Kanama alisema watendaji wa Jumuiya wamekuwa wakiingilia utendaji wa shule pamoja na bodi, hali ambayo itasababisha shule hizo zishindwe kujiendesha na kusababisha aibu ya kushuka kitaaluma na pengine kupoteza mwelekeo na sifa za shule hizo.

"Tuna mifano ya baadhi ya shule ambazo zimeshaingia kwenye mfumo huo kwa muda wa miezi sita tu, lakini hadi sasa zimeshuka kitaaluma sana, na sisi tumeona tukikaa kimya hizi shule zitabakia vichekesho kwa taifa," alisema Dk. Kanama.

Katibu Mkuu Jumuiya hiyo, Erasto Sima, alisema lengo la kuanzisha mfumo huo ni kuangalia namna fedha hizo zinavyoweza kutumika ili kuepukana na madeni ambayo chama kimekuwa kikidaiwa.

Alisema kama kuna shule zitashindwa kutekeleza agizo hilo wakuu wa shule hizo waondoke kwani shule hizo sio zao ni mali ya chama na wakishindwa waondoke na kuziacha.





# Mtendaji, mgambo wadaiwa kumwomba rushwa mahabusi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) Mkoa wa Dodoma inamshikilia Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mlowa Bwawani na askari kanzu (mgambo), kwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh.400,000 kwa mahabusi.

Mkuu wa taasisi hiyo mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ofisa Mtendaji Luis Pearson ambaye anafanya kazi Kata ya Mlowa Bwawani wilayani Chamwino na mgambo Josephat Msambili.

Kibwengo alisema watuhumiwa hao waliomba rushwa kwa mahabusi mkazi wa kijiji cha Wiliko, Samwel Chilulumo.

Alisema walimkamata Chilulumo na kumweka mahabusu ya kata kutokana na madai ya ugomvi wa kifamilia na kumtaka awape rushwa ya Sh. 600,000 ili wamwachie huru.

"Huyu mahabusi aliomba apunguziwe kiasi hicho cha fedha na kufikia Sh.400,000 na kuomba atolewe mahabusu ili akatafute fedha hizo, lakini alikataliwa na wakaamua kwenda kutafuta mteja wa mbuzi 10 zilizokuwa nyumbani kwake ili ziuzwe kiasi hicho kipatikane ndipo aachiwe huru," alisema.

Mkuu huyo alisema baada ya kupata taarifa taasisi hiyo ilifanya uchunguzi na kubaini kuna vitendo vya rushwa na kuanza kulifanyia kazi suala hilo na kuwabaini watuhumiwa hao.

Kibwengo alisema baada ya uchunguzi wao, walibaini mtuhumiwa Msambili alikwenda kutafuta mnunuzi wa mbuzi na kumpeleka mahabusi (Chilulumo) kwa ajili ya kufanya majadiliano ya bei.

"Chilulumo ambaye alikuwa mahabusi walienda naye nyumbani kwake kuona mbuzi na kisha kurejea tena mahabusu ndipo wakakubaliana bei," alisema.

Kibwengo alisema imethibitika mnunuzi alitoa kiasi cha fedha hizo ambazo watuhumiwa walizipokea na kumwachia huru mahabusi huyo.

Hata hivyo alisema watuhumiwa hao wanatarajia kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kusomewa mashtaka baada ya taasisi hiyo kukamilisha uchunguzi wake.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa pale wanapoona kuna uonevu wa vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Sambamba na hilo, aliwataka watendaji wa kata, mitaa na vijiji kuacha tabia ya kuomba rushwa kwa jamii ili kuwasaidia kutatua matatizo yanayowakabili, badala yake wafanye kazi kulingana na maadili.

"Nawaomba watendaji muache kufanya vitendo hivyo kwa sababu ni kinyume na kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007," alisema Kibwengo.

# PSSSF yaboresha huduma kielektroniki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umeanza kutumia mfumo wa kielektroniki kuendesha shughuli zake ili kupunguza matumizi ya karatasi na kuondokana na malalamiko ya upotevu wa nyaraka za wanachama wake.

Hayo yalielezwa jana na Meneja Kiongozi Uhusiano wa mfuko huo, Eunice Chiume, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, jijini hapa.

Alisema mfumo huo unatumika kuhifadhi kumbukumbu mbalimbali na husaidia kuongeza ufanisi, kupunguza matumizi ya karatasi na utunzaji wa uhakika wa kumbukumbu. "Kwa hiyo mtu akileta barua masijala inaingizwa kwenye mfumo inamfikia ofisa husika kwa kutumia mfumo na si tena kutembeza faili. Na hata kushughulikiwa kwake ni haraka kwa kuwa ukiingia kwenye mfumo unaona ipo kwa nani na imeshughulikiwa kwa hatua gani," alisema.

Kuhusu mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao (GePG), Chiume alisema unatumika kukusanya michango ya wanachama, mapato ya uwekezaji na mengine.

Alibainisha kuwa mfumo huo umesaidia mwajiri kujifanyia tathmini ya michango inayoletwa PSSSF, kujitengenezea ankra za malipo, kutengeneza kumbukumbu namba za malipo, kuweka hesabu sawa, kuwezesha utoaji risiti kwa wakati.

"Huu mfuko umeongeza uwazi, ufanisi, kukusanya michango kwa wakati, mawasiliano rahisi na kutambua wanaowasilisha michango," alisema.

Aidha, alisema mfuko huo kwa mwaka huu ulishiriki Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Sabasaba ambapo jumla ya wastaafu 381 na wanachama wengine na wananchi 1,040 walihudumiwa.



Katibu wa kikosi kazi cha Taifa cha kuratibu mpango wa serikali kuhamia Dodoma na uratibu wa ujenzi wa Mji wa Serikali, Meshack Bandawe, akiwaonyesha waandishi wa habari (hawapo pichani) jengo la Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walipotembelea eneo hilo jana kuangalia maendeleo ya ujenzi wa mji huo eneo la Mtumba jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Abiria wa treni waendelea na safari

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

ABIRIA 1,294 wa treni iliyokuwa ikitoka Dar es Salaam kwenda Kigoma ambao walikwama kwa zaidi ya saa 15 kutokana na ajali ya treni ya mizigo iliyotokea eneo la Makutupora, wameendelea na safari.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alisema abiria hao waliondoka kituo cha Dodoma usiku wa jana.

"Kutokana na changamoto waliyoipata kwa kushinda siku nzima Dodoma kila abiria amepewa Sh. 8,000 kwa ajili ya chakula kabla hawajaanza safari kutoka kituo cha Dodoma," alisema.

Katambi alisema amekaa kikao cha muda na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) Stesheni ya Dodoma na kuelezwa sababu ya kukwama abiria hao ambazo ni kutokana na ajali hiyo.

"Nimefika hapa baada ya kuletewa malalamiko na baadhi ya abiria wenzenu ofisini kwangu, nikaona nifike kujionea kuna nini kilichotokea. Lakini naomba niwajulishe kutokana na ajali hiyo wasingeweza kuwaruhusu kuondoka hapa mpaka mafundi wakamilishe kazi hiyo," alisema.

Katambi alisema alijulishwa kuwa ajali hiyo ilitokea baada ya treni hiyo ya mizigo iliyokuwa na mabehewa 17 iliyokuwa ikitokea stesheni ya Saranda kuingia Makutupora, breki zake zilishindwa kufanya kazi na kuanguka kwenye stesheni ya Makutupora.

"Katika ajali hiyo mabehewa hayo yaliharibika na kuharibu pia miundombinu ya reli, hivyo mafundi walikuwa wakiendelea na kuondoa mabehewa yaliyoanguka na kutengeneza miundombinu hiyo," alisema Katambi.

Alisema baada ya kumaliza shughuli hiyo ya mafundi, ndipo treni ya abiria ikaruhusiwa kuendelea na safari.


Mkuu wa Wilaya alifafanua kuwa aliagiza uongozi wa TRC kuwapa huduma ya chakula kwa usiku huo na kuhakikisha kuwa abiria wa treni hiyo wanatumia huduma ya choo bila kutozwa fedha yoyote hadi watakapoondoka kwenye stesheni hiyo. Juzi abiria hao walimlalamikia Katambi kuwa wamekwama kuendelea na safari huku uongozi wa TRC ukishindwa kuwaeleza sababu ya kukwama kwao na wala kuwapatia huduma.

Mmoja wa abiria hao, Elifasi Masawe, aliyekuwa akienda Kigoma alizitaja baadhi ya changamoto walizokutana nazo katika stesheni hiyo kuwa ni kutozwa huduma ya choo pamoja na kuzuiliwa kutumia maji katika kituo hicho.

"Tulianza safari yetu Dar es Salaam Julai 22 majira saa 9:00 alasiri na tulifika stesheni ya hapa Dodoma juzi majira ya saa mbili asubuhi na kushinda kutwa nzima huku tukikabiliwa na baadhi ya changamoto, "alisema.

Naye Sifa Ramadhani alisema tangu walipofika stesheni hiyo hakuna huduma yoyote waliyopewa na uongozi wa TRC na kuahidiwa kuwa wangepewa fedha za chakula lakini hawakutekeleza.

"Hakuna mtu aliyepanga tukwame hapa, lakini wangetujulisha ukweli kuwa safari yetu imekwama hadi muda fulani ili tufanye maarifa mengine maana wengine tuna watoto wadogo. Tungeweza kuwatafuta ndugu zetu hapa Dodoma Mjini tukapumzika huko kwa muda kwanza kuliko kupata shida hii," alisema.





Mkuu wa Idara ya Misitu na Mali zisizorejesheka kisiwani Pemba, Said Juma Hamad (kushoto), akitoa maelezo ya mazingira yaliyopo ya mashamba ya serikali Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar Balozi Seif Ali Idd. **PICHA: RAHMA SULEIMANI**

# Waonywa kutumia chokoleti 'sindano'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZAZI na walezi wametakiwa kuepuka kuwanunulia watoto wao chokoleti zilizotengenezwa mfano wa bomba la sindano kutokana na kuingizwa nchini kimagendo bila kuthibitishwa ubora na usalama wake kwa watumiaji.

Mkurugenzi wa Udhibiti Usalama wa Chakula wa Mamlaka ya Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA), Dk. Khamis Ali Omar, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mombasa Mjini Zanzibar, kuhusu uwepo wa bidhaa hiyo katika soko.

Alisema mwingizaji wa bidhaa hizo hakupita katika ofisi yake, hivyo bidhaa hizo bado hajizasajiliwa wala kupita katika maabara yao kujulikana ubora na usalama wake. Dk. Khamis alisema ZFDA kwa kushirikiana na vyombo vingine vya uchunguzi, inaendelea kumtafuta mfanyabiashara aliyeziingiza bidhaa hizo nchini kinyume cha sheria na akipatikana atafikishwa katika vyombo vya sheria.

"Jukumu la ZFDA kwa sasa ni kuziondoa katika soko kutokana na kutokidhi vigezo na wakati huo huo kwa kushirikiana na vyombo vingine, tunamtafuta mfanyabiashara huyo ili tumpeleke katika vyombo vya kisheria," alisema.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Usajili wa Bidhaa kutoka ZFDA, Khadija Ali Sheha, alisema bidhaa hiyo si halisi kwa vile haionyeshi hata kampuni au kiwanda kilichotumika kutengeneza.

Alisema katika vifungashio vya bidhaa hiyo, imeandikwa inatoka China lakini hakuna maelezo ya ziada kuelezea kiwanda kilichotumika na jimbo husika nchini China ili kufuatilia zaidi.

Kuhusu kifungashio chake, alisema bidhaa hiyo inamlaghai mtoto, hivyo inaweza kupelekea athari kubwa kwa watoto siku za mbele. "Kifungashio kinamlaghai mtoto lakini kinaweza pia kusababisha watoto hata kutumia mabomba ya sindano ya kawaida kutia maji au juisi wakaanza kutumia na mwisho kupata maambukizi mbalimbali," alisema Khadija.

Kutokana na hali hiyo, alisema tayari mamlaka inaendelea kuzichunguza bidhaa hizo katika maeneo tofauti ili zisiwapo katika soko. Mohamed Shadhil Shauri, Mkuu wa Ukaguzi wa Chakula ZFDA alisema tayari wamekagua maduka 25 ya mjini kazi hiyo itaendelea maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini.

Alisema kuna uwezekano wa bidhaa hizo kupitia katika bandari bubu au vituo vya forodha bila kufahamika vyema hasa kwa wale wafanyabiashara wanaochanganya bidhaa tofauti katika kontena moja.

Jumla ya maboksi 24 yenye chokoleti 600 tayari yamekamatwa katika maduka mbalimbali ili kuondolewa katika soko.

# SMZ kutoa uamuzi ukaguzi mashamba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa uamuzi baada ya kukamilisha uhakiki wa mashamba yote yaliyoko katika maeneo mbalimbali.

Amesema uamuzi huo pamoja na mambo mengine, utazingatia pia kuwapa wananchi ili wayaendeleze kwa kilimo hasa yale yaliyokosa usimamizi na kuyaendeleza kwa muda mrefu na kusababisha uzalishaji mdogo wa mazao ikiwamo karafuu.

Balozi Iddi alisema hayo juzi wakati akiendelea na ziara yake kisiwani Pemba akikagua mashamba yanayomilikiwa na serikali yaliyomo ndani ya Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema umefika wakati mashamba ya serikali yawe na uwezo kamili wa uzalishaji kama yalivyo ya watu binafsi na pale inaposhindikana kukosa huduma za usafishaji ni vyema ukaandaliwa utaratibu na taasisi zinazohusika kuwapa wananchi wale wenye nia ya kuyaendeleza kwa kilimo.

Alisema Serikali ya Zanzibar iko tayari kuridhia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuandaa utaratibu wa kutoa ajira kwa vijana ili yasafishwe mashamba yote ya serikali ambayo hukaa muda mrefu na kupoteza uzalishaji.

Balozi Iddi alisema usafishaji wa mashamba hayo utakaoongeza mapato ya taifa, lakini kwa upande mwingine fursa hiyo itatoa ajira kwa vijana watakaokuwa tayari kufanya kazi hiyo ya kizalendo ya kuokoa uchumi wa taifa.

Aliushauri uongozi wa Wizara ya Kilimo mbali na kufanya uhakiki utakaoongozwa na wakuu wa wilaya wa kuyatambua mashamba ya serikali, pia kuzingatia wananchi waliojitolea kuyasafisha baadhi ya mashamba hayo bila kushurutishwa. Makamu wa Pili wa Rais alisema uhakiki huo uwaandalie wananchi hao njia na namna ya kuandika maombi na kuyapeleka serikalini kupitia kwa masheha na wilaya zao yatakayotoa utaratibu wa kumilikishwa katika matumizi yake.

Akitoa ushauri wa kunawirishwa kwa mashamba ya serikali, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis, alisema ni vyema vikatumiwa vikosi vya SMZ wakiwamo watu wa Chuo cha Mafunzo katika usafishaji wa mashamba hayo.

Shamata alisema hatua hiyo ya dharura inaweza kusaidia kipindi hichi cha mpito kuelekea mafunzo ya msimu wa vuli ambao hutegemea kuzalisha mazao mengi hasa lile la uchumi wa taifa la karafuu.

# Awaonya walimu kuhusu unyanyasaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka walimu wa shule za sekondari kuwa na imani na lugha nzuri kwa wanafunzi wao ili wafanikiwe katika masomo yao.

Akizungumza na walimu wa shule za ukanda wa Magharibi na Mashariki Kielimu, katika ukumbi wa Suza Mchamdogo na Benjamin Kongwe, Wete, aliwataka kujirekebisha ili kuweka heshima na nidhamu katika fani ya ualimu.

Riziki alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wazazi ya baadhi ya walimu kuwatolea lugha chafu wanafunzi na hata kuwakatisha tamaa hali inayosababisha baadhi ya wanafunzi kuacha shule na kuzurura mitaani.

Pia aliwataka kushirikiana vyema na wazazi na kuwa na subira katika utendaji wa kazi zao pamoja na matatizo madogo yanayowakabili huku akiwahakikishia kuwa wizara inaendelea kuyatatua.

Aidha, aliwaomba kuzidisha bidii katika ufundishaji huku akiendelea kuwahakikishia kuwa Wizara ya Elimu itaendelea kuzinunua alama za ufaulu wa daraja la kwanza kwa kila somo kwa mwalimu yeyote atakayefaulisha alama hizo.

Waziri pia aliwahakikishia kuwa ataendelea kuwatetea walimu kwa Rais wa Zanzibar katika kuwaongezea maslahi kutokana na juhudi kubwa walizo nazo, huku akiwataka kuendeleza jitihada hizo ili kupiga hatua katika sekata la elimu nchini.

Kuhusu dhana ya baadhi ya watu kudai kuwa vyuo vya ualimu vimefutwa, waziri huyo alisema hakuna chuo kilichofutwa bali ni kukuzwa vyuo hivyo na kuingizwa katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ili kuongeza ufanisi wa ufundishaji kwa walimu katika ngazi mbalimbali. Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Idrissa Muslim Hija, alisema hakuna njia ya mkato katika kupata mafanikio na uongozi, hivyo aliwataka walimu kuwa wabunifu katika kazi, kutumia fursa zilizopo, bidii ya kazi na heshima. Alisema hali hiyo ndiyo itakayowawezesha kuonekana na kuweza kupata nafasi za juu za uongozi katika nchi.

## Wataka upandaji miti uwe endelevu

**Na Elizabeth Zaya**

VIONGOZI mkoa wa Geita na vijiji vinavyozunguka shamba la miti la Biharamulo mkoani humo wamewataka wananchi kupanda miti kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

Hayo yalisemwa na viongozi hao baada ya kutembelea shamba la miti Sao Hill mkoani Iringa, linalosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Walizuru eneo hilo kwa lengo la kujifunza shughuli mbalimbali za uendeshaji katika shamba hilo.

Kiongozi wa msafara huo ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mtemi Msafiri, alisema wameona ni vyema kujifunza katika shamba hilo kwa sababu ndilo shamba kongwe na kubwa zaidi miongoni mwa mshamba yanayosimamiwa TFS.

"Shamba la miti Sao Hill ndilo shamba kubwa zaidi kati ya mashamba yote ya serikali na ni nguzo ya maendeleo, na mkombozi wa mazingira wa Wilaya ya Mufindi na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini nasi tumeona ni vema tujifunze kutoka kwa wenzetu.

"Tumejionea jinsi shamba hili lilivyo kuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa sekta ya viwanda vidogo na vikubwa vya uchakataji wa mbao, linavyosaidia kuongezeka kwa ari ya upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira kwa wananchi wanaolizunguka," alisema Msafiri.

Aidha, alisema pia wameelezwa kuwa wananchi wa Wilaya za Mufindi, Kilombero na jamii jirani wamekuwa wakipatiwa gawio la asilimia tano ya mrabaha kila mwaka.

Alisema ni wazi shamba hili lina mchango mkubwa katika maendeleo, alisema Msafiri.

Mkurugenzi wa Rasilimali Misitu na Nyuki TFS, Zawadi Mbwambo, alisema shamba hilo limehamasisha kwa kiwango kikubwa upandaji wa miti kwa jamii inayolizunguka ambapo pia hutoa msaada wa mafunzo na miche ya miti kwa ajili ya kupandwa ili kupambana na uharibifu mkubwa wa misitu unaoendelea nchini.

"Takribani hekta 372,000 ya misitu inapotea kila mwaka na ili misitu hii isiweze kupotea tunatakiwa tuendelee kupanda angalau hekta 185,000 kwa mwaka kwa hapa Mufundi na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini," alisema Mbwambo.

Meneja wa Shamba la Miti la Biharamulo, Thadeus Shirima, alisema kupitia ziara hiyo anaamini kutakuwa na uelewa wa pamoja wa umuhimu wa shamba hilo katika kuleta maendeleo katika Kanda ya Ziwa na Tanzania nzima.

# Watumishi manunuzi wakumbushwa uadilifu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Ashatu Kijaji, amewaagiza watumishi wa serikali na wadau wanaohusika na zabuni za manunuzi kuwa waadilifu na wazalendo. Katika maagizo yake, waziri huyo aliwaagiza wajumbe wa Bodi za Zabuni, watendaji wa vitengo vya ununuzi, ukaguzi wa ndani na nje wa taasisi za serikali, kutanguliza uzalendo na uadilifu katika manunuzi ya umma.

Akizungumza jana jijini Arusha, katika uzinduzi wa kongamano la saba la mwaka la usimamizi wa umma lililoandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Dk. Ashatu alisema kwenye bajeti ya serikali zaidi ya asilimia 75 inatumia kwenye manunuzi ya umma hivyo kila mtaalamu awe mwadilifu.

"Eneo hili la manunuzi ni muhimu katika kutekelezwa miradi ya maendeleo, hivyo kila mtaalamu akiliheshimu na kutanguliza uzalendo na uadilifu taifa litafikia mipango yake yote iliyojipangia katika kufikia kiuchumi wa kati na uanzishwaji wa viwanda kabla ya mwaka 2025," alisema.

Dk. Ashatu alipongeza PPRA kwa kufanya ukaguzi kwenye taasisi za umma na kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 46 sawa na asilimia 23 ya taasisi zilizokaguliwa.

"Lakini lazima tujiulize kwanini tunasubiri kukaguliwa hiyo ni kukosa kulitendea haki taifa letu pia tunakosa uzalendo, hivyo kila mmoja ahakikishe anatimiza wajibu wake katika nafasi yake," alisema Naibu Waziri.

Aidha, aliagiza taasisi zote za umma kuhakikisha zinatumia mfumo wa kimtandao wa manunuzi (E Procurement) na hawatasita kuzifungia taasisi zisizotumia mfumo huo.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Mhandisi Leonard Kapongo, alisema kauli mbinu ya kongamano hilo ni: "Manunuzi katika miradi mikubwa kuelekea uchumi wa viwanda." Alisema uchumi wa viwanda utafikiwa endapo maofisa hao watazingatia sheria za manunuzi katika miradi mikubwa inayotekelezwa nchini.

Kapongo alisema PPRA ni muhimu katika kuisaidia serikali kutimiza malengo, kwani katika ukaguzi waliofanya karibuni katika manunuzi kwenye malipo ya makandarasi walibaini kufanywa malipo kinyume cha utaratibu na kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 46.

Alisema anaamini ukaguzi huo ungefanyika katika taasisi nyingi ungeokoa fedha zaidi ya hizo na kuwezesha serikali kutimiza malengo yake.

Aliongeza kuwa wameshindwa kukagua taasisi zote za umma, kutokana na changamoto ya ufinyu wa bajeti.

Kwa upande wake Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya PPRA, Profesa Sufian Bukurura, alisema taasisi ina upungufu wa wafanyakazi.

Alisema kwa sasa wapo 74 na mahitaji ni watumishi 152, hivyo aliomba serikali kuwaongezea wafanyakazi.

"Tukiongezewa bajeti na wakaguzi itatuwezesha kufanya ukaguzi zaidi ya taasisi 100 tunazofanya sasa kati ya taasisi 540, mfano sasa tumekagua taasisi 100 tukaokoa zaidi ya Sh. bilioni 46, je, tungekagua zote zilizopo tungeokoa zaidi," alisema.



Meneja Mauzo wa Kampuni ya Mbegu ya Seedco, Daniel Ulimboka (kulia), akifafanua juu ya mbegu za tikiti zinazozalishwa na kampuni hiyo katika maonyesho za teknolojia ya kilimo yaliyoandaliwa na Baraza la Nafaka la Afrika Mashariki, katika eneo la kituo cha utafiti wa kilimo cha Tari, Seliani jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Kahama kujengewa hospitali ya kisasa

**Na Mohab Dominick,**
KAHAMA

JUMUIYA ya Waislam ya Istiqaamah Muslim Community (IMCOT), inatarajia kujenga hospitali ya kisasa ya rufani katika Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga.

Hayo yamebainishwa juzi na Mwenyekiti wa Istiqaamah Wilaya ya Kahama, Aley Abeid, katika mkutano na wanahabari.

Alikuwa akizungumzia ujio wa Balozi wa Oman nchini Ally Abdallah Al-Mahruk wilayani humo.

Abeid alisema kuwa ziara ya Balozi wilayani Kahama ni kutembelea matawi ya Istiqaamah pamoja na kukagua maeneo yanayomilikiwa na taasisi hiyo ikiwamo eneo linalotarajiwa kujengwa hospitali ya kisasa, itakayohudumia watu wote bila kujali imani za dini zao.

Alifafanua kuwa miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa hospitali ya kisasa ambayo bado gharama yake haijabainishwa inayotarajiwa kuwa na vipimo vya kisasa na watajitahidi kuweka wataalamu wa magonjwa mbalimbali na kwamba wanachohitaji kwa sasa ni ushirikiano wa viongozi wa dini, pamoja na wa serikali ya wilaya na mkoa wa Shinyanga.

Alisema kuwa wamefikia uamuzi huo ili kuwaondolea adha wananchi ya kwenda katika hospitali za rufani kufuata matibabu ya magonjwa sugu na badala yake watahakikisha huduma zote zinapatikana katika hospitali hiyo. Sambamba na ujenzi wa hospitali hiyo kubwa, taasisi hiyo pia imedhamiria kujenga msikiti mkubwa wa kisasa wilayani Kahama utakaokuwa na ghorofa tano hadi sita kutokana na wilaya hiyo kutokuwa na msikiti mkubwa wenye uwezo wa kubeba waumini wengi kwa wakati mmoja. Aidha, utatumiwa pia nyakati za sikukuu na makongamano mbalimbali yanayowakutanisha pamoja Waislamu wengi na pia kumaliza tatizo la baadhi ya sala na dua kufanyikia viwanjani.

# Bobi Wine atangaza nia kumng'oa Museveni

**KAMPALA,** Uganda

MBUNGE wa Jimbo la Kyadondo Mashariki nchini Uganda, Robert Kyagulanyi 'Bobi Wine', ametangaza azma yake ya kuwania urais nchini humo 2021.

Ili kufanikisha nia yake hiyo, Wine amezindua kikosi kitakachoendesha kampeni yake ya kuwania urais 2021.

Umaarufu wake miongoni mwa vijana nchini Uganda umeonekana ni changamoto kwa Rais Yoweri Museveni ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 74 na anatarajiwa kuwania muhula wa sita madarakani.

**Ili kufanikisha nia yake hiyo, Wine amezindua kikosi kitakachoendesha kampeni yake ya kuwania urais 2021.**

Kwa sasa Wine, anakabiliwa na mashtaka ya uhaini baada ya kukamatwa mwaka jana akituhumiwa kuushambulia msafara wa Rais Museveni baada ya mkutano wa kisiasa.

Wine alieleza kuwa aliteswa na kupigwa akiwa mikononi mwa Jeshi la Polisi Agosti mwaka jana, tuhuma ambazo maofisa wa serikali wanazikana.

Mwanamuziki huyo ambaye hivi majuzi alijiunga na siasa amethibitisha kwamba atampinga Rais Museveni katika kinyang'anyiro cha urais kama mgombea huru na hivyo basi kumaliza uvumi uliokuwa ukienea kuhusu uamuzi wake.

Akizungumza na Gazeti la Finacial Times baada ya kufanya mahojiano na Shirika la Habari la AP, Wine alisema: "Tuliamua kwamba tutaupinga utawala huu, hivyo nitawania urais"

Aliliambia gazeti la Financial Times kwamba zaidi ya wabunge 50 wakiwamo 13 kutoka chama tawala cha Rais Museveni cha National Resistant Movement NRM waliunga mkono ugombeaji wake na hivyo kumpatia ujasiri wa kugombea kiti hicho. **BBC**



Waziri Mkuu mpya wa Uingereza, Boris Johnson (kushoto) akisalimiana na Malkia Elizaberth muda mfupi baada ya kutangazwa mshindi wa uchaguzi. **PICHA: AP**

# Boris kuunda serikali akiruhusiwa

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu mpya wa Uingereza, Boris Johnson, ataanza mchakato wa kuunda serikali yake baada ya kuapishwa rasmi na kupokea wadhifa wa Waziri Mkuu kutoka kwa mtangulizi wake, Theresa May.

Kiongozi huyo mpya wa chama cha Conservative atachukuwa rasmi hatamu ya uongozi baada ya kukutana na Malkia katika Ikulu ya Buckingham Palace.

Baada ya kuingia Downing Street, Boris anatarajiwa kutangaza sehemu ya baraza lake la mawaziri, ikiwa ni pamoja na Waziri wa Fedha na yule wa usalama wa ndani.

Vyanzo vya habari karibu na Boris vinaripoti kuwa viongozi wa ngazi ya juu watakuwa wale wanaoegemea uongozi wa Uingereza ya sasa.

Pia, anatarajiwa uchukua nafasi hiyo kuongeza idadi ya wanawake katika baraza la mawaziri na kuimarisha uwakilishi wa makundi ya jamii zilizotengwa.

Johnson alimshinda mpinzani wake Jeremy Hunt kwa kura 92,153 dhidi ya 46,656.

Katika hotuba yake baada ya ushindi huo, Meya huyo wa zamani wa mji wa London aliahidi kuwa ataiwasilisha Brexit, kuiunganisha nchi.

Akizungumza mjini London, alisema: "Tutaipa nchi nguvu.Tutaiwasilisha Brexit kufikia Oktoba 31 na kuchukua fursa zote zitakazotokana na muamko mpya. Tutajiamini upya na tutainuka upya na kuondosha shaka na fikra za kutojiamini." **BBC**

## Maambukizi mapya 14 yatangazwa

**KINSHASA,** Congo

WIZARA ya Afya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imetangaza maambukizi mapya 14 ya Ebola katika mkoa wa Kivu Kaskazini na Ituri.

Maambukizi hayo mapya yameripotiwa kutokea katika mji wa Beni, Mandima na Mutwanga.

Mbali na maambukizi hayo, watu wengine sita waliokuwa wameambukizwa virusi vya ebola wamefariki dunia.

Ugonjwa wa ebola umesababisha vifo vya watu zaidi ya 1,700 na wengine zaidi ya 2,000 kuambikizwa tangu Agosti 2018. **RFI**

# Kenya kutaifisha shirika lake la ndege

**NAIROBI,** Kenya

NI rasmi sasa mchakato wa kulitaifisha Shirika la Ndege la Kenya Airways (KQ) umeanza baada ya bunge la nchi hiyo kupitisha kwa pamoja ripoti ya kamati ya uchukuzi inayotaka serikali kusimamia shirika hilo.

Serikali ya Kenya inamiliki asilimia 48.9 ya hisa za shirika hilo ambalo limekuwa likipata hasara kila mwaka wa kifedha.

Hata hivyo wabunge wametofautiana kuhusu jinsi ya kulipa madeni ya KQ, baadhi wakisema wananchi walipa kodi hawastahili kugharamia makosa ya usimamizi yaliyofanywa na watu binafsi.

Kupitishwa kwa ripoti hiyo imemaamisha kuwa serikali ya Kenya italazimika kulipa madeni yote ya KQ kabla ya kutaifishwa.

Hatua ya kulitaifisha KQ inachukuliwa ili kulinusuru na madeni yanayoendelea kuongezeka.

Shirika la Air france - KLM, linamiliki asilimia 7.8 ya hisa za shirika hilo la ndege. Asilimia 38.1 ya hisa inamilikiwa na kampuni zinazoikopesha Kenya airways.

Kenya Airways ilipendekeza kusimamia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta (JKIA) kwa muda wa miaka 30, ili kuimarisha mapato yake, baada ya kupata hasara ya dola bilioni mbili mwaka 2017, mpango uliokataliwa na kamati ya bunge kuhusu uchukuzi.

Kamati ya bunge badala yake ilipendekeza kwamba shirika hilo litaifishwe, katika ripoti iliyowasilishwa bungeni Juni 18.

Kadhalika, wabunge wametaka wamiliki wa sasa wa hisa za shirika hilo wagharamie hasara. Pia wamekubaliana kwamba serikali itabeba mzigo wa kulipa madeni yote.

Kupitishwa kwa ripoti hiyo ni hatua inayotoa fursa ya kuanza kwa mchakato wa kuangazia maslahi ya wafanyakazi wa KQ ikiwamo kusawazisha kiwango chao cha mishahara na majukumu yao jinsi ilivyopendekezwa katika ripoti.

Kenya Airways, litapata msamaha wa kulipa kodi kwa muda maalum ili kuiwezesha kutekeleza shughuli zake bila matatizo ya kifedha.

Ripoti pia inapendekeza kwamba mamlaka ya safari za anga KAA, JKIA na KQ, viwekwe chini ya usimamizi mmoja.

Mwenyekiti wa shirika hilo, Michael Joseph, katika mahojiano na Shirika la Habari la Reuters alisema: "Utaifishaji ni muhimu sana ili tuweze kushindana kwa kiwango sawa. Sio tu tunachotaka, bali ni kitu tunachohitaji"

Alisema Shirika la ndege la Ethiopia limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu linasimamiwa na serikali. Hata hivyo, wasimamizi wa shirika la ndege la Air France –KLM, hawakuweza kupatikana wakati wa kutayarisha ripoti hiyo. **VOA**

# Mume afungwa jela miaka 2 kuua mke bila kukusudia

**Na Hellen Mwango**

Mhandisi Novat Kaberwa, amehukumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka miwili baada ya kukiri kosa la kumuua mke wake Clara Munishi bila kukusudia.

Kaberwa ambaye muda wote alikuwa akiangua kilio tangu apande kizimbani alisomewa hukumu yake jana mapema saa 4:20 asubuhi.

Hukumu hiyo ilitolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji iliyoketi chini ya Naibu Msajili Pamela Mazengo.

Akisoma hukumu hiyo, Msajili alisema mshtakiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza, lakini mahakama yake imeangalia madhara yaliyotokana na kusababisha kifo ni makubwa.

"Pamoja na kwamba mshtakiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza, mahakama yangu imeangalia mazingira ya utendekaji wa kosa na utetezi wa mshtakiwa kupunguziwa adhabu inamhukumu kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka miwili," alisema Msajili Mazengo wakati akisoma hukumu hiyo.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo Karani wa Mahakama hiyo, Evodia Kimario, alimsomea mshtakiwa mashtaka yake kuwa Januari 13, 2016 eneo la Keko Mwanga jijini Dar es Salaam mshtakiwa alimuua bila kukusudia Clara Munishi.

Mshtakiwa alikiri kosa hilo kwamba ni kweli alimuua mke wake bila kukusudia.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Justus Ndibalema, ulimsomea mshtakiwa maelezo ya kesi.

Ulidai kuwa mshtakiwa na Clara (kwa sasa marehemu) walikuwa mke na mume na waliishi kwenye nyumba yao Keko Mwanga.

Alidai kuwa Januari 13, mwaka huu, majira ya alasiri Veronica Munishi alikwenda nyumbani kwa Clara na mshtakiwa.

Ndibalema aliendelea kusoma maelezo hayo kwamba Veronica ni dada wa marehemu Clara, siku ya tukio walitoka nyumbani na saa 3:00 usiku walikutana na mshtakiwa eneo la makazi yao.

"Mshtakiwa alimshika Clara na kuanza kumshushia kipigo Veronica alifanikiwa kukimbia, lakini majirani na mdogo wa marehemu walijitokeza kuamulia ugomvi na mshtakiwa huyo alifanikiwa kutoroka," ulidai upande wa Jamhuri.

Upande huo wa Jamhuri uliendelea kudai kuwa majirani na mdogo wa Clara walimkimbiza kituo cha Polisi Chang'ombe, walipata fomu namba tatu na kumpeleka Hospitali ya Rufani Temeke.

Januari 14, 2016 Clara alifariki na uchunguzi wa daktari ulionyesha kwamba alikufa kutokana na damu kuvilia kulikosababishwa na kipigo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitoroka na alikamatwa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, Julai 15, 2016 na alifunguliwa mashtaka.

Mshtakiwa alikiri maelezo hayo kwamba ni kweli tukio lilitokea.

Msajili Mazengo alisema kwa kuwa mshtakiwa amekiri mashtaka na maelezo ya kesi, mahakama yake inamtia hatiani kwa kosa la mauaji ya bila kukusudia.

Upande wa utetezi ukiongozwa na jopo la mawakili watatu, Hashim Mziray, Venance Victor na Neema Kahakabuka, ulipewa nafasi ya kuwasilisha hoja za kuiomba mahakama kumpunguzia mshtakiwa adhabu.

Mzirai alidai kuwa mshtakiwa ni kiongozi wa familia inayomtegemea ya watoto wawili, wazazi na wadogo zake wote wanamtegemea.

Pia, mshtakiwa ni injinia aliyesomeshwa na serikali na kwamba kuna miradi imesimama kwa kuwa mshtakiwa yuko mahabusu, aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza.

"Mheshimiwa mshtakiwa amekiri kosa lake kwa kuwa hakutaka kuisumbua mahakama hii tukufu tunaomba apunguziwe adhabu," alidai Mzirai.

Msajili alisema baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili mahakama yake inamhukumu adhabu hiyo.



Mhandisi Novat Kaberwa, mshtakiwa aliyehukumiwa kwenda jela miaka miwili baada ya kukiri kosa la kumuua bila kukusudia mkewe, Clara Munishi. **PICHA: HELLEN MWANGO**

# Mwigizaji filamu Mexico asifia hifadhi za taifa

**Na Mwandishi Wetu**

MWIGIZAJI maarufu wa filamu kutoka Mexico, Leticia Calderon (51), amesifia rasilimali ya hifadhi za wanyama ambayo Tanzania imejaliwa kuwa nayo.

Mwigizaji huyo ambaye amefanya kazi hiyo kwa miaka 36, na ameigiza sinema maarufu ya ESMERALDA, yuko nchini kwa mapumziko ya siku saba kwenye hifadhi za wanyama za ukanda wa Kaskazini.

Akisalimiana na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliyekuwa mkoani Arusha kwa ziara ya kikazi, Calderon alisema amevutiwa na uzuri wa hifadhi za Tanzania na idadi kubwa ya wanyama aliowaona kwenye hifadhi za Taifa za Tarangire, Manyara na Ngorongoro.

"Kwa miaka mingi nilikuwa natamani sana kuja Tanzania kuona wanyama. Tuliyoyaona yametufurahisha mimi pamoja na wanangu. Nchi yenu ina uzuri wa kustaajabisha. Watu wenu ni wema na wakarimu," alisema Calderon.

"Ninafurahi kwamba ndoto yangu imetimia. Tulienda Tarangire, Manyara na Ngorongoro na sasa tunajiandaa kwenda Serengeti. Tulipokuwa Ngorongoro, tuliona simba wanne, majike wawili na madume wawili. Tumefurahi sana na nikirudi nyumbani, nitawaonyesha picha marafiki zangu na kuwaalika waje kutembelea Tanzania," alisema.

Mwigizaji huyo ambaye amefuatana na wanawe wawili Luciano Collado (15) na Carlo Collado (14), alisema wakimaliza mapumziko yao huko Serengeti watakwenda Masai-Mara kwa siku tatu na kisha wataelekea Paris, Ufaransa kumtembelea rafiki yake ambaye waliigiza filamu pamoja huko nyuma.

# Wavuvi 2 wafa maji kwa kuzamishwa na maharamia

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

WATU wawili wanasadikiwa kufa maji na wengine watatu kunusurika kifo baada ya mtumbwi waliokuwa wanatumia kuvua samaki kugongwa na watu wanaotuhumiwa kuwa ni maharamia na kisha kuwapora zana zao za uvuvi katika Ziwa Victoria, Wilaya ya Bunda mkoani Mara.

Kamanda wa Polisi mkoani Mara, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Juma Ndaki, jana alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa lilitokea usiku wa kuamkia Jumanne (juzi), katika eneo la kisiwa cha Nafuba, kilichoko ndani ya Ziwa Victoria.

Kwa mujibu wa Kamanda Ndaki, wavuvi hao waliokuwa na mtumbwi wa kutumia kasia wakiwa wanaendelea na shughuli zao za uvuvi na kugongwa na watu hao na kuzama majini.

Alisema wavuvi waliokuwa katika mtumbwi huo walizama majini na wawili hadi jana walikuwa hawajapatikana.

"Wakati wakiendelea na uvuvi ghafla mtumbwi uliokuwa na injini uliwagonga na kuzama majini," alisema Ndaki.

Diwani wa Kata ya Nansimo, Sabatho Mafwimbo, na Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Nafuba, Charles Nalambwa, walisema kuwa wavuvi hao walizamishwa na maharamia ambao waliwapora kokoro lao la dagaa.

Walisema, baada ya kuwateka na kuwapiga waliwazamisha majini na kisha kuwapora zana zao na kutokomea, huku wavuvi waliozamishwa majini wakibaki wakihangaika kujiokoa kwa kupiga yowe la kuomba msaada.

Vile vile, walisema wavuvi watatu waliokolewa na wenzao waliokuwa karibu na eneo hilo baada ya kusikia kelele za kuomba msaada.

"Baada ya kuwazamisha majini wavuvi hao waliogelea huku wakipiga kelele za kuomba msaada na wengine watatu wakafanikiwa kuokolewa na wavuvi wengine waliokuwa wakivua ndani ya ziwa hilo, lakini wawili wanaweza kuwa wamekufa maji kwa kuwa hadi sasa bado hatujawaona," alisema Diwani Mafwimbo.

Kamanda Ndaki aliahidi kuelezea tukio hilo leo baada ya kupata taarifa kamili kutoka kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Bunda.

Habari za uhakika kutoka eneo la tukio na kuthibitishwa na baadhi ya viongozi wa eneo hilo, zimewataja watu wanaodaiwa kufa maji kuwa ni pamoja na Deogratus Vumilia (28) na Makongoro Makunja (48), wote wakazi wa Kijiji cha Nambaza, wilayani Bunda.

Walionusurika kifo baada ya kuogelea na kuokolewa na wavuvi wenzao ni pamoja na Majura Malima (18) na Siri Kabuya (16), wakazi wa Kijiji cha Nambaza, wilayani Bunda na Mwenda Isack (28), mkazi wa Kijiji cha Kisorya, wilayani humo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA

YAKO KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



**Sehewa Kapingo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba P3648-0104,**


Kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Theoflo Ngowi.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: DAR/OST/122052019**

115339102

## KUPOTEA KWA CHETI



**LYDIA N. SONDE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0989-0018** kilichotolewa na **KIBARA SEKONDARI OCTOBER 2012.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:**

**MB/RB/2577/2019.**

115338902

## CHETI KIMEPOTEA



**FARIDA M. MUSSA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1343/0008** kilichotolewa na ANNE MARIE SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/GOG/RB/155291/2019.**

115340202

## KUPOTEA KWA VYETI



**Thadeus Fredrick** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo; cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1182-0072** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2004 katika shule ya Sekondari Ulyankulu, cheti cha kidato cha sita chenye **index namba P.0563-0767** Kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2008 katika kituo cha Tabora TTC centre, cheti Kilichotolewa na St. August University Tanzania mwaka 2012 chenye namba **LLB 8610,**Transcript na Cheti kuzaliwa chenye namba BD/NO0193865 vyeti vyote vimepotelea maeneo ya Kinondoni.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: DAR/OST/RB/156063/2019**

115339702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo: TANGA MJINI**
**Usimamizi wa Mirathi No. 99/2019**

**Ombi la MOHAMED A. KAJEMBE** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu SHABBIR ISMAIL MOHAMED


Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/07/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/07/2019.

115339502

## VYETI VIMEPOTEA



**LAWRENCE BONIFACE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0168-0024** kilichotolewa na **SANU SEMINARY** mwaka 1992. Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba P.0110-0517** kilichotolewa na ILBORU SEKONDARI mwaka 1996.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MAN/MBU/137547/2019.**

115339002

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HOME AFFAIRS**
**LOSS REPORT**
**MOR/IFA/RB/140294/2019**

**EVARIST LENGESAN MAKABE**
Reported to the police on 15/05/2019 that the under-mentioned property has been lost.
Type: Document.

Property name: Certificate of registration: 11476

215339602

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HOME AFFAIRS**
**LOSS REPORT**
**MOR/IFA/RB/142561/2019**

**EVARIST LENGESAN MAKABE** Reported to the police on 15/05/2019 that the under-mentioned property has been lost .

Type: Document.
Property name: Certificate of registration No. 2940

215339602

**IN THE COURT OF DISTRICT DELIGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE & ADMINISTRATION CAUSE NO 54 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late PASCHAL LISINDO MUGABE-DECEASED**

**And**
**In the matter of Application for letters of Administration PATRICK PASCHAL MUGABE**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

**Objections to the grant should be filed on or before 7th /08/2019.**

**Dated at Dodoma this 23/07/201**

215339302

**ELISHA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHURI LA KUKATA RUFAA NA. 4/2017**
**ELISHA MHIMBANO...............MLETA RUFAA**
**DHIDI YA**
**PENDO KINDANI**
**KW PENDO KINDANI ............WAJIBU RUFAA**
**POPOTE PALE WALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA MADAI RUFAA NA. 4/2017 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA - DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA:** shauri tajwa hapo juu litasikilizwa mahakama kuu ya Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya MHE: JAJI L. MLACHA, wa Mahakama kuu ya Tanzania DODOMA saa tatu(3:00) kamili asubuhi siku ya jumatatu 19/8/2019

**HIVYO:** unatakiwa ufike wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** hatafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itavyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 28/11/2018.

215339402

## Eneo la biashara (Yard Plot) mita za Mraba 2,723 linauzwa.

Eneo (yard) Lina hati miliki, Kuna maji na umeme pia.

Eneo lipo Msamvu Morogoro, kandokando ya barabara ya Iringa, karibu na BM Garage

Eneo linafaa kwa matumizi ya kiwanda, maegesho ya malori, Hoteli, Hostel, maofisi, maghala n.k,

**Kwa mawasiliano:**
**godlisten.minja@greenresources.no**
**+255 714 432 979**

215338701

## VIWANJA VINAUZWA

Viwanja vifuatavyo ambavyo vipo kwenye eneo moja na vina Hati Halali vyenye jumla ya Mita za **mraba 12,169 vinauzwa.**

Ukubwa wa viwanja hivyo 4 ni kama ifuatavyo:-

1. **2,760 sqm**
2. **2,406 sqm**
3. **3,564 sqm**
4. **3,439 sqm**

Viwanja vipo eneo la Mbezi, Halmashauri ya Kinondoni.

**Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na namba +255 655 131 074**

615326202


NJOO UTANGAZE BIDHAA

YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# NEWCASTLE YAMSAJILI JOELINTON

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle hatimaye imefanya usajili wake wa kwanza kipindi hiki cha majira ya joto kwa kutangaza kumsajili mshambuliaji kutoka Hoffenheim, Joelinton kwa ada ya euro milioni 40 na amesaini mkataba wa miaka sita.

Mchezaji huyo raia wa Brazil ni usajili wa kwanza kwa kocha Steve Bruce tangu achukue mikoba ya kuinoa klabu hiyo kutoka kwa Rafa Benitez.

Mara baada ya kutua hapo Newcastle, mchezaji huyo alisema kwamba anajisikia furaha kujiunga na timu hiyo na kwamba atahakikisha anacheza kwa kwa bidii kuipaisha klabu hiyo.

"Nina furaha kubwa kuwa hapa. Najua kwamba klabu imefanya uwekezaji mkubwa kwangu na hivyo nina majukumu makubwa. Kwa uhakika nimehamasika na nitajitahidi kwa hali na mali."

Naye kocha, Bruce alisema: "Huyu ni mchezaji anayenivutia. Ni mchezaji kijana ambaye nimefurahia kumpata, kwani atakuwa nasi kwa muda mrefu .

"Amekuwa na wakati mzuri kule Ujerumani na naamini atakuwa na msaada mkubwa kwenye kikosi chetu kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu.

Joelinton alifurahia msimu 2018/19, akifunga mabao saba na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 28 alizocheza kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na atakuwa mbadala wa washambuliaji, Ayoze Perez, Joselu na Salomon Rondon ambao wameondoka.

Perez alijiunga na Leicester mapema Julai hii kwa ada ambayo haikutajwa, huku Joselu amekwenda Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, katika klabu ya Alaves na Rondon akiwa amekwenda nchini China kujiunga na Dalian Yifang ambayo inanolewa na Benitez.

Newcastle ilimaliza Ligi katika nafasi ya 13 kwenye Ligi Kuu msimu uliopita.

## Aston Villa yamsajili Trezeguet

**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imethibitisha kumsajili Mahmoud Hassan ambaye anajulikana zaidi kwa jina la Trezeguet kwa ada ya awali ya pauni milioni 8.5 kutoka timu ya Kasimpasa ya nchini Uturuki.

Sky Sports imeripoti kuwa Villa imefikia makubaliano ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 na bei yake itaongezeka kutokana na namna kiwango chake kitakavyopanda.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri, ambaye aliichezea mechi nne timu yake ya taifa kwenye michuano ya mataifa ya Afrika, Afcon, ni mchezaji wa nane kusajiliwa na Villa kipindi hiki cha majira ya joto.

"Kwa uhakika tumefurahi kumsajili Trezeguet. Nimemshuhudia mara nyingi tu," amesema kocha Dean Smith akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Ni aina ya mchezaji ambaye tulikuwa tukimhitaji, ambaye anaweza kuwa mtatuzi wa kufunga mabao kwa timu yetu."

Trezeguet ameungana na Wesley, Tyrone Mings, Matt Targett, Ezri Konsa, Anwar El Ghazi, Bjorn Engels, Jota na Kortney Hause hapo Villa Park baada ya kupanda Ligi Kuu msimu uliopita.

Winga huyo alianza kucheza soka la kulipwa katika klabu ya nyumbani kwao Misri, Al Ahly kabla ya kusajiliwa na Anderlecht na baadae Mouscron ya Ubelgiji na akahamia Uturuki kabla ya kutua Ligi Kuu ya England.



## Klopp: Liver haitatumia fedha nyingi kusajili



**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp amesema kwamba Liverpool bado iko sokoni kwa ajiili ya kusaini wachezaji wapya, lakini amebainisha hawatatumia kiasi kikubwa cha fedha.

Klopp bado hajaongeza mchezaji yoyote katika kikosi chake msimu huu zaidi ya beki kinda wa Uholanzi, Sepp van den Berg. Manchester City na Tottenham zote zimevunja rekodi zao za usajili kipindi hiki cha majira ya joto, lakini Klopp amesema kuwa hana hofu ya Liverpool kutoongeza wachezaji wapya na amesisitiza kuwa ana furaha na kikosi chake.

"Sio rahisi," amesema Klopp akiiambia televisheni ya Liverpool. "Nilisema mwaka jana kwamba, kuimarisha timu sio kitu rahisi. Hatuwezi kutumia fedha nyingi, ingawa bado tupo sokoni.

"Sisi sio klabu ambayo inatumia fedha nyingi. Hatuwezi kufanya hivyo. Ni ukweli kwamba ni matajiri, lakini hatuwezi kufanya kama wengine wanavyofanya. "Lakini bado tupo sokoni. Tutaangalia nini cha kufanya, lakini kikosi changu bado kipo imara.

"Kuna wakati mwingine kusajili wachezaji wapya siyo suluhisho, tuna wachezaji wengi kikosini mwetu na wao ndio wanatakiwa kuwa suluhisho letu."

## HABARI MICHEZO

# Madrid wakomaa na Pogba

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid wapo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 150 kwa ajili ya kumsajili Paul Pogba na pia wapo tayari kumpa mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki.

Mchezaji huyo wa Manchester United amekuwa katika rada ya Real Madrid ambayo kwa sasa ipo chini ya kocha, Zinedine Zidane kwa muda mrefu na imefahamika kuwa mkakati wa kumnasa nyota huyo ni kama unakwenda sawa kwa sasa.

Tatizo lililopo ni kwamba Real hawawezi kulipa mishahara miwili kwa Gareth Bale na Pogba kwa wakati mmoja, hivyo ni lazima wamuuze nyota wa Wales ndipo wamnase Bale.

Msimu huu Zidane, ameshawanunua wachezaji watano katika dirisha la usajili linaloendelea na amemfanya Pogba kuwa namba moja katika jitihada za usajili.

Katika siku za karibuni kulikuwa na habari kwamba Pogba amekalishwa chini na viongozi wa Manchester United na kumtuliza lakini taarifa kutoka kambini kwake zinasema kuwa mchezaji huyo bado ana mpango wa kutua Hispania.

Katika hatua nyingine, Bale, yuko katika kikosi cha Real huko Amerika Kaskazini kwa ajili ya mechi za kujiandaa na msimu na habari mbaya ni kwamba haelewani na kocha wake Zidane.






# HUDSON-ODOI KUSAINI MIAKA 5 CHELSEA

**LONDON,** England

CALLUM Hudson-Odoi anatarajia kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na Chelsea, kwa mujibu wa ESPN FC.

Mshambuliaji huyo kinda yupo kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake na ofa nne zilizotolewa na Klabu ya Bayern Munich zilikataliwa na sasa atabakia hapo Stamford Bridge.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England atasaini mkataba huo ambao utamfanya alipewa pauni 180,000 kwa wiki, huku kukiwa pia na uwezekano wa kuongezeka hadi pauni 200,000 kwa wiki.

Ofa ya mwisho ya Bayern kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 ilitolewa Januari mwaka huu ya pauni milioni 35.

Hudson-Odoi amekubali kusaini mkataba mpya baada ya kushawishiwa na kocha wa sasa, Frank Lampard ambaye amemwambia kwamba yupo kwenye mipango yake ya baadae.

Kocha wa zamani wa Chelsea, Maurizio Sarri alikuwa hampi nafasi ya kucheza Hudson-Odoi na hivyo kuibua uvumi kwamba mchezaji huyo angeondoka kipindi hiki cha majira ya joto.

# *Bondia afariki dunia baada ya kichapo*

**MOSCOW,** Urusi

BONDIA raia wa Urusi, Maxim Dadashev, amefariki dunia baada ya pambano lake na Subriel Matias kumsababishia majeraha makubwa ya ubongo.

Dadashev mwenye miaka 28, alishindwa kutembea mwenyewe baada ya pambano hilo ambalo kocha wake, Buddy McGirt alilazimisha lisimamishwe katika raundi ya 11 baada ya bondia huyo kupokea kichapo kikali bila majibu.

Pambano hilo lilipigwa Ijumaa wiki iliyopita na punde tu baada ya pambano hilo, Dadashev alikimbizwa hospitali. Madaktari waligundua kuwa damu ilikuwa ikimvuja kwenye ubongo na kufanyiwa upasuaji wa haraka, lakini akafikwa na umauti juzi Jumanne.

Shirikisho la ndondi la Urusi limesema tayari uchunguzi umeshafuguliwa juu ya mkasa huo. Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Umar Kremlev amedai kuwa kulikuwa na aina fulani ya uvunjwaji wa taratibu.

"Tutaiunga mkono familia yake, ikiwemo kifedha. Tutakamilisha uchunguzi wa kuangalia mazingira ya pambano, tunahitaji kujua ukweli wa kilichotokea.

"Hili linaweza kutokea kwenye mchezo wowote. Naamini kuna mapungufu ya kibinadamu yamechangia kuwapo na aina fulani ya uvunjwaji wa taratibu," alisema Umar.


Dadashev ambaye alikuwa akifanya shughuli zake za masumbwi nchini Marekani alishinda mapambano yake yote 13 aliyoyacheza kabla.

Ijumaa alipambana na Matias kutoka Puerto Rico katika jimbo la Maryland ambapo alisukumiwa makonde mazito na kwa kasi kali.

Kocha McGirt alieleza kuwa baada ya pambano alishindwa kumshawishi kukubali kushindwa, lakini akaamua kurusha taulo ulingoni baada ya kuona akipigwa zaidi za zaidi kwa makonde ya wazi kadri pambano lilivyokuwa likiendelea.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MAN YAINOA INTER USAJILI WA LUKAKU

**Yataka ifanye haraka muda unakimbia...**

**SHANGHAI,** China

KLABU ya Manchester United imeitaka Inter Milan kuharakisha mpango wao wa kumsajili mshambuliaji wake, Romelu Lukaku kwa sababu muda unakimbia.

**Inter ilitoa ofa ya pauni milioni 54 za kumsajili mshambuliaji huyo, lakini zilikataliwa na sasa wanajipanga kutuma ofa nyingine kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.**

United, ambao wanataka ada ya pauni milioni 90 ambazo ziliwagharimu wakati wakimnunua Lukaku kutoka Everton miaka miwili iliyopita, wanataka kutumia fedha hizo kununua mchezaji mwingine kama akiuzwa.

Huku usajili wa wachezaji kwa Ligi Kuu ya England ukiwa inafikia tamati Agosti 8 mwaka huu, ina maana kwamba, Inter wamebakiwa na wiki mbili tu za kuhakikisha wanamsajili mshambuliaji huyo.

Ingawa mwisho wa usajili kwa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, unafungwa Agosti 23, United imeiambia Inter wanatakiwa kufanya haraka ili wao wapate nafasi ya kumsajili mchezaji mwingine kama wakimuuza Lukaku.

Imeripotiwa kwamba, Solskjaer hawezi kuanza msimu mpya wa Ligi akiwa anamtegemea Marcus Rashford pekee kama mshambuliaji wao wa mbele, kwani anataka kusajili mchezaji mwingine.

Anthony Martial anaonekana wazi kwamba hawezi kuwa mchezaji muhimu wa kucheza mara kwa mara, lakini United wanajua kwamba hawataweza kumtegemea kinda Mason Greenwood pekee licha ya kuonyesha kiwango kizuri katika mechi za mandalizi ya msimu mpya.

Man United imeshabainisha wazi kwamba kama Lukaku atauzwa wanataka kumsajili Nicolas Pepe kutoka klabu ya Lille ya Ufaransa.

United pia inatarajia kumsajili Harry Maguire ingawa Leicester City wanataka kiasi cha pauni milioni 80 ili kuweza kumuachia beki huyo.

## ZISIKUPITE

### PSG WAIPIKU JUVENTUS

KLABU ya Paris St-Germain wameishinda Juventus katika kinyang'anyiro cha kumsaini mlinzi wa Tottenham, Danny Rose mwenye umri wa miaka 29, na wanaamini watafikia mkataba wa pauni milioni 20 kumsajili kiungo huyo wa kimataifa wa England. ***(Sun)***

### TOTTENHAM KUONGEZA BEI

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy, yuko tayari kuongeza bei ya Toby Alderweireld kutoka pauni milioni 30 hadi pauni milioni 40 ikiwa mkataba unaodhibiti uhamisho wa mchezaji huyo raia wa Ubelgiji utafikia kikomo chake Ijumaa hii. ***(Telegraph)***

### MAN KUINGIA SOKONI KUSAJILI

MAKAMU Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward yuko mbioni kushughulikia suala la usajili wa wachezaji wapya, zikiwa zimesalia wiki mbili kabla ya muda wa mwisho wa uhamisho wa wachezaji kukamilia. ***(ESPN)***

### MAGUIRE AKARIBIA KUTUA UTD

KLABU ya Manchester United ina matumaini ya kukamilisha mchakato wa usajili wa mlinzi wa timu ya taifa ya England na klabu ya Leicester City, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 26 na mchezaji wa safu ya kati wa Newcastle Sean Longstaff mwenye umri wa miaka 21. ***(London Evening Standard)***

### UNAI ATOA WIKI MBILI

KOCHA wa Arsenal Unai Emery ana wiki mbili kuamua ikiwa atamuachilia winga wa England wa chini ya miaka 21, Reiss Nelson kujiunga na Hertha Berlin kwa mkopo msimu ujao. ***(Sun)***

### CELTIC KUTETA NA TIERNEY

KOCHA wa Celtic, Neil Lennon, anatarajia kufanya mazungumzo na beki wa Scotland Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 22, baada ya ofa ya tatu ya Arsenal ya kumnunua mchezaji huyo kukataliwa. ***(Daily Record)***

### SPURS YAMKARIBIA CELSO

KLABU ya Tottenham wanakaribia kumsaini kiungo wa kati wa Real Betis, Muargentina Giovani lo Celso, 23, kwa kima cha pauni milioni 45. ***(Sun)***

### FERNANDES HAONDOKI LISBON

NYOTA wa Sporting Lisbon na Ureno Bruno Fernandes, 24, amesema kuwa ataendelea kucheza katika ligi kuu ya Ureno licha ya tetesi zinazomhusisha na uhamisho wa kwenda Manchester United. ***(Mirror)***

### YAWEKA NGUMU KWA EJARIA

LIVERPOOL haitamruhusu kiungo wa kati wa England mwenye umri wa chini ya miaka 21, Ovie Ejaria kuondoka klabu hiyo kwa mkopo msimu huu, lakini wako tayari kumuuza mchezaji huyo. ***(Daily Mail)***

### ADARABIOYO KUTUA B'BURN



MLINZI wa Manchester City, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye msimu uliopita alikuwa West Brom kwa mkopo, anajiandaa kujiunga na Blackburn. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

## JKT Tanzania kucheza mechi 10 Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya JKT Tanzania, Abdallah Baress, amesema timu yake itacheza mechi 10 za kirafiki ikiwa ni mandalizi ya Ligi Kuu Tanzania bara, ingawa bado hajajua ni timu gani watacheza nayo.

Kikosi cha JKT Tanzania kiliwasili jana visiwani Zanzibar kwa kuweka kambi ya kujiandaa na ligi kuu ya Tanzania Bara itakayoanza mwezi ujao.

Kikosi hicho chenye wachezaji 28 kinatarajia kuweka kambi ya mwezi mmoja visiwani na kucheza mechi za kirafiki katika kujiandaa na ligi.

Hata hivyo, alisema katika mechi hizo anapanga kucheza na timu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar pamoja na timu nyengine za madaraja ya wilaya na taifa.

"Mechi tutakazocheza za kirafiki ni 10, timu zozote zile ambazo nitazipata ila zikiwemo na zile za zinazoshiriki Ligi Kuu," alisema.

Alisema timu hiyo itakuwa ikifanya mazoezi mara mbili kwa siku katika uwanja wa Amaan au Mao Tse Tung itategemea na uwanja ambao wataupata. Hata hivyo alisema kuwa kwa kuanzia watakuwa na program ya kufanya mazoezi katika Pwani ya Kizingo nyuma na klabu ya Timu ya soka ya KMKM.

## Mavunde mgeni rasmi muziki wa Kigogo

**Na Sabato Kasika**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Anthony Mavunde, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika tamasha la muziki wa Kigogo.

Tamasha hilo lenye lengo la kuonyesha utekelezwaji wa utamaduni wa Mtanzania, linalotarajia kuanza kesho kwenye viwanja vya Chamwino, jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa tamasha hilo, Dk. Kodman Mapana alisema jana kuwa pamoja na naibu waziri huyo na wadau mbalimbali wa mambo ya sanaa na utamaduni wanatarajia kuhudhuria.

"Tamasha hilo litasindikizwa na makundi zaidi ya 30 na wadau wengine kutoka nchi mbalimbali na pia kutakuwa na matukio mengi ambayo yatashirikisha wanafunzi," alisema Mapana.

Mapana ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Sanaa za Ubunifu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema wanafunzi watakaoshiriki kwenye tamasha hilo ni wa kuanzisha shule za msingi hadi chuo kikuu.

"Wito wangu ni kwamba watu wajitokeze kwa wingi kwenye viwanja vya Chamwino ili wajionee utekelezwaji wa utamaduni wa Mtanzania unavyofanywa na wasanii waliosheheni vipaji," alisema.

# JUMA ABDUL AIGOMEA YANGA KISA MSHAHARA

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa Klabu ya Yanga, Juma Abdul amesema ameshindwa kujiunga na kambi ya timu hiyo inayoendelea mkoani Morogoro, kwa sababu uongozi wa Klabu hiyo umeshindwa kumlipa mishahara yake.

**Akizungumza na Nipashe jana, Abdul alisema hawezi kuingia kambini wakati familia yake inakufa njaa.**

"Mimi kweli sipo kambini, siwezi kujiunga na timu wakati familia yangu inakufa njaa,"alisema Juma.

Aliongeza kuwa endapo wakimlipa ataendelea na majukumu yake kama kawaida na kudai mpira ndio kazi yake.

"Wakinilipa haki yangu nitaendelea na majukumu kama kawaida kwa sababu ninajiamini nina uwezo mzuri,"alisema mchezaji huyo.



Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza akirusha mpira kuashiria ufunguzi wa mashindano ya mpira wa Wavu kitaifa yanayofanyika mkoani Morogoro juzi. **PICHA: MAELEZO**



# *Nyoshi atoa somo bendi za dansi*

**Na Sabato Kasika**

RAIS wa bendi ya muziki wa dansi inayokuja kwa kasi ya Bogos, Nyoshi El-Sadaat amezitaka bendi zisikate tamaa na badala yake zikaze buti, kwa madai kwamba soko bado limebana.

"Kukata tamaa ni kukubali kushindwa, hivyo jambo la msingi ni kukaza buti na kuendelea kukomaa, kwani ipo siku muziki wa dansi utarudi kwenye levo kama zamani," alisema Nyoshi.

Nyoshi ambaye bendi yake hiyo inaundwa na sehemu kubwa ya wanamuziki vijana, aliliambia gazeti hili jana kuwa kikosi chake kiko imara na kinaendelea kutoa burudani kama kawaida bila kuyumba.

Alisema, siri ya mafanikio ni kupambana, hivyo anawashauri wanamuziki wa bendi nyingine kuzingatia hilo ili waendelee kutoa burudani lakini pia wakitunga nyimbo ambazo zinaweza kurudisha bendi zao kwenye soko.

"Katika mafanikio hakuna njia ya mkato, tuendelee kukomaa tu ipo siku kitaeleweka na tutafanya maonyesho makubwa kama zamani, ila tukumbuke kuwa hakuna mafanikio yasiyo na changamoyo," alisema.

Alisema, kwa sasa ni kama muziki wa dansi umelala, kwa madai kwamba baadhi ya bendi hazifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa mashabiki hali ambayo inaonyesha kuwa mambo siyo mazuri.

# Michezo

Alhamisi Julai 25, 2019

Nipashe




## Man yainoa Inter usajili wa Lukaku

UKURASA 30



Wachezaji wa Simba wakiwa kwenye mazoezi katika kambi yao waliyoweka nchini Afrika Kusini, kwa ajili ya maandalizi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa. **PICHA: MTANDAO**

# *Yanga kuivaa Kariobangi kilele wiki ya Mwananchi*

## ● ● ● Ni baada ya AS Vita kuchomoa...

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Yanga itacheza dhidi ya Kariobangi Sharks ya Kenya Agosti 4 mwaka huu kwenye uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam katika kilele cha Wiki ya Mwananchi.

**Wiki hiyo ya Mwananchi iliyopewa jina la 'Kukusanya Kijiji' kilele chake kinatajiwa kuhitimishwa Agosti 4, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na Waandishi wa Habari jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredirick Mwakalebela, alisema kuwa wanacheza na Kariobang baada ya AS Vita ya DR Congo kuomba hudhuru baada ya kuingiliwa na ratiba ya Caf.

Mwakalebela alisema baada ya kupokea barua hiyo ya udhuru haraka wakazungumza na Kariobang na kukubali kuja nchini kucheza mchezo huo.

"Maandalizi ya Wiki ya Mwananchi yanakwenda vizuri na siku hiyo tunatarajia kucheza mchezo mmoja wa kirafiki dhidi ya Kariobang ambao walitufunga kwenye michuano ya SportPesa Super Cup.

"Hivyo mchezo huo kwetu tunauchukulia wa umuhimu kwa ajili ya kulipa kisasi," alisema Mwakalebela.

Kwa upande wa katibu wa Kamati ya Maandalizi ya wiki hiyo ya Mwananchi, Deo Mutta alisema kuwa uzinduzi wa Wiki ya Mwananchi utafanyika Julai 27 mwaka huu kwa baadhi ya wanachama wa Yanga kwenda Zanzibar kutembelea kaburi la mwasisi wa klabu hiyo na Rais wa kwanza wa Zanzibar, Abeid Karume na baada ya hapo jioni watacheza mchezo wa kirafiki wa wanachama.

# Simba ni mwendo wa vichapo tu

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Simba imeendeleza ubabe katika mechi zake za kujiandaa na msimu mpya baada ya jana kuwachapa wenyeji, Platinums Stars FC mabao 4-1 mjini Rusternburg, Afrika Kusini.

Clatous Chama raia wa Zambia alifunga mabao mawili dakika za 11 na 58, wakati mabao mengine yamefungwa na viungo wenzake, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman kwa penalti dakika ya 13 na Muzamil Yassin dakika ya 87, wakati la Platinums Stars FC limefungwa na Ruele Modise dakika ya 75 kwa penalti pia.

Huo ni mchezo wa pili mfululizo katika kambi yake ya Rusternburg kujiandaa na msimu mpya baada ya jana kuichapa 4-0 timu ya Chuo Kikuu cha Orbit Tvet, mabao ya nahodha na mshambuliaji tegemeo, John Raphael Bocco dakika ya tisa na 28, kiungo Hassan Dilunga dakika ya 23 na mshambuliaji mpya, Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino ya Daraja la Nne kwao, Brazil dakika ya 30.

Baada ya mchezo wa jana Simba itateremka tena uwanjani Jumamosi kumenyana na Township Rollers ya Botswana kabla ya kukamilisha ziara yake kwa kucheza na Orlando Pirates ya Johannesburg Julai 30, mechi zote zikipigwa Rusternburg.

Simba watacheza na Power Dynamos ya Zambia Agosti 6 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, katika mchezo wa kirafiki kwenye Tamasha la Simba Day. Simba wataanzia ugenini dhidi ya UD do Songo ya Msumbiji kati ya Agosti 9 na 11 kabla ya kurejea nyumbani kwa mchezo wa marudiano kati ya Agosti 23 na 25.

# Ligi Kuu Bara kupata mdhamini mpya

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kukaa muda mrefu bila kuwa na mdhamini wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) linatarajia kutangaza mdhamini wa ligi hiyo msimu ujao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kumaliza mkutano na Waziri Mwakyembe Rais wa Shirikisho hilo, Wallace Karia, alisema wanatarajia kumtangaza mdhamini huyo kabla ya Agosti 15 mwaka huu.

"Mwezi ujao tunatarajia kumtangaza mdhamini wa Ligi Kuu msimu ujao mazungumzo yakikamilika tutamtaja mdhamini tuliyempata," alisema Karia.

Alisema hawakurupuki kuchukua mdhamini bali wanachukua mdhamini anayeendana na hadhi ya ligi yetu.

Aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi katika mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Wachezaji wa Ndani (CHAN) kati ya Taifa Stars na Harambee Stars ya Kenya Jumapili ya Wiki hii jijini Dar es Salaam.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >